# Nipashe

Ijumaa Oktoba 18, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580052

www.ippmedia.com


MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US







## Muuguzi atoroka kazini kwa tuhuma kumbaka mgonjwa

UKURASA 10

UKURASA 13

# Kompyuta za DPP zaibwa



• **Zinadaiwa** kuwa na kumbukumbu za kesi za uhujumu uchumi, taarifa za fedha zilizolipwa...*Endelea uk. 2*



## Kigogo sekta binafsi matatani

UKURASA 3

Wananchi, waendesha pikipiki wakipita kwa shida kwenye maji ya mafuriko katika Barabara ya Morogoro, eneo la Jangwani, jijini Dar es Salaam kutokana na mvua kubwa iliyonyesha jana. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store




## Sheria kuruhusu uchangiaji figo

UKURASA 2

**MICHEZO** WABRAZIL SIMBA WATISHA MCHANGANI UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Wanafunzi 30,000 wapewa mikopo bil. 113/-

**Na Beatrice Shayo**

BODI ya Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) imetangaza awamu ya kwanza yenye wanafunzi 30,675 ambao watapata mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 113.5.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, aliwaambia waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana kuwa wanafunzi wa awamu ya kwanza kwa mwaka wa masomo 2019/20 waliopewa mikopo ni 30,675. Kati ya hao, alisema wanamume ni 19,632 (asilimia 64) na wanawake ni 11,043 sawa na asilimia 36.

Alisema katika mwaka huu wa masomo, serikali imetenga Sh. bilioni 450 zinazolenga kuwanufaisha wanafunzi 128,285 wakiwamo 45,000 wa mwaka wa kwanza na wengine 83,285 ni wanaoendelea na masomo. Badru alisema mwaka 2018/19 fedha zilizotengwa na kutolewa zilikuwa Sh. bilioni 427.5 na ziliwanufaisha wanafunzi 123,283 wakiwamo 41,285 wa mwaka wa kwanza. Pia alisema waombaji wa mikopo wanatakiwa kufungua akaunti binafsi walizotumia na kuomba mkopo ili kupata taarifa za mikopo.

Alisema orodha kamili ya wanafunzi hao inapatikana katika tovuti ya bodi (www.heslb.go.tz) na itatumwa vyuoni ili kuwawezesha kufanya usajili na kuendelea na masomo.

"Pamoja na tovuti, wanafunzi wanaweza kufungua akaunti zao walizoombea mkopo mtandaoni na kuona walivyopangiwa na tunaanza kupeleka fedha kesho (leo) kwa kuwa serikali imeshatukabidhi Sh. bilioni 125 ambazo tuliomba kwa malipo kati ya Oktoba na Desemba mwaka huu," alisema Bandru. Mkurugenzi huyo alisema HESLB inakamilisha awamu ya pili ambayo itatangazwa kabla ya mwisho wa wiki ijayo na fedha za watakaopewa vyuoni kabla ya vyuo kufunguliwa.

"Baada ya kukamilisha uchambuzi wa maombi ya mikopo kutoka kwa wanafunzi waliochelewa kukamilisha taratibu za udahili au kuchelewa kurekebisha maombi yao ya mkopo mtandaoni, tutatangaza majina yao," alisema.

Kuhusu makundi maalumu yenye uhitaji, alisema katika orodha ya awamu ya kwanza wako wanafunzi 6,142 ambao ni yatima au wamepoteza mzazi mmoja, wenye ulemavu ni 280 na wengine 277 wanaotoka katika kaya zinazofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf).

Badru aliwataka wanafunzi waliomba mikopo kuwa watulivu na kuendelea kufuatilia vyombo vya habari na akaunti zao ili kupata taarifa mbalimbali kuhusu uombaji wa mikopo na wanapokuwa na maswali wawasiliane na bodi kupitia namba za simu zinazopatikana katika tovuti.

# Kigogo sekta binafsi matatani

**Na Dege Masoli,** KOROGWE

MFANYABIASHARA nchini, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Taasisi ya Sekta Binafsi Tanzania (TPSF), Salum Shamte pamoja na vigogo wa Kampuni ya Katan LTD, wamekamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Tanga wakihusishwa na upotevu wa zaidi ya Sh. bilioni 54, zikiwamo za serikali.

Kukamatwa vigogo hao ni agizo la Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigella kwa Kamanda wa Polisi mkoani Tanga, Edward Bukombe na Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) mkoa, Christopher Mariba.

Kamanda wa Bukombe aliwataja waliyokamatwa kwenye mkutano huo sambamba na Shamte ni Mkurugenzi

Mtendaji wa Katan Ltd, Juma Shamte, Fadhil Mhina ambaye ni mhasibu wa Katan Ltd, Fatma Diwani mkurugenzi na Theodora Mtegeti Ofisa Mahusiano.

Shigela alitoa agizo hilo baada ya kupokea ripoti ya mkaguzi wa ndani wa serikali aliyoitoa katika mkutano wa wadau wa mkonge uliofanyika jijini Tanga, ambapo

INAENDELEA UK. 26


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA 111 YA 2019
ACCESS BANK TANZANIA LIMITED ....................MDAI
DHIDI YA
MWANAISHA HAMADI RAMADHANI..................................MDAIWA

Kwa
MWANAISHA HAMADI RAMADHANI
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Alhamis, Tarehe 24 Mwezi 10 - 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

ANGALIZO:

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **7 Mwezi 10 Mwaka 2019.**

..........................
Hakimu Mkazi
Mahakama Ya Wilaya
Kinondoni

215464502



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA 117 YA 2019
ACCESS BANK TANZANIA LIMITED ....................MDAI
DHIDI YA
GAWKA COMPANY LIMITED NA WENZAKE 4..................................MDAIWA

Kwa
KHERI SELEMANI KANTINGA
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya**Jumatatu, Tarehe 28 Mwezi 10 - 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

ANGALIZO:

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **7 Mwezi 10 Mwaka 2019.**

..........................
Hakimu Mkazi
Mahakama Ya Wilaya
Kinondoni

215464502



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA 117 YA 2019
ACCESS BANK TANZANIA LIMITED ....................MDAI
DHIDI YA
GAWKA COMPANY LIMITED NA WENZAKE 4..................................MDAIWA

Kwa
MBALU STIMA
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya**Jumatatu, Tarehe 28 Mwezi 10 - 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

ANGALIZO:

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **7 Mwezi 10 Mwaka 2019.**

..........................
Hakimu Mkazi
Mahakama Ya Wilaya
Kinondoni

215464502



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI
SHAURI LA MADAI NA 111 YA 2019
ACCESS BANK TANZANIA LIMITED ....................MDAI
DHIDI YA
MWINYIJUMA AHMAD SAMNDAEL..................................MDAIWA

Kwa
MWINYIJUMA AHMAD SAMNDAEL
DAR ES SALAAM

KUITWA SHAURINI

Kwa kuwa Mleta madai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unahitajika kuhudhuria Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya **Alhamis, Tarehe 24 Mwezi 10 - 2019 Saa 2:00 Asubuhi**

Kwa mujibu wa madai hayo,na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kutaja shauri hilo ni lazima ulete hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

ANGALIZO:

Kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe **7 Mwezi 10 Mwaka 2019.**

..........................
Hakimu Mkazi
Mahakama Ya Wilaya
Kinondoni

215464502

# Uamuzi ushahidi kesi ya kina Mbowe leo

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam, imepanga kutoa uamuzi leo kuhusu pingamizi la awali kama washtakiwa au mashahidi katika kesi ya uchochezi inayowakabili Mwenyekiti Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe na wenzake wanane kundi lipi lianze kutoa ushahidi.

Hatua hiyo imefikiwa jana baada ya mawakili wa pande zote mbili kuwasilisha hoja zao katika mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Thomas Simba.

Jopo la Jamhuri liliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Dk. Zainabu Mango, Mawakili wa Serikali Jaqline Nyantori na Salim Msemo.

Akiwasilisha hoja nne za pingamizi hilo, Nchimbi alidai kuwa upande wa Jamhuri wanapinga ombi la utetezi la kuanza kusikiliza mashahidi kabla ya washtakiwa wenyewe kutoa utetezi kwamba halitekelezeki kwa sababu linakiuka sheria ya ushahidi na mwenendo wa mashauri ya jinai inayotoa mwongozo wa kuendesha na kusikiliza mashauri.

Alidai kifungu cha 144 cha Sheria ya Ushahidi sura ya 6 iliyofanyiwa marejeo

INAENDELEA UK.8



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua skimu ya umwagiliaji ya Kiwalala katika Halmashauri ya Mtama mkoani Lindi, jana. Wa pili kushoto ni Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga na (wa tatu kushoto) ni Mbunge wa Mtama, Nape Nnauye. **PICHA: OWM**




# Waziri aagiza hatua sakata kontena 38 chuma chakavu

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

OFISI ya Makamu wa Rais imepokea ripoti ya uchunguzi wa kontena 38 za chuma chakavu zilizokuwa zisafirishwe nje.

Hata hivyo, kontena hizo zilizuiliwa bandarini Dar es Salaam.

Ripoti imeeleza kuwapo kwa udanganyifu mkubwa wa kusafirisha bidhaa ambazo hazimo katika orodha ya vitu vilivyoruhusiwa kusafirishwa nje kama chuma chakavu au taka hatarishi.

Akipokea taarifa hiyo, Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, alisema uchunguzi umeibua mambo mengi na kwamba serikali itawachukulia hatua kali wahusika wote katika kashfa hiyo.

"Ripoti inaonyesha kumekuwapo kwa hujuma kubwa ya miundombinu ya nchi; kwa mfano mifuniko ya chemba za maji, nyaya za umeme, mataluma ya reli kinyume cha sheria na tarabitu za biashara ya chuma chakavu," alisema na kuongeza:

"Ripoti imebaini hata kuwapo kwa kampuni isiyo na kibali cha kufanya biashara hiyo. Tutaifutia leseni ya biashara kampuni hiyo na nyingine zitakazoonekana zimefanya udanganyifu na kuuhujumu uchumi wa taifa."

Simbachawene alifanya ziara katika Bandari ya Dar es Salaam Agosti 9, mwaka huu. Baada ya kuyaona kontena 38 za chuma chakavu zilizozuiliwa bandarini, alilagiza Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira(NEMC) kuwasilisha serikalini taarifa juu ya makontena hayo.

Alieleza kuwa katazo la serikali la kusafirishwa vyuma chakavu na taka hatarishi nje ya nchi limetokana na udanganyifu mkubwa wa wafanyabiashara. "Katazo hilo lengo lake ni kulinda viwanda vyetu vinavyotegemea vyuma chakavu kama malighafi ya kuzalisha bidhaa mbalimbali zikiwamo nyaya za umeme na mikeka ya plastiki."

Simbachawene alisema ni muhimu kulinda viwanda vilivyopo nchini kwa kuzuia malighafi kama chuma chakavu kusafirishwa nje ya nchi ili kuongeza uzalishaji wa bidhaa na pia kuzalisha ajira nchini.

"Ameeleza kuwa azma ya serikali ya ujenzi wa viwanda itafanikiwa iwapo kuna malighafi kwa ajili ya viwanda vya ndani.

Aidha, ametangaza kwamba kuanzia sasa hatoruhusiwa mtu yeyote kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha ama kupeleka kiwandani kwa ajili ya kurejeleza mali bila kibali kutoka kwa waziri na kwamba mamlaka za serikali za mitaa ndizo zitakazosimamia ukusanyaji wa vyuma chakavu na taka hatarishi kwa ngazi ya mtu mmoja mmoja.

Akiwasilisha ripoti hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alieleza kuwa licha ya sheria kumtaka mfanyabiashara wa chuma chakavu kujaza fomu namba tatu inayoonyesha anakopata mali hiyo hakuna mfanyabiashara aliyefanya hivyo.

"Tutaendelea kusimamia sheria ili taratibu za kufanyabiashara zitekelezwe ikiwa ni pamoja na kuonyesha mzigo unakopatikana na kibali cha nchi ambako mzigo unakwenda," aliahidi Dk.Gwamaka.

**MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**
**ISO 9001: 2015**
**IDARA YA KODI ZA NDANI**

# TAARIFA KWA UMMA

## WAJIBU WA KUTOA NA KUDAI RISITI/ANKARA ZA MASHINE ZA KIELEKITRONIKI (EFD).

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), inapenda kuwataarifu Wafanyabiashara wote na umma kwa ujumla kwamba, kulingana na kifungu namba 36 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015, kinawataka watoa Huduma au wafanyabiashara wanaostahili kutumia mashine za kielektroniki za kutolea risiti (EFD) kutoa risiti za kielektroniki kwa mauzo yote ya bidhaa au huduma yanayofanywa. Utoaji huu wa risiti za EFD ulianzishwa ili kuboresha utunzaji wa kumbukumbu za Walipakodi, kurahisisha ukadiriaji wa kodi na kuongeza ulipaji kodi kwa hiari na hivyo kuongeza pato la Taifa.

Uchunguzi uliofanywa na TRA umebaini kwamba, baadhi ya wafanyabiashara wanaendelea kutotoa risiti kwa makusudi na wengine kutoa risiti zenye viwango vya chini visivyoendana na gharama ya bidhaa au huduma iliyouzwa. Kitendo cha kutotoa risiti kupitia mashine za Kielekitroniki (EFD) ni hujuma juu ya juhudi za Serikali kukusanya mapato yanayolenga kuleta maendeleo kwa watanzania wote.

Mamlaka ya Mapato Tanzania inaendelea kuwakumbusha Wafanyabiashara kuwa, kwa mujibu wa kifungu tajwa hapo juu, muuzaji wa bidhaa au mtoa huduma anawajibika kutoa risiti/ankara sahihi kupitia mashine ya kielekitroniki (EFD).

TRA, inautangazia umma kwamba, itaendesha msako kwa biashara zote nchi nzima ili kukagua matumizi sahihi ya mashine za kielektroniki na kujiridhisha utekelezaji wa sheria husika. Mfanyabiashara yeyote ambaye atabainika kutotumia vyema mashine hizi katika biashara yake au kukaidi kutimiza wajibu huu wa kisheria atakuwa ametenda kosa na atachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwa ni pamoja na kutozwa faini inayoanzia **Shilingi 3,000,000 /-** na isiyozidi **Shilingi 4,500,000 /- au kifungo cha miaka 3 jela** au vyote kwa pamoja, kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015 kifungu cha 86.

Pia wanunuzi wote wanatakiwa kudai risiti pindi wafanyapo manunuzi ikiwa ni haki ya msingi kisheria kwa kila manunuzi. kwani kutokufanya hivyo ni kosa linaloweza kupelekea kupata adhabu kali ikiwa ni kutozwa faini inayoanzia **Shilingi 30,000 /-** na isiyozidi **Shilingi 1,500,000/-** kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2015.

**Taarifa za msingi ambazo risiti/ankara inahitaji kuwa nazo ni pamoja na zifuatazo;**

1. **Jina la Mnunuzi.**
2. **Namba ya usajili ya mnunuzi (TIN)**
3. **Namba ya Usajili wa Kodi ya Ongezeko la Thamani ya mnunuzi (VRN kwa waliosajiliwa VAT).**
4. **Jina la bidhaa/huduma iliyouzwa au kutolewa.**
5. **Thamani halisi ya bidhaa/huduma iliyouzwa**

Kwa ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na kituo cha huduma na elimu kwa mlipakodi kwa kupiga simu za bure: **0800780078 / 0800750075 au Barua pepe Huduma@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Abdul Y. Mapembe**
**KAIMU KAMISHNA WA KODI ZA NDANI**

215466002

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tusipuuze chanjo tuwalinde watoto

**MAMILIONI** ya watoto nchini wenye umri mbalimbali wanapewa chanjo kuanzia wiki hii hadi Oktoba 21.

Ni sawa na kusema ni wiki ya chanjo ya kitaifa kwa watoto ambao kwa mujibu wa Wizara ya Afya watachanjwa surua, rubella na polio.

Mamillioni ya watoto kote nchini watapokea chanjo dhidi ya magonjwa hayo yanayowaathiri na wakati mwingine kusababisha vifo na ulemavu.

Chanjo hiyo iliyozinduliwa jana kitaifa mkoani Morogoro na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, ni mojawapo ya njia za kuwaokoa watoto na magonjwa na kuwahikikishia kuwa wanalindwa ili wakue badala ya kufa wakiwa na umri wa chini ya miaka mitano.

Ni vyema kujua kuwa maisha yao yanalindwa kutokana na magonjwa yanayoweza kuwaua, kudhibitiwa kupitia chanjo iwe kwa njia ya sindano au kuchanjwa.

Watanzania wanapaswa kujua kuwa chanjo ina tiba ya kuaminika na wataalamu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), wanasema inaweza kuzuia vifo kati ya milioni mbili na tatu kila mwaka.

Lakini, kwa upande mwingine Ripoti ya Shirika la Watoto la Kuhudumia Watoto (UNICEF) inasema mtoto mmoja kati ya watano hajapata chanjo, hasa katika mataifa yanayokabiliwa na migogoro ya kisiasa ikiwamo vita na uasi.

Ni wazi kuwa japo Tanzania hakuna uasi wala matatizo ya kisiasa, wapo wanaopinga chanjo kwa madai kuwa inasababisha ugumba au kupunguza nguvu za kiume madai ambayo ni uzushi.

Kukataa chanjo kunaibuliwa na familia za watoto maskini ambazo mara nyingi zinakabiliwa na changamoto za kukosa huduma bora za afya kwa watoto kwani wana kipato cha chini na uwezo duni kiuchumi. Hali hiyo huchangia vifo vya watoto wao.

Hawa ndiyo wanaopinga chanjo na kutoa madai yenye uzushi. Wakati hayo yanazikuta familia maskini wale wenye uwezo wanawahudumia watoto wao kwa matabibu, lishe bora pamoja na chanjo na dawa nyingine za kutibu magonjwa.

Ndiyo maana serikali inaleta ulinzi wa watoto kwa kutoa chanjo ili kuondoa au kupunguza tofauti hiyo ya kitabaka, kwa kuhakikisha kila mtoto anapata huduma bora za chanjo.

Kwa hiyo kila familia haina budi kumpa mtoto chanjo na kuachana na madai ya kizushi na uongo kuwa dawa hizo zina madhara hasa kupunguza nguvu za kiume na kuleta ugumba.

Hebu wote tuone umuhimu wa kila mmoja kuwajibika kuwachanja watoto wengi bila kujali ni wafamilia maskini au tajiri ili watibiwe na kuwa afya bora kupitia chanjo.

Ikumbukwe hili si jukumu la serikali pekee kila mmoja anawajibika kuanzia mashirika ya kijamii na vyombo vya habari na taasisi za dini ziunge mkono ili kusaidia kuiondoa jamii nyingi kutoka mila na tamaduni potofu ambazo hukataa au kupuuza manufaa ya chanjo hasa za vijijini na maeneo duni.

Ijulikane kuwa chanjo ni kwa kila mtoto aliye na umri chini ya miaka 11 na ni mkakati wa kuwalinda watoto wa Tanzania na vifo, magonjwa na athari nyingine zinazotokana na matatizo ya kiafya.

Hivyo tunaungana na serikali na wadau wengine kuhamasisha kampeni ya kimataifa ya chanjo na kuwasihi wazazi, walezi, walimu na viongozi wa dini kuhakikisha kuwa utoaji chanjo unafanikiwa.

Pamoja na hayo tunaomba viongozi wa serikali na jamii kupita nyumba kwa nyumba kuwabaini wale ambao hawajawachanja watoto na kuwaelimisha ila nao wawapeleke watoto wakapatiwe tiba hiyo inayowalinda na magonjwa kama kifua kikuu, surua, polio, homa ya ini na ndui.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge

Na Peter Orwa

# Tuegemee siri ya ufaulu kutoka Kanda ya Ziwa

**MATOKEO** ya mtihani wa darasa la saba ambalo ndilo daraja la kumvusha mtoto kutoka elimu ya msingi kwenda sekondari, kwa wanaobahatika kuna maana kubwa, tangu yaanikwe hadharani .

Nikiwarejea wanafunzi, hilo ni jambo ninalolitamkia neno 'bahati' kwa maana wapo ambao kutokana na mitihani yao, kufaulu kumewahakikishia kuendelea na masomo tena bure. Sheria inawabana wazazi kuwajibikia hilo, ama watake au wastitake watoto hao wanandelea na sekondari.

Mbali na hilo, mahali hapo hakuna gharama zozote, cha muhimu kwao nikujitoa kitaaluma ili kufanikisha lengo.

Pia, kuna lingine la wale walau wana ahueni kiuchumi. Daima wanahakikishiwa kuendelea na masomo ya sekondari katika shule binafsi iwe wamefaulu au la.

Wapo ambao sura yao katika tija ya kitaaluma. Nao huwa zaidi wanapatikana katika shule za sekondari za kulipia.

Jambo ninalotaka kusema ni kwamba, katika matokeo hayo ya wiki hii kuna mengi ya kujifunza ambayo mazuri yanaweza kusambazwa kutumika kila mahali na mabaya yakakandamizwa.

Ukanda wa Ziwa ndio umekuwa kinara katika kiwango cha ufaulu. Ni kiasi gani kanda nyingine za nchi zinaweza kudodosa hayo kunusa siri ya tija.

Kuna asasi huru za kitaaluma na nazo zimedokeza mambo kadhaa ya kitaaluma. Zote zikikusanywa na kuwekwa sehemu moja inazaa makubwa katika maamuzi ya jumla.

Hatuishii hapo, kwani matumizi ya elimu yanafika mbali zaidi ya manufaa ya mitihani. Elimu ni dhana inayotafsiri makubwa zaidi, maisha halisi ya jana, sasa na baadaye. Inabuni na kutafsiri njia ya maisha.

Msingi bora unawekwa katika elimu kuanzia ngazi ya chini, inasaidia ubora hadi ngazi ya juu zaidi kutoka hapo tulipo.

Mwanafunzi anapojiunga na masomo ya vyuo, iwe kunakotolewa digirii au vyeti vingine vya kati na maarifa ya jumla wa elimu inampa msingi bora mhusika.

Mwanazuoni wa chuo, awe mkufunzi au mhadhiri wote ufanisi na mafanikio ya kazi yake katika kutoa elimu inaanzia katika tija ya uelimishaji inayotolewa chini msomaji huyo alikotokea.

Tija ya msomaji si cheti pekee. La hasha! Inaenda mbali kidogo katika wasifu kama kiwango cha uelewa, mbinu za usomaji na nidhamu ya usomaji wake.

Hiyo ndiyo inayorejesha mkasa katika chuo fulani cha elimu ya juu kukumbwa na vichekesho ndani ya ulingo wa mjadala wao wa kitaaluma, kilio kikuu kikiangukia katika madhara ya kuendekeza tuisheni, badala ya mwanafunzi kujikita rasmi katika usomaji.

Inafahamika tuisheni stadi tegemezi inayomtoa nje ya mstari msomaji akikaririshwa mambo ambayo anaweza kuyabandika katika majibu ya mtihani na hata akafaulu, lakini akibanwa kuonyesha wigo wa uelewa anaagukia katika 'sifuri.'

Mtaaluma mmoja wa sosholojia alitoa ushahidi wa kilichomkuta, akiungwa mkono na mwenziwe mwanasheria, wote wakijenga hoja kwamba walipatwa na mshangao.

Huo ulihusu mwanachuo wa darasa la ngazi yao, katika matukio mawili tofauti wakidai darasa la tuisheni na mambo yanayofanana nayo. Ilikuwa aibu!

Je cha kujiuliza, kosa limeegemea mahali gani? Hapo ana shaka ni huko katika ngazi chini ambako kuna msingi.

Swali zaidi laweza kujitokeza, kulikoni yakatokea leo na zamani hayakuwako? Nani anawajibika nao hilo? Kunawezekana kukawepo maswali mengi, yenye majibu ya kigugumizi.

Hapo ndipo dhana kukumbatia ufafanuzi wa mikoa Kanda ya Ziwa na siri yao ya ushindi katika mahali penye msingi wa elimu. Walishadokeza kadhaa kama mlo wa mchana.



Naibu Waziri wa Maji, Jumaa Aweso (kushoto), akitoa maelekezo baada ya kukagua mradi wa maji wa Litola/Kumbara, mkoani Ruvuma juzi, ambapo ameitaka Ruwasa kukamilisha mradi huo baada ya kusitisha mkataba wa mkandarasi kampuni ya Vibe International. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania mwenyeji mkutano mawaziri SADC

**Na Mwandishi Wetu**

TANZANIA itakuwa mwenyeji wa Mkutano wa Mawaziri wa Sekta za Mazingira, Maliasili na Utalii wa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) utakaofanyika kuanzia Oktoba 21 hadi 25 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC).

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Maliasili na Utalii jana ilisema mkutano huo utakaofunguliwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, pamoja na mambo mengi, utajadili mwenendo wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi.

Pia utafanya tathmini ya utekelezaji wa mikakati ya hifadhi na usimamizi wa mazingira; kupitia mkakati wa SADC wa uchumi wa bahari na kutathmini maendeleo katika sekta za misitu, wanyamapori na utalii.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, mkutano huo utatanguliwa na mikutano ya wataalam wa sekta ya wanyamapori uliotarajiwa kufanyika jana na leo na baadaye mkutano wa makatibu wakuu wa sekta za mazingira, maliasili na utalii utafanyika keshokutwa hadi Oktoba 24, utakaofunguliwa na Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamis Kigwangallah. "Mikutano hii miwili itajadili na kuandaa mapendekezo yatakayowasilishwa katika kikao cha mawaziri kitakachofanyika Oktoba 25 kwa uamuzi na maelekezo," ilisema taarifa hiyo. Tanzania ni miongoni mwa nchi 16 wanachama wa SADC zinazotekeleza mkakati wa SADC kuhusu usimamizi wa sheria na vita dhidi ya ujangili wa wanyamapori.

Maeneo mengine yanahusu programu za uhifadhi yaliyovuka mpaka wa nchi moja hadi nyingine kwenye maeneo ya misitu, uvuvi, mazingira na mabadiliko ya tabianchi, utalii, ukuzaji viumbe maji na mkakati wa ubora wa afya wa wanyama wa majini na Programu ya Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mkutano wa mawaziri wa sekta za mazingira, maliasili na utalii ni mwendelezo wa mikutano itakayofanyika nchini katika kipindi cha mwaka mmoja ambacho Tanzania ni mwenyekiti wa jumuiya hiyo.

Agosti, mwaka huu, serikali ya Tanzania ilikuwa mwenyeji wa Mkutano wa 39 wa Nchi Wanachama wa SADC uliofanyika jijini Dar es Salaam. Katika mkutano huo, Rais John Magufuli, alikabidhiwa na kupokea rasmi jukumu la uenyekiti wa jumuiya hiyo.

SADC ni moja ya jumuiya za kikanda katika bara la Afrika na iliundwa kwa lengo la kuimarisha ushirikiano katika nyanja za uchumi, ulinzi, siasa na usalama.

Nchi wanachama wa SADC ni 16 ambazo ni Angola, Botswana, Comoros, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), Eswatini (zamani Swaziland), Lesotho, Madagascar, Malawi, Mauritius, Msumbiji, Namibia, Shelisheli, Afrika Kusini, Tanzania, Zambia na Zimbabwe.

# Auawa na kutupwa katika shamba la jeshi

**Hamisi Nasiri,** MASASI

MKAZI wa mtaa wa Nyasa, Masasi mkoani Mtwara, Barnaba Athumani (48), amekutwa amekufa kwa madai ya kupigwa ndani ya mashamba ya kambi ya Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mtwara, Blasius Chatanda, alisema tukio hilo lilitokea juzi, majira ya 4:45 asubuhi na mwili wa mtu huyo uliokotwa ukiwa katika shamba lililoko katika eneo la kambi ya JWTZ wilayani hapa.

Alisema jeshi la polisi lilipata taarifa ya maiti hiyo kutupwa ndani ya shamba moja la eneo la kambi ya JWTZ huku ikiwa na majeraha mbalimbali mwilini.

Chatanda alisema hakuna taarifa zozote za kiuchunguzi zinazoeleza kuwa mauaji hayo yamefanywa na askari wa jeshi hilo licha ya kwamba baadhi ya taarifa zinadai kuwa aliuawa katika tukio la wizi wa korosho.

Kamanda Chatanda alisema katika uchunguzi awali, Athumani inaonekana amefanyiwa kitendo hicho cha kupigwa hadi kupoteza maisha na watu wasiojulikana kisha kutupwa katika mashamba hayo.

Alisema kuwa pia jeshi la polisi halina uchunguzi wa moja kwa moja kuwa marehemu ameuawa kwa madai ya kuiba korosho kwenye mashamba ya kambi ya jeshi hilo.

Alisema kumekuwa na taarifa ambazo bado hazija thibitishwa na jeshi la polisi kuwa mtu huyo ameuawa na askari wa jeshi la wananchi kambi ya Masasi kwa vile uchunguzi bado unaendelea na taarifa rasmi itatolewa baada ya uchunguzi kukamilika.

"Tunachojua mtu huyu amekutwa ametupwa ndani ya shamba lake ambalo liko maeneo ya kambi ya jeshi. Hatufahamu aliyehusika na tukio hili na hatujui kama ni kweli alikuwa akiiba korosho," alisema Kamanda Chatanda.

Kutokana na tukio hilo, alisema jeshi la polisi linaendelea na uchunguzi na kwamba yeyote atakayebainika kuhusika atafikishwa kwenye mkono wa sheria bila kujali ni askari au raia.

Baadhi ya wananchi wa karibu na familia ya marehemu, ambao waliomba majina yao kuhifadhiwa, wanamfahamu Athumani kwa miaka mingi na kwamba hakuwa tabia ya wizi kama inavyodaiwa.

Walisema wako baadhi ya watu ambao wameshuhudia akipigwa na baadhi ya askari wa JWTZ kwa madai alikutwa akiwa katika moja ya mashamba ya korosho ambalo linamilikiwa na askari wa jeshi hilo.

"Sisi tulikuwa tukipita na njia kutoka mashambani kwetu. Tuliona mtu mmoja ambaye hakutambua kama ndiye yeye akipigwa na askari ambaye hatumjui jina lake ndipo baadaye tulisikia kuna mtu ameuawa ndani ya mashamba ya kambi ya jeshi," alisema mmoja wa wananchi hao.

Wananchi hao walisema si mara moja kwa raia ambao wanalima karibu na kambi hiyo kukamatwa na baadhi ya askari wa JWTZ kisha kuteswa na kupigwa kwa madai kuwa ni wezi wa korosho katika mashamba ya askari hao.

Kwa mujibu wa wananchi hao, Athumani kwa muda mrefu alikuwa akijishughulisha na useremala, kazi ambayo ilikuwa ikimwingizia kipato, hivyo si kweli kwamba alikuwa na tabia ya wizi.


PRO SHARE CAPITAL LTD
"We build your future"

PROSHARE CAPITAL LIMITED,
MIKOCHENI REGENT ESTATE, MIGOMBANI STREET
P.O. Box 79632 DAR ES SALAAM, TANZANIA TEL: +255 22 27 72885

Kampuni ya Mikopo Proshare Capital Ltd kushirikiana na Kampuni ya Ukusanyaji madeni Koti Brothers Company Ltd, Inatafuta magari yaliyowekwa dhamana na kufichwa na wateja.

Kwa atakaefanikisha kupatikana kwa magari hayo atapata Ofa ya shilingi laki mbili (200,000/-) kwa kila gari moja.

Mawasiliano Zaidi piga namba zifuatazo;

- **0657 741578**
- **0684 217723**
- **0713 235517**
- **0657 470214**

215464602

| S/N0. | AINA YA GARI | NAMBA YA GARI |
|---|---|---|
| 1 | TOYOTA BREVIS | T742 DFJ |
| 2 | TOYOTA RAUM | T197 DEM |
| 3 | TOYOTA WISH | T476 CGA |
| 4 | TOYOTA PLATZ | T309 DKW |
| 5 | MERCEDES BENZ | T262 DEX |
| 6 | TOYOTA MARKX | T796 DFG |
| 7 | MITSUBISHI PAJERO MINI | T113 DFP |
| 8 | TOYOTA CARINA | T839 DAV |
| 9 | NISSAN CIVILIAN | T747 CFP |
| 10 | SCANIA | T843 CBT |
| 11 | TOYOTA VEROSA | T908 DEZ |
| 12 | SUZUKI WAGON | T216 CNX |
| 13 | TOYOTA ALLEX | T925 DGA |
| 14 | TOYOTA IST | T392 CSU |
| 15 | TOYOTA VITZ | T287 DDU |

| S/N0. | AINA YA GARI | NAMBA YA GARI |
|---|---|---|
| 16 | TOYOTA PORTE | T667 DDJ |
| 17 | TOYOTA WILL | T164 DGA |
| 18 | TOYOTA IST | T694 CVR |
| 19 | TOYOTA ALTEZZA | T827 CVJ |
| 20 | DAF TRACTOR | T482 CPY |
| 21 | TOYOTA PROGRES | T123 DHP |
| 22 | MERCEDES BENZ | T328 DJH |
| 23 | TOYOTA MARKX | T756 DKM |
| 24 | SUZUKI JEEP | T402 CXL |
| 25 | TOYOTA NOAH | T517 DEL |
| 26 | TOYOTA OPA | T919 CFW |
| 27 | MITSUBISHI COLT | T584 DBV |
| 28 | TOYOTA VEROSSA | T172 BEL |
| 29 | TOYOTA RAV4 | T497 DML |
| 30 | TOYOTA PORTE | T133 DGR |
| 31 | TOYOTA OPA | T949 BKM |

# Mvua zasababisha kizaazaa Dar es Salaam

**Na Elizabeth Zaya**

WAKAZI wa Jiji la Dar es Salaam jana walijikuta katika wakati mgumu baada ya kukwama kupata usafiri, nyumba kufurika maji huku maeneo mengine yakishindwa kupitika.

Maeneo ambayo yalishuhudiwa na gazeti hili na taarifa zilizosambazwa kwenye mitandao ya kijamii, yameonyesha barabara nyingi kujaa maji ya mvua na kushindwa kupitika kirahisi.

Makutano ya barabara ya Goba na Bagamoyo, maji yalionekana kujaa hali iliyosababisha watumiaji wa barabara hiyo kushindwa kuitumia baada ya kingo za barabara hiyo kufunikwa na maji hayo.

Eneo la Jangwani, wakazi wanaozunguka Mto Msimbazi, nyumba zao zilizingirwa na maji hayo yaliyosababishwa na mvua zinazoendelea kunyesha katika jiji la Dar es Salaam.

Watu wa eneo hilo walilazimika kutembea kwa miguu kutokana na kusekana kwa usafiri kutokana na barabara inayopitia Jangwani kufunikwa na maji hayo. Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakazi wa eneo hilo, walisema miongoni mwa sababu zinazochangia mafuriko hayo ni pamoja na takataka kujaa kwenye Mto Msimbazi na kushindwa kupitisha maji kipindi cha mvua.

Jumanne Bushiri, mkazi wa eneo hilo, Kata ya Magomeni, alisema bila serikali kuchukua hatua za haraka, kuna hatari ya kutokea madhara makubwa kwa wakazi wa eneo hilo.

Akizungumza na Nipashe, Mjumbe wa Baraza la Usuluhishi katika kata hiyo, Habiba Mondoma, alisema ni vyema mpango wa kuendeleza mto huo ukafanyika haraka ili kuokoa wananchi wake. "Tunajua kwamba kuna mpango wa kuendeleza Bonde la Mto Msimbazi, na hii ndiyo itakuwa msaada mkubwa kwa wakazi wanaouzunguka, kwa sababu nyumba nyingi zinajaa maji kutokana na kukosa pa kwenda, badala ya kwenda Msimbazi yanaingia kwenye nyumba za watu," alisema.

Kutokana na hali hiyo, alisema wakazi kutoka kata 18 zinazouzunguka mto huo nyumba zao zimejaa maji na kulazimika kukimbia kwa muda.

"Hivi ninavyozungumza na wewe, nyumba nyingi kutoka katika kata hizi zinazozunguka Mto Msimbazi, zimejaa maji, wakazi wamelazimika kukimbia katika nyumba zao kupisha maji mpaka yatakapopungua," alisema Mondoma.

"Tunaiomba Wizara ya Fedha itoe fedha ili mradi huu wa kuboresha Mto Msimbazi uendelee, na sisi tupo tayari kulipwa fidia ili tuondoke, tunaamini pesa zipo, tunaomba watusaidie, hizi mvua ni za vuli tu, bado masika na huenda zikaleta madhara kuliko haya."

Eneo la Tandale, Mto Ng`ombe ulifurika maji na kupita juu na kuleta adha kubwa kwa wakazi wa eneo hilo pamoja na vyombo vya usafiri. Ramadhani Majuto mkazi wa eneo hilo ni miongoni mwa wananchi waliolazimika kukaa pembeni kusubiri maji yapungue ili wavuke.

Pia ilishuhudiwa baadhi ya madereva wa bodaboda wakilazimika kuwavusha wanafunzi.

# Sheria kuruhusu uchangiaji figo

INATOKA UK. 2

Katika upasuaji huo walifanikiwa kuokoa Sh. bilioni 4.5 ambazo zingetumika kama wengeenda kutibiwa nje ya nchi ambako mgonjwa mmoja angegharimu Sh. milioni 120 wakati nchini mgonjwa mmoja anagharimu Sh. milioni 30.

Alisema wamechukua uamuzi huo baada ya kuwapo kwa changamoto ya watu kuhofia kutoa viongo vyao na kuepuka kiungo hicho kufanywa biashara na baadhi ya watu. Alisema Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Muhimbili wanashirikiana kuandaa sheria hiyo ambayo itakuwa muongozo kwa hospitali zote zinazotoa huduma za upandikizaji wa viungo nchini.

"Hospitali ya Muhimbili kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, tupo kwenye hatua za mwisho za kukamilisha sheria ya upandikizaji wa figo ambayo itakuwa dira itakayotumiwa na hospitali zote zinazofanya upandikizaji nchini," alisema Prof. Museru.

Mbali na sheria hiyo, alisema pia kwa miaka ya baadaye wataanzisha sheria itakayoruhusu watu waliokufa kutumia figo zao kupandikiza kwa wagonjwa.

"Sheria hii itaanzishwa siku za baadaye baada ya kuandaa mazingira lakini pia kujifunza kwa nchi za wenzetu kwa sababu tunahitaji sheria inayoeleweka katika kuteleza hilo," alisema Prof. Museru.

**UPANDIKIZAJI ULOTO WATOTO**

Kadhalika alisema MNH, inatarajia kujenga kituo maalum cha huduma za kibingwa za upandikizaji wa viungo kama figo, ini, uloto na watoto kwa wazazi ambao hawajawahi kupata katika tawi la Mloganzila.

"MHN ipo kwenye mipango ya kuanzisha huduma za upandikizaji uloto utakaoanza Novemba mwaka huu. Tunategemea kuanza kuhudumia familia zilizoshindwa kupata watoto na tupo katika hatua za mwisho kwa ajili ya kuanza upandikizaji," alisema Prof. Museru.

"Kutokana na kufanikiwa kupandikiza figo wagonjwa 51, MNH itaanza kufanya upandikizaji figo kwa kundi la wagonjwa wenye vihatarishi vya juu kama wenye maambukizi ya Ukimwi, Homa ya Ini na watu wa karibu kuruhusu kutoa figo badala ya ndugu peke yake kama ilivyo sasa," alisema Prof. Museru.

"Madaktari bingwa wa figo sasa wanafanya maandalizi na uchunguzi hadi mgonjwa kufikia hatua ya kupandikizwa figo na kumfuatilia kliniki baada ya upasuaji kwa asilimia 100," alisema Prof. Museru.

Alisema madaktari bingwa wa upasuaji wa figo wamefanya upasuaji wao wenyewe kwa anayetoa figo kwa asilimia 100 na kupandikiza kwa anayepokea figo kwa asilimia 80.

# Sakata la wakurugenzi kukatiwa rufani Afrika

**Na Enock Charles**

SIKU mbili baada ya Mahakama ya Rufani kutengua uamuzi wa Mahakama Kuu kuwazuia wakurugenzi wa halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi, Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (Jukata), Bob Wangwe, amesema anakusudia kukata rufani katika Mahakama ya Afrika.

"Nitakata rufani katika Mahakama ya Afrika. Ninashauriana na mawakili wangu kuona nini tutafanya," alisema Wangwe.

Katika Uamuzi uliotolewa Jumanne iliyopita na jopo la majaji wa

Mahakama ya Rufani likiongozwa na Jaji Augustine Mwarija, wakurugenzi watendaji wa halmashauri za wilaya na wakurugenzi wa miji, manispaa na majiji wanaruhusiwa kusimamia uchaguzi kwa niaba ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kama ambavyo wamekuwa wakifanya kwa miaka kadhaa iliyopita.

Majaji wengine katika kesi hiyo ya kusikiliza rufani ya serikali iliyowasilishwa na Wakili wake Mkuu, Dk. Clement Mashamban ni Stella Mugasha, Richard Mziray, Rehema Mkuye na Jacobs Mwambegele.

Wakitoa uamuzi huo, majaji hao walisema kabla ya wakurugenzi hao kuteuliwa kuwa wasimamizi, huapishwa na kutoegemea chama chochote cha siasa, hivyo wanafuata taratibu za kisheria. Pia walikubaliana na hoja za warufani kwamba wanapobainika kuvunja sheria na kukiuka kiapo, huondolewa na kuchukuliwa hatua zinazostahili. Mahakama Kuu katika uamuzi wake katika kesi hiyo iliyofunguliwa na Bob Wangwe, ilisema wakurugenzi hao kusimamia uchaguzi ni kinyume na Katiba

inayotaka Uchaguzi kuwa wa huru na wa haki, hivyo kubatilisha

kifungu 7(1) cha Sheria ya Uchaguzi kinachoipa mamlaka NEC kuwateua kufanya kazi hiyo na kifungu cha 7(3)

kinachoipa NEC mamlaka ya kuteua mtumishi yeyote wa umma kuwa msimamizi wa uchaguzi.

Hukumu hiyo ya Mei 11, mwaka huu, iliyotolewa na jopo la majaji watatu, Dk. Atuganile Ngwala, Dk. Benhajj Masoud na Firmin Matogolo wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam Mahakama iliweka bayana kuwa vifungu hivyo ni kinyume cha Katiba ya nchi.

Kwa mujibu wa hukumu hiyo, wakurugenzi hao ni wateule wa Rais aliyeko madarakani na si waajiriwa wa NEC, hivyo kuwateua kusimamia uchaguzi kutaifanya tume hiyo kutokuwa huru na pia uchaguzi hautakuwa huru na wa haki.

**WATOA MAONI**

Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, George Kahangwa, alisema jana kuwa uamuzi wa Mahakama ya Rufani utaendeleza ukandamizwaji wa demokrasia kwa kuwa ukada wa chama cha siasa hauwezi kuondolewa kwa kiapo cha maneno.

"Watanzania ni mashahidi jinsi wakurugenzi wanavyovuruga uchaguzi, wanavyokimbia wakati wagombea wanaporudisha fomu. Kwa hali hii demokrasia itaendelea kukandamizwa. Ni ukweli uliowazi kwamba ukada hauwezi kuondolewa kwa kiapo," alisema Dk. Kahangwa.

Naye Mwenyekiti wa Baraza la Vijana la Chama cha Demokrasia na

Maendeleo (Chadema), Patrik Ole Sosopi, alisema kurejeshwa kwa wakurugenzi kusimamia uchaguzi kutawarejesha katika mbinu za awali zilizotumiwa na chama tawala katika kupata ushindi kwa wabunge wake.

"Tutaendelea kutumia mbinu zetu za wakati wote na tunatoa onyo kwa wale wataovunja sheria za uchaguzi kuwa hatutavumilia," alisema Sosopi.

Katibu Mwenezi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Ado Shaibu, alisema katika kiapo wanachopewa kabla ya kusimamia uchaguzi, hakuna kipengele kinachowataka kukana uanachama wao, hivyo kushauri suala hilo kupelekwa mahakama za kimataifa.

# Uamuzi ushahidi kesi ya kina Mbowe leo

INATOKA UK. 4

mwaka 2002, kinazungumzia uongozaji wa mashahidi.

Alidai upande wa Jamhuri unaishawishi mahakama kwamba utaratibu wa uwasilishaji mashahidi wakati wa utetezi unatamkwa na kifungu cha 231 (1) (a) na (b) pamoja na mambo mengine kinazungumzia haki na utaratibu wa kuwasilisha utetezi.

Akifafanua hoja zake, alidai kuwa mshtakiwa hawezi kuingia kwenye haki ya kuita mashahidi kama yeye mwenyewe hajaamua au hajatoa ushahidi wake mahakamani.

"Mheshimiwa Hakimu Mahakama ijielekeze pia katika kifungu cha 38 (2) (a) na (b) kwa kuwa utaratibu wa utoaji wa ushahidi wa utetezi mahakama inapaswa kumuita mshtakiwa kama ushahidi ili atoe utetezi wake," alidai Nchimbi.

Alidai washtakiwa wanavaa kofia mbili kwa wakati mmoja kwa sababu wanasimama kama washtakiwa na mashahidi kwa wakati mmoja.

Nchimbi alidai sheria inataka ushahidi unapotolewa mashahidi wengine wasiwepo wakati wa ushahidi na kwamba iwapo upande wa utetezi watapewa nafasi ya kusikiliza mashahidi kabla ya washtakiwa kujitetea, hawataruhusiwa kusikiliza kinachosemwa na mashahidi.

Pia alidai ushahidi unapotolewa ni lazima washtakiwa wawepo hivyo hawawezi kuwaondoa wakati ni sehemu ya shauri hilo.

Hata hivyo, aliomba mahakama itoe mwongozo utakaowataka washtakiwa hao kutoa utetezi wao kabla ya mashahidi.

Wakili wa utetezi, Peter Kibatala akijibu hoja za Jamhuri, alidai kuwa hakuna kifungu chochote cha sheria za hapa nchini au nje ya Tanzania ambacho kinazuia washtakiwa kusikiliza mashahidi wake.

Mbali ya Mbowe, washtakiwa wengine ni Katibu Mkuu Taifa, Dk. Vicent Mashinji, Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko, Katibu Mkuu Taifa, Naibu Katibu Mkuu Taifa, Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche, Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa na Mbunge wa Kawe Halima Mdee.

Wengine ni Mbunge wa Tarime Mjini, Ester Matiko na Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya.

# Wafanyabiashara waiangukia serikali

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA mkoani Manyara wamemwomba Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, awasaidie kufikisha kilio chao serikalini ili idadi kubwa ya taasisi za serikali zinazowabana kulipa kodi zipunguzwe ama kodi zinazodaiwa ziunganishwe.

Lengo la ombi hilo ni kumwondolea mfanyabiashara adha ya kudhibitiwa na mamlaka nyingi.

Baadhi ya taasisi zilizotajwa ni Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Wakala wa Usalama Mahali pa Kazi (OSHA) na nyingine ambazo wamesema mbali na kuwatoza kodi kubwa, lakini wamekuwa wakipata usumbufu wa aina mbalimbali.

Hata hivyo, wameahidi kuendelea kulipa kodi kwa hiari baada kuridhishwa na utendaji kazi wa serikali kwa kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Walimweleza Dk. Kijaji aliyekutana nao Mjini Babati kujadili fursa na changamoto zinazoikabili sekta binafsi pamoja na kuwaelimisha namna serikali ilivyofuta kodi lukuki kwa lengo la kuwawezesha kufanyabiashara zao kwa tija zaidi.

Akijibu hoja mbalimbali za wafanyabiashara hao, alipongeza kwa kulipa kodi ambayo imeiwezesha serikali kutekeleza miradi mikubwa ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa vituo vya afya.

"Kwa mara ya kwanza katika historia ya nchi hii, Septemba, tumekusanya zaidi ya Sh. trilioni 1.76 kiasi ambacho hakijawahi kutokea tangu nchi ipate uhuru," alisema Dk. Kijaji.

Alisema kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya ufanyaji biashara ambapo mpaka sasa imeondoa zaidi ya kodi 50 zilizokuwa zikiwakwaza wafanyabiashara lengo likiwa ni kuwawezesha kufanyabiashara yao kwa ufanisi zaidi ili waendelee kulipa kodi.

"Tumepunguza kodi nyingi sana, mwaka wa fedha(2018/2019) tulipunguza kodi 108 na mwaka huu wa fedha (2019/2020) tumepunguza kodi na tozo 54 kwa makusudi, Rais John Magufuli ameamua kuwawezesha Watanzania, kila mmoja kwenye eneo lake la kazi afanye kazi vizuri," alisisitiza.

Aidha, Dk. Kijaji aliwataka wafanyabiashara waliopata msamaha wa riba kwenye kodi mbalimbali walizokuwa wanadaiwa, walipe madeni yao kwa mujibu wa makubaliano yaliyofikiwa na kwamba hakutakuwa na muda mwingine utakao ongezwa.

Aliwataarifu kwamba serikali imesitisha kwa muda utoaji fedha kwenye miradi mikubwa ya kimkakati iliyopangwa kutekelezwa na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa-Tamisemi yenye lengo la kuziwezesha halmashauri kujitegemea kimapato hadi pale mfumo madhubuti wa kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo utakapowekwa.

Dk. Kijaji alitoa kauli hiyo baada ya kupokea maombi kutoka kwa Mbunge wa Babati Mjini, Pauline Gekul, aliyeomba Sh. bilioni 5.5 kutoka serikalini kwa ajili ya kujenga kituo cha mabasi ili kuboresha mazingira ya biashara na utoaji huduma kwa wananchi.

Naibu Kamishna Operesheni ya Kodi, Simon Kingu, alisema Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) iko tayari kushirikiana na wafanyabishara na kuhakikisha wanatatua kero zao ili walipekodi kwa hiari kwa ajili ya maendeleo ya nchi.




Mkuu wa Mkoa wa Kigoma, Brigedia Jenerali (mstaafu), Emmanueli Maganga (kushoto), akishuhudia muuguzi akitoa chanjo ya surua, rubela na polio kwa mtoto, wakati wa uzinduzi wa chanjo ya watoto chini ya miaka mitano iliofanyika kwenye uwanja wa kituo cha afya Kikungu, Kata ya Gungu, Manispaa ya Kigoma/Ujiji juzi. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Bil. 4/- kupeleka maji kwenye kata

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MBUNGE wa Msalala, Ezekieli Maige, amesema Wizara ya Maji imetenga Sh. bilioni 4 kwa ajili ya kupeleka huduma ya majisafi na salama katika kijiji na kata ya Busangi kutoka katika mradi wa maji wa Ziwa Victoria ambapo kwa sasa umefika Kata ya Lunguya.

Maige aliyabainisha hayo jana, wakati akizungumza na wananchi wa kijiji na Kata ya Busangi Halmashauri Msalala mkoani Shinyanga, na kusema serikali imekuwa ikiendelea kutatua changamoto ya ukosefu wa huduma ya maji katika vijiji na kata ambavyo havina huduma hiyo.

Alisema shilingi milioni 700 zimeshatolewa kwa ajili ya kuanza kwa mradi huo, na mkandarasi aliyeteuliwa kuanza kutekeleza mradi huo atahakikisha anafikisha maji kwanza maeneo yenye changamoto.

Katika hatua nyingine, Maige alisema ng'ombe katika kata ya hiyo ziko hatalini kutoweka kutokana na kukosekana kwa mabwawa ya maji ya kunyweshea mifugo baada ya kutoka kwenye malisho.

Aidha, alisema awali walikuwa wakitumia bwawa ambalo lilichimbwa na mkoloni, lakini limejaa tope na kusababisha kukosekana kwa maji ya kunyweshea mifugo.

Meneja Mkuu wa migodi ya Buzwagi na Bulyanhulu, Benedict Busunzu, alisema katika kutatua changamoto ya ukosefu wa mabwawa ya maji ya kunyweshea mifugo, atahakikisha anakarabati moja ya bwawa lililochibwa enzi ya mkoloni.

# Majaliwa akemea ujenzi mbovu hospitali

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amekagua ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Ruangwa, mkoani Lindi na kusema hajaridhishwa na baadhi ya majengo.

Amemwagiza Mhandisi wa Halmashauri ya Wilaya, Tengamaso Wilson, abomoe kuta zenye hitilafu na kurekebisha kasoro zilizopo kwenye majengo hayo ikiwamo kutonyooka kwa kuta za majengo hayo.

Alitoa agizo hilo juzi wakati akikagua majengo ya hospitali hiyo, na kumweleza mhandisi huyo kwamba kuta zimepishana unene kwa sababu hakusimamia kazi yako ipasavyo. "Ukuta huu ni mbovu kwa sababu hukuwasimamia vizuri mafundi wako. Kuna mahali juu unaona ukuta ni mdogo na huku chini ni mnene."

Majengo ambayo Waziri Mkuu aliyakagua na kuonyesha kutoridhishwa nayo ni ya utawala, wagonjwa wa nje (OPD) na maabara. Majengo mengine yanayojengwa ni jengo la wazazi, la X-ray, la utoaji dawa na la kufulia nguo.

Alipouliza ni kwa nini kumetokea tofauti baina ya kuta hizo, Waziri Mkuu alijibiwa kwamba tatizo ni upigaji wa lipu. "Mhandisi wa Wilaya simamia hili, kagonge upya kuta za jengo hili na lile. Hatuwezi kuwa na jengo la serikali la aina hii. Tukitoa fedha ya serikali ni lazima mjiridhishe kama kilichojengwa ndicho sahihi."

"Tunahitaji majengo yote yawe smart, hata ujenzi wake nao uwe smart. Usikubali kutoa certificate kama kazi haijakamilika. Kama kuna kazi haujaridhika nayo, usikubali certificate itoke. Zile sentimeta 30 ni lazima zirekebishwe la sivyo, itaonekana huku uliweka matofali mengi kuliko upande ule," alisisitiza.

Akiwa hospitalini hapo, Waziri Mkuu alielezwa kwamba katika awamu ya kwanza, serikali imetoa Sh. bilioni 1.5 na kuelekeza yajengwe majengo saba ya kipaumbele ambayo ni jengo la wazazi, la wagonjwa wa nje (OPD), maabara, la X-ray, la utoaji dawa, la kufulia nguo na la utawala.

Ujenzi wa hospitali hiyo unafanyika kwa kutumia njia ya manunuzi inayoitwa 'Force Account' ambapo halmashauri inanunua vifaa vya ujenzi na kuajiri mafundi wa kujenga majengo yaliyoelekezwa wakisimamiwa na wataalamu wa halmashauri na kamati mbalimbali.

Wakati huohuo, Waziri Mkuu amemwagiza mweka hazina wa halmashauri hiyo, Frank Chonya, ajiridhishe na kazi za ujenzi zinazofanyika kabla hajaamua kutoa fedha za malipo.

"Mweka hazina, wakati wote ukiambiwa kuwa certificate imeletwa ni lazima uende ukakague mradi na kama haujaridhika, sema wazi kwamba hujaridhika na kazi iliyofanywa," alisema Waziri Mkuu.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Andrea Chezue, alisema kiasi chote kilichotolewa na serikali cha Sh. bilioni 1.5 kimeshatumika, na kwamba halmashauri ilitumia zaidi ya Sh. milioni 100 ili kusafisha eneo na kulipa fidia ili wapate eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 56.

# Muuguzi atoweka kisa kubaka mgonjwa

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

MUUGUZI wa Hospitali ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Damian Mgaya (41), anadaiwa kutoroka hospitalini hapo, kufuatia tuhuma za kumbaka mgonjwa ambaye ni binti mwenye miaka 16.

Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Ruta Deus, alithibitisha tuhuma hizo na kusema kesi imefikishwa katika kituo cha polisi.

Binti huyo (jina tunalo) ni mkazi wa mtaa wa Buyumba, Kijiji cha Mwanzugi Igunga mjini.

Akizungumza na wanahabari baada ya kuruhusiwa kutoka katika wodini alikokuwa amelazwa akisumbuliwa na tumbo mama wa msichana huyo (jina linahifadhiwa), alifafanua kwamba tukio hilo lilitokea wiki iliyopita Oktoba 10, kati ya saa 4:00 na 8:00 usiku katika maeneo ya hospitali hiyo.

Aidha, mama huyo alisema muuguzi huyo alifika katika wodi namba 3 kumwangalia mgonjwa na alipoona hali yake siyo nzuri, alimwambia anambadilishia dawa.

Alibainisha kuwa ndipo muda mfupi baada ya kutoa ushauri huo aliomba aondoke na msichana huyo aliyekuwa akiuguzwa na mama yake na walipofika ofisini kwa muuguzi huyo, alimchoma sindano ya usingizi na kisha alianza kumbaka hadi saa 8:00 usiku.

Alifafanua mama huyo kwamba baada ya kuona muda umekuwa mrefu bila mwanaye kurejeshwa, aliomba msaada kwa baadhi ya wagonjwa wenzake wenye hali nzuri ili wamsaidie kumtafuta mwanaye.

Hata hivyo, mama huyo alisema baadhi ya wauguzi waliokuwa zamu walipopata taarifa hiyo waliungana na baadhi ya wagonjwa kumsaka msichana huyo, ndipo walipomkuta eneo la wagonjwa wanawake la kufulia nguo akiwa kwenye nyasi, huku akiwa hajitambui na akiwa amemwagiwa maji mwili mzima.

Kwa mujibu wa mama mzazi wa mtoto huyo baada ya kumwondoa kutoka kwenye nyasi hizo alikuwa akivuja damu nyingi sehemu za siri kutokana na kumbakwa.

"Kitendo alichofanyiwa mwanangu ni cha kinyama na hakipaswi kufumbiwa macho ninaviomba vyombo vya dola kumsaka muuguzi huyo popote alipokimbilia ili aweze kufikishwa mahakamani." Alilalamika.

Baadhi ya kinamama wanaokwenda kutibiwa katika hospitali ya wilaya ya Igunga, walisema wanaingiwa na hofu kubwa kutokana na kitendo hicho na hivyo kuiomba serikali kuchukua hatua.

Muuguzi huyo hakupatikana kwa njia ya simu kuzungumzia tuhuma hizo, licha ya kutafutwa kwa siku tatu.

Aidha, Mganga Mkuu wa Wilaya ya Igunga, Dk. Ruta Deus, alipotakiwa kuzungumzia tuhuma hizo, alikiri kwamba Mgaya alimbaka msichana huyo.

"Ni kweli tukio hilo lipo na hiyo siyo mara ya kwanza kwani siku za nyuma Mgaya akiwa kituo cha afya cha tarafa ya Igurubi alifanya tukio kama hilo hivyo hii ni mara ya pili na huo ni ukiukwaji wa taratibu na kanuni za kiutumishi," alisema Mganga Mkuu wa Wilaya.

Kwa mujibu wa Deus suala hilo liko polisi Igunga na kwam-

# Serikali yaonya usugu wa dawa

**Na Yasmine Protace**

MFAMASIA mkuu wa serikali, amewataka wananchi kuacha kutumia dawa kiholela ili kuepusha uwezekano wa baadhi ya dawa kuwa na usugu.

Ametaka jamii kufuata ushauri wa madaktari kwenye matumizi sahihi ya dawa ili kuzuia kupata usugu wa vimelea.

Daudi Msasi, Mfamasia Mkuu na Mkurugenzi wa Huduma za Dawa katika Wizara ya Afya, alisema wakati akizungumzia mkutano uliowashirikisha wadau mbalimbali wa afya kutoka Tanzania na nchi nyingine uliokuwa ukizungumzia matumizi sahihi ya dawa.

Aliwaambia washirikia kuwa dunia nzima inapambana na usugu dhidi ya dawa na ili kunusuru usugu wa vimelea vya dawa, wananchi wanatakiwa kufuata utaratibu wa kumeza dawa kwa ushauri wanaopewa na madaktari.

Alisema kuwa lengo kuu la kujadili mnyororo wa ugavi wa dawa ni kuibua hoja na kuchangia uzoefu na kutafuta majibu kwenye masuala mbalimbali yahusuyo tiba.

"Malengo ya mnyororo wa ugavi ni kuhakikisha wananchi wanapata dawa wanazostahili na kwa wakati."

Vilevile, alisema eneo ambalo wanalisisitizia ni kuanzisha vyanzo vya fedha ili viweze kusaidia upatikanaji wa dawa.

Aliongeza kuwa ili kufanikiwa lazima takwimu ziwe sahihi na kwamba wanawafundisha watu masuala ya takwimu ili waweze kujua jinsi ya upatikanaji wa dawa na wapi zinakwenda.

Aliongeza kuwa mfumo utasaidia upatikanaji wa taarifa na utaisaidia serikali kufahamu dawa zinapopelekwa.

Alisema takwimu zisipotolewa kwa usawa itasababisha athari kubwa ambapo mahitaji yatakuwa mengi au yatakuwa madogo na hali hiyo itasababisha wananchi kutopata dawa.

Akizungumzia dhana ya dawa 30 alisema ilianzishwa kwa kuangalia kuwa angalau asilimia zaidi ya 80 ya wagonjwa wakifika katika kituo wanatibiwa.

Kwa upande wa magonjwa makubwa inabidi watafutiwe dawa sehemu nyingine.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi St. Anne Marie Academy ya Mbezi kwa Msuguri wakiwa na furaha baada ya shule yao kutangazwa kuwa ya kwanza kwa Mkoa wa Dar es Salaam, kati ya shule 459 kwa Wilaya ya Ubungo, kwenye matokeo ya darasa la saba yaliyotangazwa na Baraza la Taifa Ala Mitihani (NECTA). **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanaume waambiwa wasitegee kupima VVU

**Na Joctan Ngelly,** KIGOMA

MKUU wa Mkoa wa Kigoma, Emmanueli Maganga, amewataka wananchi kupima afya zao hasa wanaume na kuwaasa wasiwaachie wake zao kupima VVU na Ukimwi.

Maganga alitoa rai hiyo jana, wakati akizungumza na wananchi kwenye uzinduzi wa chanjo ya surua, rubela na polio kwa watoto wa chini ya miaka mitano katika uwanja wa Kikungu ulioko kwenye Manispaa ya Kigoma/Ujiji.

Alisema msingi mkubwa ni kupima afya wala wasiogope kuchunguzwa VVU na Ukimwi. Kadhalika, alisema watu wengi wanapopima wakishachukuliwa damu na kuambiwa wasubiri majibu, baadhi wa wananchi kwa woga huzidi kuwa na hofu. Aliwaambia ni bora waambiwe ukweli kama unaumwa au la na iwapo ukipatikana unaumwa unaanzishiwa matibabu na kupunguza makali ya VVU. Alisema ni vyema kupika kuliko kukaa kimya kwa sababu mke wako mjamzito amekwenda kliniki baada ya kupima akaonekana.

Aidha, alisema zaidi ya vipimo vya mama na watoto wameandaa sehemu ya kuwapima kinababa na kuwataka wajitokeze kwa wingi kupima VVU.

Alisema kazi ya chanjo kwa ajili ya watoto chini ya miaka mitano kwa watu wa Kigoma, ilizinduliwa rasmi, jana na kuwataka wawachanje watoto ili kuwakinga.

Alisema kila mtu anaelewa kuwa kirusi hakina matibabu hivyo kitakachofanyika ni kutoa chanjo na kuzuia watoto wasipate magonjwa nyemelezi yanayohusiana na surua. Alisema kuna wananchi wengine watoto wao wakiugua watawapa dawa za asili kama kutwanga mikonge na mapapai kwa sababu mji wao una waganga wengi wa kienyeji. Alionya kuwa kila mtu ajipange kuhakikisha watoto wote wenye umri chini ya miaka mitano wanapata chanjo ya surua, rubela na polio.

Alisema kinga ni muhimu kwa watu wote au chanjo za magonjwa malimbali na saratani mbalimbali lakini msingi mkubwa ni kupima afya wala wasiogope.

# Vifo vya kinamama, watoto vyadhibitiwa

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAISHA ya wazazi, watoto na wagonjwa ambayo huenda yangepotea kwa kukosa huduma za afya, sasa yameokolewa baada ya wadau kujenga zahanati kwa ajili ya kuwahudumia wanakijiji cha Losinoni Juu kilichoko Arumeru mkoani Arusha, kilichokuwa hakina huduma hiyo.

Zahanati hiyo imejengwa na Shirika la Friend of Tanzania-Arusha kwa kushirikiana na ndugu na jamaa waishio nchini Ujerumani, kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa huduma za kijamii kijijini hapo.

Akizungumza wakati wa kukabidhi zahanati hiyo, Mratibu wa Miradi wa Friends of Tanzania -Arusha, Harald Pfiffer, alisema wananchi wa Ujerumani walitambua changamoto ya ukosefu wa huduma za afya, ndiyo maana waliona kuna umuhimu wa kuwajengea zahanati hiyo.

Aidha, Pfiffer alisema licha ya yeye binafsi kuwa rafiki mkubwa wa wananchi wa kijiji hicho, kwa muda mrefu, safari hii ameridhishwa zaidi na uongozi wa Rais John Magufuli, kwa kuwahudumia wananchi hususani wa maeneo ya vijijini.

Alisema vijijini watu wanakabiliwa na changamoto nyingi za kijamii hivyo aliwataka wananchi kukitumia kituo hicho vizuri na kuyatunza majengo yake na vifaa ili vidumu kwa muda mrefu.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Jerry Muro, alilishukuru shirika hilo, kwa kuunga mkono juhudi za serikali ya awamu ya tano za kuwahudumia wananchi.

Muro aliwaomba wadau hao kuendelea kusaidia ujenzi wa nyumba za watumishi ili huduma hiyo, iweze kutolewa kwa saa 24 na kwa muda wote kwa mwaka.

Hata hivyo, aliwataka wananchi wa kijiji hicho, kutumia zahanati hiyo vizuri, huku akiwasisitiza kina mama wajawazito kuhudhuria kliniki kwa muda wote wa ujauzito.

Aliwataka kuacha kujifungulia nyumbani pia aliwahimiza kuwapeleka watoto wa umri wa chini ya miaka mitano kupata chanjo zote zinazowastahili.

Alisema lengo la serikali ni kupunguza vifo vya mama na mtoto, kwa kusogeza karibu huduma za afya kwa wananchi na kutumia wataalamu kupunguza matatizo yanayoweza kudhibitiwa.

Aidha, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati, kila kata ina kuwa na kituo cha afya pamoja na hospitali za wilaya na rufani kwa kila mikoa.

Ujenzi wa zahanati hiyo, imegharimu Sh. milioni 56, na hadi sasa halmashauri hiyo, imefikisha jumla ya zahanati 48, vituo vya afya saba na hospitali mbili.



Neema Mollel (kushoto), akijiandikisha kwenye daftari la wapiga kura wa serikali za mitaa kwenye kituo cha kuandikisha cha Ngusero Nairobi Shine, Kata ya Osunyai, jijini Arusha juzi. **PICHA: DANIEL SABUNI**

## Waomba baruti ipunguzwe bei

**Na Allan Isack,** MIRERANI

WACHIMBA tanzanite wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro Mkoa wa Manyara, wameiomba Wizara ya Madini kuwapunguzia kibali cha kununua baruti kutoka Sh. 100,000 hadi Sh. 20,000 kiwango walichokuwa wakilipa awali.

Wachimbaji hao waliyasema hayo, wakati kikao chao kilichofanyika Endiamtu Mjini - Mirerani na kwamba lengo la kikao hicho ni kuiomba serikali kupunguza bei ya baruti.

Abubakari Madiwa ni mmoja wa wachimbaji wa madini ya tanzanite aliyemwomba Waziri wa Madini Dotto Biteko, kuwapunguzia ada ya kiwango cha kibali cha kununua zana za milipuko kutokana na gharama hizo kuongezeka. Madiwa alisema, chama cha wachimbaji madini Mkoa wa Manyara (Marema), kinapaswa kulisemea jambo hilo, na kumwomba Waziri Biteko, kufuta kanuni elekezi kwani wachimbaji wananyonywa kutokana na kanuni hizo.

"Viongozi wetu wa Marema simameni kidete suala hili kwani wamiliki wengi wa migodi wanalalamika sana kuhusu bei ya milipuko hiyo kwani kiasi cha manunuzi ya zana za milipuko hiyo zinapandishwa siku hadi siku," alisema Madiwa.

Mmoja kati ya mameneja wa migodi, Rashid Bakari, alisema kiwango hicho siyo rafiki kwa wachimbaji madini kwani kinazidi kuwadhoofisha kiuchumi. Alisema awali walikuwa wanalipia kibali hicho, kwa Sh. 20,000, lakini ghafla bei ikapanda hadi kufikia Sh.100,000, jambo ambalo ni changamoto kubwa kwa wachimbaji wadogo wa madini.

"Haiwezekani ulipe kiasi hicho cha fedha, na unapofuata huduma hiyo, inawezekana ukapata na kukosa, lakini kwa namna yoyote ile utapaswa kulipia gharama ya Sh. 100,000 ili kupata kibali." Mjumbe wa Marema Tawi la Mirerani, Dk. Curtius Msosa, akieleza mikakati waliyoweka juu ya jambo hilo, na kusema wapo mbioni kulifikisha wizarani ili litafutiwe ufumbuzi. Msosa aliwalaumu baadhi ya watu wanaopotosha jambo hilo, kuwa kuna mtu anaweza kumaliza tatizo hilo zaidi ya kumfikishia waziri husika.

# Waaswa kuitumia mitandao kwa faida

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANAOTUMIA mitandao ya kijamii wametakiwa kuzingatia matumizi sahihi ili kuchochea maendeleo endelevu yanayotokana na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano -Tehama.

Akizungumza wakati wa kufungua mkutano Mkuu wa Jukwaa la Uongozi na Utawala wa Mitandao nchini(IGF), Mkuu wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) , Frofesa Eliamani Sidoyeka, alisema ipo haja kwa watumiaji kulenga kuleta maendeleo na si vinginevyo.

Aidha, aliishauri serikali kuweka mazingira shirikishi katika matumizi sahihi ya mitandao, yatakayonufaisha wadau na wateja wote.

Sidoyeka ambaye ni mbobezi wa masuala ya Tehama, alisema hakuna haki ya matumizi ya mitandao isiyoendana na wajibu na kwamba utumiaji wa mitandao kwa kutoa taarifa zisizo za kweli, wala tija kwa wengine ni ukiukaji wa sheria.

"Kuna taasisi nyingi wakati mitandao inaingia nchini ziliingiwa na hofu kwa kupiga marufuku matumizi ya mtandao lakini sasa hivi zimeelewa umuhimu wa teknolojia ya mitandao," alisema Sidoyeka. Mratibu wa Jukwaa la Uongozi na Utawala wa Mitandao, Nazar Nicholas, alisema mkutano huo umewaunganisha wadau wote wa mitandao, zikiwamo asasi za kiraia, mamlaka ya mawasiliano Tanzania na wataalamu wa mitandao kwa lengo la kujadili matumizi sahihi ya teknolojia ikiwamo usalama wa taarifa mtandaoni. Alisema kuwa, mkutano huo umewaleta wadau wote wa maendeleo kwa ajili ya kuzungumzia masuala yanayohusu usalama wa watoto mtandaoni na taarifa za watu.


Alisema kuwa changamoto kubwa ni pamoja na watu wamekuwa wakitumia mitandao vibaya matumizi ambayo hayapo sahihi, hivyo alisema kuna haja ya watu kuelimisha juu ya mambo ya kuzingatia yakiwamo utu na maadili.

Aidha, aliwataka vijana na wazazi kuangalia namna ya kutumia mitandao kwa ajili ya manufaa endelevu ambayo yatasaidia kuleta tija katika maisha ya kila siku.

Mmoja wa watoa mada ambaye ni Mkurugenzi wa Klabu za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC) Abubakar Karsan, alisema mitandao imekuwa na faida kubwa katika kuchochea maendeleo ikiwamo kwa wanahabari kupeleka taarifa zao kupitia teknolojia mtandao.

Alisema mitandao imekuwa ikitumika kwa ajili ya taarifa na huduma afya, elimu na utawala bora, hivyo alitoa rai kwa serikali kupeleka mitandao nchi nzima na wananchi waweze kupata huduma hiyo kwa bei nafuu kwa ajili ya kuchochea kasi ya maendeleo.

Vilevile, alisema kuna haja ya kutoa elimu na njia sahihi za kutumia mtandao ili watu waweze kufanya shughuli zao kupitia mitandao kwa lengo la kuendeleza mambo mfano biashara, uwekezaji, elimu na mawasiliano.





# DC aanza kusikiliza kero za watumishi wa umma

**Na Godfrey Mushi,** SAME

MKUU wa Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule, ameanza kusikiliza kero za watumishi wa umma zaidi ya 2,500.

Aidha, ameagiza waajiri kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi ambao hawaonekani kwenye vituo vya kazi.

Alisema kutokana na utafiti uliofanyika kwenye maeneo ya huduma, moja ya matokeo yanaonyesha baadhi ya watumishi ni watoro.

Senyamule alisema: "Ninaendelea na vikao kwa kukutana wa watumishi wote ili kuwaeleza mafanikio ya serikali kwa kipindi cha miaka minne ya Rais John Magufuli kuanzia mwaka 2016/2019. Na huko nasikiliza pia kero zao pamoja na kutoa maelekezo mbalimbali ya serikali.

"Kama tunawaeleza wananchi, viongozi wa dini, asasi zisizo za kiserikali (NGOs), wafanyabiashara, makundi mbalimbali pamoja na wadau juu ya mafanikio ya serikali na tunasikiliza kero zao, kwa nini nyie watumishi wa serikali tusikae nanyi na kuwasikiliza?"

Aliwaambia ni muhimu pia nao kusikilizwa kero zao na kuzitatua ili wawatumikie Watanzania kwa moyo mkunjufu.

Mkuu huyo wa wilaya alianza jana kusikiliza kero za watumishi hao akianzia na Tarafa ya Gonja, yenye kata nne na kukutana na watumishi zaidi ya 150.

Katika kikao chake, aliahidi kuzitatua kero zinazowakabili watumishi hao kwa wepesi zile ambazo zipo ndani ya uwezo wa Halmashauri ya Wilaya ya Same na kufuatilia zinazoenda ngazi za juu.

Katika hatua nyingine, Mkuu wa Wilaya ameeleza kuwa mchakato wa uwekezaji katika wilaya hiyo umeanza kupata mafanikio makubwa, baada ya Rais wa Taasisi ya Kimataifa ya Foundazione Same ya nchini Italia Fransisco Carozza, kuthibitisha rasmi kwamba atawekeza katika sekta ya viwanda au elimu.

Carozza anamiliki asilimia 100 ya hisa za uwekezaji wa kiwanda cha utengenezaji wa matrekta nchini Italia.

Kwa mujibu wa Senyamule, pia Carozza ameeleza kuridhishwa kwake na sera nzuri ya uwekezaji, akisema Tanzania ni sehemu nzuri ya uwekezaji kutokana na kuwa na soko la uhakika, nguvu kazi na bandari lakini kubwa zaidi ni sera mbalimbali zimefanyiwa kazi.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Yohana Sintoo (kulia), akijibu kero ya kujaa maji katika soko la walaji la Bomang'ombe juzi, ambapo alilipatia ufumbuzi kwa kuwekwa moramu. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Atumia viongozi wa vyama kuhamasisha uandikishaji

**Na Godfrey Mushi,** SIHA

WAKATI jana ilikuwa siku ya mwisho ya kuandikisha wapiga kura uchaguzi wa serikali za mitaa, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira, ameagiza viongozi wa CCM, Chadema na SAU kupewa usafiri kuwafikia wananchi.

Viongozi hao walitakiwa kuwazungukia na kuwahamasisha wananchi kwenye maeneo yote yaliyo chini ya viwango vya uandikishaji ili wajitokeze kujiandikisha na kupiga kura Novemba 24.

Zoezi hilo la uandikishaji wapiga kura lilifungwa rasmi jana, baada ya serikali kutoa nyongeza ya siku tatu. Tangazo la kuongezwa muda wa uandikishaji Jumapili iliyopita Oktoba 13 mwaka huu na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo.

Akiwa katika Kijiji cha Matadi, Kata ya Endumeti, Wilaya ya Siha, Mghwira, alitoa maelekezo kwa viongozi hao wa vyama kuruhusiwa kupita sehemu mbalimbali kuhamasisha wananchi wajitokeze kujiandikisha katika muda uliokuwa umebakia.

Uchaguzi huo wa serikali za mitaa, vijiji na vitongoji, unatarajiwa kufanyika Novemba 24 mwaka huu nchini kote.

"Wapewe gari hawa viongozi wa vyama na wapite huku na huko wahamasishe wananchi wajitokeze kujiandikisha katika muda huu uliobakia," aliagiza Mghwira.

Hoja ya kutaka kutumika kwa viongozi hao wa vyama vya upinzani kutoa hamasa iliwasilishwa juzi kwa Dk. Mghwira na aliyekuwa mgombea Ubunge wa Jimbo la Siha katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015, Azaria Mdoe wa chama cha SAU. Juzi, Waziri Jafo alinukuliwa akisema mkoa wa Kilimanjaro unashika nafasi ya mwisho kwa uandikishaji wapigakura ukiwa na asilimia 48, ukifuatiwa na Kigoma yenye asilimia 53 na Arusha asilimia 59.

Hadi kufikia Jumatatu ya Oktoba 14 saa 12 jioni, kwa mujibu wa Waziri Jafo, Watanzania milioni 15.54 sawa na asilimia 68 walikuwa wamejiandikisha katika daftari la wapiga kura.

Katika hatua nyingine, Dk. Mghwira alitoa saa 72 kupelekewa majina ya viongozi wote wa serikali katika Wilaya ya Siha, ambao wanashindana na wananchi kuchukua vitalu katika shamba la Miti la Taifa la West Kilimanjaro. Uamuzi huo wa Mghwira unatokana na malalamiko ya wakazi wa Kata ya Endumeti, kwamba viongozi wa wilaya hiyo ya Siha wamejigawia vitalu na wanalima mazao mbalimbali, huku wananchi wakikosa maeneo ya kilimo.

# Chama chaapa hakisusi uchaguzi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KATIBU wa Chama cha Sauti ya Umma (SAU) mkoani Kilimanjaro, Isaac Kireti, amesema chama hicho kitashiriki kikamilifu katika uchaguzi wa serikali za mitaa Novemba 24, 2019 kwa kusimamisha wagombea katika maeneo yote ya Manispaa ya Moshi.

Kireti alikuwa akizungumza jana na Nipashe katika mahojiano maalum kuhusu hali ya uandikishaji wapiga kura unavyosuasua katika Manispaa ya Moshi na nia ya chama chake kushiriki uchaguzi huo.

Katika mahojiano hayo maalum, Kireti alisema miongoni mwa mambo ambayo chama hicho hakiwezi kuthubutu kufanya ni kususia uchaguzi huo au uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2020 wa Rais, wabunge na madiwani.

Pamoja na kwamba kuna hali tete ya kisiasa tuliyonayo hatuwezi kususia uchaguzi, kususia sio dawa ya kuleta mabadiliko, lazima tukashindane, tujipime na tuone wapi tunapaswa kufanya maboresho au kuongeza nguvu ili siku moja tupate viongozi wa kutosha katika serikali," alisema Kireti alipoulizwa endapo chama chake kinatarajia kushiriki uchaguzi.

Mwaka 2015, Kireti alikuwa mgombea ubunge wa Jimbo la Moshi Mjini, kwa tiketi ya SAU.

Kwa sasa, Kireti ameeleza kuwa tayari chama chake kimempatia ridhaa ya kugombea nafasi ya ujumbe wa serikali ya Mtaa wa Bondeni, Manispaa ya Moshi, licha ya ukweli kwamba bado ana nia ya kugombea ubunge katika uchaguzi mkuu ujao.

Chama hicho cha SAU katika Manispaa ya Moshi hakina kiongozi yeyote aliyewahi kuchaguliwa kuongoza mtaa, kitongoji, kijiji, diwani wala mbunge.

"Kwanza, chama changu kimejipanga vizuri kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa na sasa tupo kwenye mchujo wa majina ya wagombea waliojitokeza na majina yao tutayawasilisha kunakohusika," alieleza katibu huyo.

Alisema ana imani endapo haki itatendeka, chama hicho kitafanya vizuri zaidi katika chaguzi huu kuliko uchaguzi uliopita, kwa kuwa mazingira sasa yamebadilika na chama kimeboreshwa zaidi.

Akizungumzia hali ya wananchi kushindwa kujitokeza kujiandikisha katika daftari la wapiga kura, Kireti alisema imetokana wananchi kukosa hamasa ya kutosha kuhusu uchaguzi huo.



Ukurasa 15

Kenya yazindua SGR nyingine



Ukurasa 16

Kuuza asali kwa wingi nje kunavyosuasua kitaalamu



Ukurasa 14

## Wakulima kinamama magwiji wa maharage wasaidiwa kuokoa 25%


# BUFE

Ijumaa Oktoba 18, 2019

Nipashe

BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA




# KUMKOSOA NYERERE KUNAVYOPISHANA NA UCHUMI

**Na Profesa Godius Kahyarara**

MTU anapotafsiri mfumo wa uchumi wa Rais wa Kwanza, Mwalimu Julius Nyerere, ni kwamba uliangukia ujamaa wa kidemokrasia, uhuru wa kiuchumi, kujitegemea, usawa haki na fursa ya kumiliki na kunufaika na uchumi wa kitaifa.

Kiongozi huyo alichukia mfumo wa kinyonyaji uchumi duniani na umuhimu wa nchi kusimamia uchumi, kujitosheleza kwa kujenga viwanda na kupunguza utegemezi wa bidhaa za nje.

Mwalimu Nyerere, alikataa masharti ya vyombo vya fedha vya kimataifa; Shirika la Fedha Duniani (IMF) na Benki ya Dunia, yaliyokuwa kinyume na sera na mwelekeo wa Tanzania wakati ule.

Madhara ya masharti hayo, yalionekana katika kulazimisha mashirika hayo kubadili mtazamo na kuanzisha Mikakati ya Kuondoa Umasikini na Nafuu ya Madeni, mambo ambayo Mwalimu Nyerere aliyatabiri mwaka 1979.

INAENDELEA UK.18

UCHUMI

## Habari katika picha




Ukurasa 17

## Wasomi Tanga wanavyochangamkia ufugaji ng'ombe, wakiipa kisogo ajira

Ukurasa 20

BIASHARA

# Wakulima kinamama magwi maharage wasaidiwa kuoko

• Mashine maalum inayokausha mazao • Walianzia gunia 10 le

**Na Nebart Msokwa,** Mbeya

KILIMO ni sekta inayoongoza kuajiri Watanzania wengi, wakishiriki kuzalisha mazao ya aina mbalimbali, yakiwamo ya vyakula na biashara zitonakazo, vyote vikiwa na muhimu kwa ustawi wa uchumi kitaifa, pia usalama wa chakula.

Mbeya ni miongoni mwa mikoa ambayo wananchi wake wanajishughulisha na kilimo kwa asilimia kubwa, hali inayoifanya kuwa juu katika hadhi ya mikoa ijulikanayo kama 'Ghala la Taifa la Chakula' ukiungana na mengine ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini.

Katika orodha hiyo, inajumuisha maharage ni miongoni mwa mazao yanayozalishwa kwa kiwango kikubwa katika mkoa huo, kutokana na hali ya hewa nzuri inayoambatana na mvua za kutosha kuwezesha zao hilo kustawi.

Wakulima wengi wanashawishika kuzalisha zao hilo, kutokana na kuwapo soko la uhakika ndani na nje ya nchi na matumizi yake inaongezeka, tofauti na ilivyokuwa awali inatumika kwa ajili ya chakula pekee.

Taarifa za soko la maharage Mkoa wa Mbeya zinaonyesha kuwa yanauzwa kwa bei ya kati ya Sh. 28,000 mpaka 40,000 kwa kilo 20, kulingana na hali ya uzalishaji katika maeneo tofauti ya mkoa.

Baadhi ya wakulima wamekuwa wakichangamkia fursa ya kuzalisha zao hilo na wapo wanaozalisha kupitia kampuni, vikundi na mkulima mmoja mmoja, kulingana na uwezo wao kiuchumi.

**KINAMAMA WA ZINDUKA.**

Kikundi cha wanawake kinachoitwa 'Zinduka' kipo katika Kata ya Mshewe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, imo katika orodha ya wanaochangamkia fursa hizo.

Mwenyekiti wa kinamama hao, Witness Sikayange, anasema walianzisha kikundi mwaka 2010 na kina wanachama 21, wote kinamama.Walianza na kulima ekari 10, lakini mpaka sasa wanalima ekari 300.

Witness anasema, baadhi ya mashamba waliyanunua kutokana na faida walizopata kwenye kilimo hicho na kuna ekari 100 walipewa na Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza na yapo ambayo ni maeneo yao ya asili.

Kuhusu mbinu za ulimaji, anasema awali walitumia mbinu za asili na mbegu za kienyeji, hali iliyochangia kuwapo kupata tija ndogo kwa kupata kilo 100 kwa ekari wakati tafiti za kitaalamu zikionyesha kuwa katika eneo hilo mkulima anatakiwa kupata kilo



Mratibu wa Mtandao wa Utafiti wa Maharage Kusini mwa Bara la Afrika, Rolland Chirwa (kushoto), akipeana mkono na Mwenyekiti wa Kiku ness Sikayange, kuashiria kukabidhiana mtambo wa kukaushia maharage, uliotolewa na shirika la kimataifa la CIAT. **PICHA ZOTE: NEBART M**

> Kikundi cha wanawake kinachoitwa 'Zinduka' kipo katika Kata ya Mshewe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, imo katika orodha ya wanaochangamkia fursa hizo.



Wanachama wa Kikundi cha Zinduka, kilichoko katika Kata ya Mshewe, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wakiimba na kucheza kuzunguka mtambo wa kukaushia maharage, unaotumia nishati ya jua, baada ya kupatiwa na taasisi ya CIAT.

# iji wa
# a 25%

## eo wamefika 300



ndi cha Wanawake cha Zinduka, Wit-
**MSOKWA.**



800 kwa ekari.

Anasema wataalamu kutoka katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (Tari), kutoka Kituo cha Uyole jijini Mbeya, waliwasaidia kuwapa elimu kuhusu kilimo bora pamoja na kuwapatia mbegu za kisasa ambazo ziliwaletea matokeo chanya.

"Walitufundisha matumizi ya mbegu bora za maharage, matumizi ya mbolea, pamoja na viuatilifu na baada ya kuanza kuzitumia uzalishaji uliongezeka na mpaka sasa tunapanda kilo 30 za mbegu na tunavuna kilo 800 kwa ekari moja na kukiwa na hali ya hewa mbaya, tunavuna sio chini ya kilo 600," anasema Witness.

Anafafanua kwamba, huwa wanalima awamu tatu kwa mwaka, ambazo ni awamu mbili kipindi cha masika na awamu moja kiangazi, kupitia mfumo wa umwagiliaji unaotokana na eneo hilo kuwa na utajiri wa maji.

Pia, Witness anasema kikundi hicho kilisaidiwa na taasisi zingine, ikiwamo Taasisi ya Kilimo Trust iliyoshirikiana na kampuni nyingine kuwajengea ghala la kuhifadhi mazao kabla ya kuyauza.

Vilevile, anasema kampuni hiyo ya kwanza, ambayo pia ni mteja mkuu wa maharage wanayozalisha, iliwasaidia mizani ya kidigitali kupimia mazao hayo, badala ya vipimo vya asili ambavyo havikubaliki kibiashara nchini pamoja na kipimo cha uyevu ya barometa.

Anasema, hivi sasa wamezalisha vikundi vingine viwili anavyovitaja kuwa ni Mshebhaje kinachojumuisha wazee, pamoja na Mshewe Jikomboe Kijana, kwa ajili ya vijana wa kiume.

Katibu wa Kikundi hicho, Andusamile Mbandile, anasema kutokana na kilimo cha maharage, hali yao kiuchumi imeimarika na wamejenga nyumba bora wanazoishi, kununua miradi ya vyombo vya usafiri kama pikipiki na kumudu kuwasomesha watoto.

Andusamile anasema, kwa sasa wameanza kuyatumia kuzalisha bidhaa mbalimbali kama bagia, sambusa, maandazi na unga wa lishe, wakitumia maharage yenye madini ya Zinki. Katibu anaongeza, kwa sasa wameanza kusindika maharage na kuyauza kwa ajili ya chakula, wakiyachemsha na kuyakausha kuwarahisishia wateja.

### KUPOTEZA MAZAO

Anasema, pamoja na kuzalisha maharage kwa wingi, wamekuwa wakikabiliwa na changamoto ya hali ya hewa katika kipindi cha mvua, wakishindwa kuyakausha kwa ufasaha mazao yao, hivyo yanaoza.

Wataalamu kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari), kituo cha Uyole, wanasema walibaini kikundi hicho pamoja na wakulima wengine wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanapoteza asilimia 25 ya mazao yao kutokana na hali ya hewa.

Mratibu wa Utafiti na Ubunifu wa Tari, Dk. Ndabhemeye Mlengera, anasema Wilaya ya Mbeya, kipindi cha masika huwa na mvua za muda mrefu, inayochangia mazao kukauka na yanaoza, yakiwa ama shambani au yanapohifadhiwa ndani baada ya kuvunwa. Wanashindwa kuyakausha kwa kiwango kinachotakiwa.

"Mazao mengi wanavuna kipindi cha mvua nyingi na kutokana na teknolojia ndogo ya ukaushaji, wanajikuta sehemu kubwa ya mazao yanaharibika kwa kuoza. Yanaoza wakiwa wameyahifadhi ndani ya nyumba au yakiwa shambani," anasema Dk. Mlengera.

### WAPATIWA MTAMBO

Changamoto hiyo ya ukaushaji maharage iliifanya Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Mazao ya Kitropiki - CIAT, kukiwezesha kikundi cha Zinduka kupata mtambo wa kisasa wa kukausha maharage, unaotumia nishati ya Jua (Bean Solar Drier).

Ni mtambo huo unaoelezwa kuwa na uwezo wa kukausha mpaka kilo 1000 za maharage kwa siku moja, kwa muda wa kati ya saa mbili hadi tatu, manufaa yakisogeswea hadi kwa wananchi jirani wa Kata ya Mshewe, wanaozalisha mazao hayo.

Akiwakabidhi mtambo huo kwa niaba ya CIAT, Mratibu wa Mtandao wa Utafiti wa Maharage Kusini mwa Bara la Afrika, Rolland Chirwa, anasema walichukua uamuzi huo wa kukisaidia kikundi mashine, lengo ni kuepuka hasara ya kupoteza mazao.

Chirwa anasema, ni mtambo unaomuwezesha mkulima kuanika mazao, huku akiendelea na shughuli ingine za uzalishaji pasipo hofu ya mazao ama kunyeshewa au kuliwa na mifugo.

Kwa mujibu wa Chirwa, ni mtambo utakaosaidia kuwaongezea tija wakulima kupitia ukaushaji maharahe kwa ufasaha na kufikia kiwango cha unyevunyevu wa chini ya asilimia 15.

"Hiki ni kikundi ambacho kina mafanikio makubwa, lakini wanaposhindwa kukausha vizuri mazao yao, kuna hatari ya mazao hayo kutengeneza sumu kuvu, ambayo ni hatari kwa afya. Pia, maharage yakioza, yanakosa soko na ndio maana tumewapa mtambo huu," anasema Chirwa.

Anasema mtambo huo mbali na kuwasaidia wakulima kukausha maharage, pia utawasaidia kukausha mazao mengine wanayozalisha na kwamba una uwezo wa kufanya kazi hata kama kuna hali ya hewa yenye mawingu.

### MENEJA UTAFITI

Meneja wa Mradi wa Utafiti katika Kilimo Endelevu kwa Ajili ya Vizazi Vijavyo wa Tari - Uyole, Leonard Sabula, aliyekiunganisha kikundi cha kilimo na taasisi wawekezaji, anasema kwa sasa kunatakiwa kuunganisha nguvu ya wadau kufikia lengo la kuongeza uzalishaji.

Sabula ambaye pia ni Mtafiti kutoka katika Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (Tari), Kituo cha Uyole Mbeya, anasema kuna wadau wanaotekeleza miradi mingi na kila mmoja anamlenga mkulima, kitu anachokitafsiri kuwachanganya wakulima.

Mtafiti huyo anasema, amewaunganisha wakulima kuzalisha maharage lishe yenye madini ya chuma na zinki na kikundi hicho 'kilijiongeza' kwa hatua zaidi ya kuzalisha aina zingine za maharage.

"Ili mkulima aweze kufikia lengo lake anatakiwa kupatiwa huduma iliyokamilika na hii itafikiwa endapo wadau tofauti tutaungana kwa pamoja kama ilivyofanyika kwenye kikundi hiki ambacho kinasaidiwa na wadau tofauti lakini kwa pamoja," anasema Sabula.

# Kenya yazindua SGR nyingine




Ujenzi wa stesheni ya Kisasa Nairobi.



Kituo cha treni jijini Nairobi. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Nairobi, Kenya**

RAIS Uhuru Kenyatta wa Kenya, amezindua mradi wa reli ya kisasa maarufu SGR utakaounganisha Uwanja wa Kimataifa wa Jommo Kenyatta hadi katikati ya jiji la Nairobi.

Ni reli inayotarajiwa kupunguza msongamano mkubwa wa magari na kugharimu Dola za Marekani milioni 6.

Barabara hiyo ya moja kwa moja, ni sehemu ya mpango wa serikali wa kupunguza msongamano wa magari katika jiji la Nairobi, ambalo idadi ya watumiaji wa magari inazidi kuongezeka.

Benki ya Dunia ilikadiria kwamba Kenya inapoteza kiasi cha Dola za Marekani 5,000 kila siku kutokana na misongamano ya magari, huku kuna idadi kubwa ya watu wanaopoteza muda wao kwenye misongamano hiyo.

Msongamano wa magari, pia inachangia wasafiri kukosa safari zao za ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jommo Kenyatta.

Rais Uhuru, akizindua mradi huu baada ya benki ya dunia kujiondoa kwenye ubia na serikali ya Kenya, anasema: "Wengine wanasema ooh, hii reli inaenda wapi? Hakuna kitu kibaya kama...wa mtu ambaye fikra zake ni namna hii. Sasa sisi tukisema tunajenga hii kusaidia wananchi, tatizo iko wapi?."

Mradi huo unakuja baada ya ziara ya Rais Kenyatta mwezi uliopita nchini China, alikohudhuria kongamano lililowaleta pamoja viongozi wa Afrika na wawekezaji.

Pia, kuna mradi wa barabara unaotekelezwa na kampuni ya ujenzi wa barabara na madaraja ya China, kwa ushirikiano na serikali ya Kenya.

Inakadirikwa kuwa kuna magari 60,000 yanayotumia barabara hiyo kutoka uwanja wa ndege wa kimataifa wa Jommo Kenyatta hadi eneo la Westland kila siku.

Njia hiyo ikikamilika, idadi ya watumiaji magari itaongezeka kwa magari 25,000, ikiwa na urefu wa kilomita 17 wakitumia muda mfupi kati ya dakika 10 hadi 15 kutoka katikati ya jiji.

BIASHARA

SOKO LIKO BAYANA, TATIZO?

# Kuuza asali kwa wingi nje kunavyosuasua kitaalamu

• Kitendawili cha wizara, watendaji wake



Mtaalamu wa kuhudumia asali akitundika mzinga wa nyuki.

**Na Nimi Mweta**

MALUMBANO ya kitaaluma na kiutendaji yamesikika hivi karibuni kati ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa upande mmoja na Wakala wa Misitu Tanzania (TFS), kuhusu upatikanaji asali ya kutosha kupelekwa nchi za nje ambako kuna soko kubwa na uwezo mpana wa kuzalisha.

Inavyoelekea mjadala huo ni mgumu kiufundi, kwani unatokana na kuangalia suala hilo kwa pande mbili tofauti siyo rahisi kupata mahali pa kusimama, mbali na wizara au wakala.

Naibu Waziri, Constantine Kanyasu, anasema kushindwa kwa Tanzania kupeleka asali nyingi katika masoko yanayongoja tu bidhaa hiyo ifike, ni tatizo la usimamizi kwa upande wakala, ambako alidai mabadiliko.

Kimsingi, wizara na wakala wanatofautiana kuhusu kiwango gani cha uzalishaji kinawezekana, kutokana na misitu iliyopo na idadi ya makoloni (vituo) vya nyuki ambavyo vina viwango vinavyojulikana vya uwezo wa kuzalisha unaojulikana.

> **Kimsingi, wizara inataka uwezo wa uzalishaji ufikiwe kama ulivyo, huku ufafanuzi wa wakala unatoa picha ya kuongezeka taratibu uwezo uliopo.**



Asali ambayo iko tayari kutumiwa. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Wizara inaanzia katika taswira hiyo pana ya misitu, vitalu (maeneo) vya nyuki na ufanisi wa uzalishaji ambao haufikii viwango. Utawala wa TFS unajenga hoja kwa mantiki tofauti ya mahitaji ya soko la nje kwa misingi kile kilichopo, kiinuliwe.

Naibu Waziri aliitaka TFS ifanye marekebisho ya kiusimamizi au kiutawala ili ufanisi wa sekta ndogo ya asali uinuke, kuwezesha asali ya Tanzania kufikia masoko Marekani, Ulaya na Asia, hasa China.

Maelezo ya wizara katika hadhara hiyo, yalilenga zaidi uwezo wa kuzalisha na siyo mazingira yake kama uwakala wa misitu ulivyofafanua. Suala lililopo ni kama viwango vya uzalishaji, ambavyo wizara ina kila sababu ya kutazamia vinaweza kufikiwa viendane na uhalisia.

Takwimu za wizara, zinaonyesha uwezo wa kuzalisha asali na bidhaa za ziada za nyuki unafikia tani za metriki 138,000, kutokana na kuwapo 'makoloni' milioni 9.2 ya nyuki wa asali.

Wizara husika inasema, kiasi hicho cha uzalishaji kinawezekana endapo kila 'koloni' linatoa kiasi cha kilo 15 za asali na kilo moja ya nta kwa mwaka. Wizara inapata shida kueleweka kwanini kunazalishwa tani za metriki 30,430 za asali kuuzwa nje, ambayo ni chini ya robo ya uzalishaji tarajiwa.

Wizara inaamini kwamba hakuna ushirikiano wa kutosha ili kuongeza uzalishaji uliopo kati ya wakala na mikoa muhimu ya uzalishaji asali, yaani Tabora, Dodoma, Singida, Shinyanga, Geita, Kigoma, Mbeya na Katavi. Pia, kuna matazamo wa pengo la ushirikiano kati ya Wakala wa Misitu na Chuo cha Ustawishaji Nyuki (BTI) huko Tabora, suala ambalo halikujitokeza kwa kina katika maelezo ya wakala.

Kimsingi, wizara inataka uwezo wa uzalishaji ufikiwe kama ulivyo, huku ufafanuzi wa wakala unatoa picha ya kuongezeka taratibu uwezo uliopo.

## UGUMU UNAPOJIONYESHA

Wakati wizara inatazamia kuwa nyenzo za kufikia ustawishaji stahili wa nyuki na upatikanaji wa mazao yake tayari zipo, wakala inatoa picha kuwa uwezo wa kuzalisha unaongezeka taratibu.

Kwa upande wa mauzo nje, wakala inagusia mahitaji ya kiufundi na kiteknolojia ili kuweza kupeleka asali kwa wingi katika masoko ya nje, kwa mfano ujazo unaohitajiwa kupata mkataba kupeleka asali, kwa mfano kwa mwaka mmoja. Pia, kuna masuala ya ubora ambayo wakala inafuatilia.

Kwa maana hiyo, wakala inaashiria siyo rahisi kufikia kuzalisha au viwango vinavyohitajiwa kutokana na sababu ambazo kwa maana hiyo ziko ndani ya uwezo na inabidi ziendelee kuzishughulikiwa kwa hatua.

Picha ya wizara iko katika mwelekeo wa 'matokeo makubwa sasa'na inatazamia inawezekana kufikia malengo hayo, wakati upande wa wakala unahisi si mkubwa kuhusu soko, kwa maana ya kuwapo kiwango fulani cha uwezo wa kuzalisha na ubora unaokubalika sokoni, wakati ikiendelea kuboreshwa viwango, kuwafahamisha wanunuzi kushiriki maonyesho tofauti.

## MTIHANI WAKE

Mtu anaweza kujiuliza, kuna tatizo lolote la ushirikiano au mawasiliano kati ya utendaji wa TFS (wasimamizi wa misitu nchini) na chuo cha uendelezaji sekta ndogo ya nyuki wa asali.

Tatizo linaonekana kwa upande wa wizara siyo hitilafu halisi iliyotokea, ila kutokana na kutokuwapo ufanisi wa kutosha kwa mahitaji hayo, ina maana kuwa tatizo halipo katika ushiriki wa chuo hicho, BTI.

Hapo kuna suala la mifumo ya upatikanaji mitaji ya kuendeleza rasilimali hiyo, uvunaji na kuyasambaza zaidi.

Moja ya matatizo yanayoonekana huenda kuisumbua wizara, ni kushindwa kufikia ujazo wa bidhaa hizo (asali na nta) unaotakiwa katika masoko yaliyopo, au nafasi ndogo kutokana na ujazo uliopo tayari kupeleka mara moja au kila mara.

Kuna masuala ya viwango vya ubora ambavyo wakala anasema kwa kawaida TFS inashiriki maonyesho na hata kupeleka maabara tofauti nje ya nchi, ambayo ina maana ni kupata vyeti kutoka mamlaka tofauti za uthibitishaji ubora wa bidhaa hiyo.

Ndiyo tatizo la kuuza kitu chetu wenyewe, bila mwekezaji wa nje anayefahamika, ambaye akitia muhuri bidhaa hiyo inapenya masoko hayo kirahisi.

Maelekezo ya wizara yalihusu umuhimu wa ushirikishwaji vyama vya wafugaji nyuki (na warina asali) kana kwamba kuna suluhisho au njia wanayoweza kuleta mezani kuhusu nini cha kufanya.

Kilichojificha hapo ni kuwa wafugaji nyuki na warinaasali wanahitaji mitaji kuendeleza biashara hiyo ifikie ngazi nyingine.

Lakini, inaoonekana kama ilivyo kwa wakulima na wafugaji wa jumla, siyo rahisi ngazi ya ufugaji mtu mmoja mmoja. Anayeweza ni mwekezaji anayejenga kiwanda cha kusindika asali kwa ubora wa kimataifa na jina fasaha.

Ufasaha wa jina ni kumthibitishia mlaji kuwa, bidhaa aliyonayo ni le aliyozoea.

Ina maana kuwa iwepo tofauti ndogo tu ya kampuni kununua asali au korosho kama malighafi au kama bidhaa iliyokamilika ili isiwe vigumu kwao kununua nchini badala ya nje ya mipaka.

Ndivyo nchi zinavyoingia kwenye soko la kimatifa. Ni jitihada kuchangamana na soko kimatifa iwe ni mtiririko huo huo wa malighafi na bidhaa zilizokamilika au kampuni husika inakuwa ni anuani tu.

# Biashara katika picha



Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Tigopesa wa Kampuni ya Tigo, Angelica Pesha (kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 5 kwa mshindi wa kwanza wa promosheni ya 'Tigopesa Wakala', Suleiman Husein kutoka Zanzibar, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam juzi. Katikati ni Mkurugenzi wa Tigo, Kanda ya Pwani, Joseph Mutalemwa. **NA MPIGAPICHA WETU**



Mfanyabiashara mdogo akiwa amepanga bidhaa zake wakati akisubiri wateja katika eneo la Tandika, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**



Wachuuzi wa bidhaa mbalimbali wakizinadi kwa abiria walioko kwenye basi katika kituo cha daladala cha Mbezi Mwisho, Manispaa ya Ubungo, jijini Dar es Salaam, mapema wiki hii. **PICHA: SABATO KASIKA**

UCHUMI

MIAKA 20 BILA BABA WA TAIFA

# KUMKOSOA NYERERE KUNAVY

- Hakuuvaa Ukomunisti, wala Ujamaa Mapindu
- Shida haikuwa Ujamaa, bali mitikisiko kiuchu

INATOKA UK.13

Wakosoaji wa Sera za uchumi za Mwalimu Nyerere, baadhi yao waenda mbali na majibu mepesi kuwa Mwalimu Nyerere, hakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu masuala ya uchumi.

Lakini kiuhalisia, kiongozi huyo wa nchi, msomi wa kiwango cha juu, akiwa na shahada ya uzamili aliyosomea fani za Uchumi, Siasa, Anthropolojia ya Jami, Sheria ya Katiba na Faslsafa ya Kiimani.

Ni katika zama watu hizo wachache walipata fursa ya kusoma mchanganyiko huo wa kitaaluma. Kimsingi, anthropolojia, inatafsirika kuwa "elimu ya binadamu inayohusiana na habari za asili na maendeleo yake ya awali."

Hivyo, Rais Nyerere, alikuwa na uwezo mkubwa kimataifa katika kufuatilia na kushiriki mijadala na mipango ya uchumi kimataifa na ule wa nchini.

### ALIKOSIMAMA KIUCHUMI

Mwalimu Nyerere aliamini katika ujamaa wa kidemokrasia, ambao ni tofauti sana na ukomunisti, uliojikita katika falsafa za Kina Karl Marx na Fredick Engels chini ya muunganiko wa nchi za kisoshalist kama za Urusi, China au Cuba, zilizojikita katika mapinduzi ya wanyonge walionyonywa na mabepari na kutawala dola.

Ujamaa aliousimamia Mwalimu Nyerere, chimbuko lake ni Ulaya Magharibi na unajulikana kama Ujamaa wa Kidemokrasia (Fabian system) na ulianzia Uingereza na nchi za Ulaya.

Tofauti na mifumo hiyo mingine ya kijamaa, huo una sura ya hiari na umekuwapo kwa muda mrefu na bado unaishi.

Vyama kama vya Democrat nchini Marekani au Labuor ya Uingereza na nchi za Singapore, Emirates, Scandinavian, India na barani Asia, nyingi sera zake zinaangukia chungu kimoja na siasa za Mwalimu Nyerere.

Mtandao wake umejikita zaidi kwa wanyonge, wenye asili tofauti na Marekani hasa weusi na jamii ya kiasia na msingi mkuu wa chama, ni usawa wa kijamii na kiuchumi, ukihimiza serikali kusimamia sera za kiuchumi kusaidia vyama vya wafanyakazi kumlinda mlaji na yale ambayo Mwalimu Nyerere aliyasimamia.

Kadhalika, chama cha Labor cha Uingereza, hata baadhi ya wasomi, wamekuwa wakihoji kwanini CCM haijabadili sera zake? Hapo inazaa swali jingine, kwanini Mwalimu Nyerere aliamini katika mfumo huo wa ujamaa wa kidemokrasia katika kujenga uchumi?

Ilikosimamia imani ni kwamba, kutokana na muundo wa maisha ya Waafrika, ikiwamo Tanzania, maisha ya jamii kushirikiana, kusikilizana na kujadiliana, mfumo sahihi



Kituo cha Utafiti Ukiliguru (Mati) Mwanza.

> "Ujamaa aliousimamia Mwalimu Nyerere chimbuko lake ni Ulaya Magharibi na unajulikana kama Ujamaa wa Kidemokrasia (Fabian system) na ulianzia Uingereza na nchi za Ulaya.



Bidhaa ya korosho iliyofanyiwa ukaguzi katika Kituo cha Utafiti Kilimo, Ilonga Kilosa. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

wa maendeleo yao ungekuwa huo wa ujamaa wa kidemokrasia.

Msimamo ulikuwa ni kupigania uhuru wa kiuchumi, unaoshirikisha wananchi kupanga na kumiliki uchumi wa nchi yao, umma kumiliki rasilimali za taifa na kwa maendeleo ya kitaifa.

Mtazamo wa Mwalimu, alisimamia dhana Afrika kuwa na nguvu ya pamoja, ili ijitawale kiuchumi, iheshimike na kuwa na sauti katika mfumo wa uchumi wa dunia, kwa kuondoa unyonyaji hasa katika uuzaji bidhaa nchi za viwanda na kupangaji bei.


Jingine, kiongozi huyo wa nchi alisimamia biashara baina ya nchi za Afrika kupitia OAU, kundi la mataifa 77 masikini na kushiriki katika mikataba kama ya Lome

Iko wazi aliwaongoza Watanzania kuanzisha ujenzi wa uchumi wa kijamaa wa kidemokrasia. Msingi mkuu ulikuwa ni uchumi uliojikita katika usawa na kuheshimiana; kuwapa haki raia nchini kumiliki

# YOPISHANA NA UCHUMI

uzi
umi







Uzalishaji ukiendelea ndani ya kiwanda cha nguo Mwatex, Mwanza.

uchumi ; kutoa haki ya kupata hifadhi ya maisha na mali liyo nayo kwa mujibu wa sheria.

Mengine ni kuhakikisha haki ya malipo halali ya kazi; umiliki rasilimali za nchi kama dhamana kwa vizazi vijavyo na wajibu wa serikali kuhakikisha inasimamia ukuaji wa uchumi.

Njia kuu za uchumi ikiwamo viwanda, benki, mashamba makubwa, nyumba za kupangisha, migodi na rasilimali nyingine zilitaifishwa na kuhamishiwa milki ya umma.

**HATUA YA MAFANIKIO**

Katika kutekeleza mipago na mtazamo wa uchumi chini ya Mwalimu Nyerere, mafanikio makubwa ya viwanda yalipatikana, hasa kufikia katikati ya miaka ya 1970, nchi ikijitosheleza kwa bidhaa za viwandani.

Hapo zinaorodheshwa vifaa vya ujenzi, redio, umeme, nguo, vyakula, vinywaji, dawa na pembejeo. Mchango wa sekta ya viwanda kwa Pato la Taifa liliongezeka kwa asilimia 400.

Mchango wa sekta ya viwanda ajira ni kwa asilimia mia 500 na uwekezaji hiyo ilipaa sana, huku mauzo ya nje yaliongezeka kwa zaidi, kutoka asilimia 9.9 ya mwaka 1966 hadi asilimia 22.3 katika miaka ya 1980.

Pia, Tanzania ilifanikiwa kupunguza utegemezi wa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje hasa vifaa vya shule, nguo, vyakula, vyombo vya nyumbani, mbolea na maeneo mengine.

Maendeleo katika sekta ya kilimo Mwalimu Nyerere, alihimiza kilimo katika ngazi ya vijiji na mashamba makubwa kupitia sera na maelekezo kama vile Siasa ni Kilimo; Kilimo cha Kufa na Kupona; Kilimo ni Uti wa Mgongo.

Tanzania iliendelea kuwa mzalishaji mkubwa duniani wa mazao kama mkonge, korosho, chai, pareto, tumbaku, kahawa na karafuu na nchi iliwekeza zaidi katika utafiti na vituo vya utafiti wa mbegu bora kama vile: Ukiriguru- Mwanza; Uyole, Mbeya; Ilonga- Kilosa; Maruku Bukoba' na Naliendele iliyoko Masasi.

> **“ Maendeleo katika sekta ya kilimo Mwalimu Nyerere alihimiza kilimo katika ngazi ya vijiji na mashamba makubwa kupitia sera na maelekezo kama vile Siasa ni Kilimo; Kilimo cha Kufa na Kupona; Kilimo ni Uti wa Mgongo.**



Profesa Godius Kahyarara.

Hiyo iliendana na Kuimarishwa kwa Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine, ambacho awali kilikuwa Kitivo cha Kilimo cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Ni mafanikio yaliyokuwa wazi nchi kuwa na akiba zaidi ya fedha za kigeni kuliko matumizi yake ambayo kitalamu inatamkwa 'Positive Trade Balance' na ndio jambo lililopandisha thamani ya fedha za Kitanzania. Inakumbukwa wakati huo, kila Dola moja ya Kitanzania, ilikuwa na thamani ya shilingi tano.

Ndio zama wastani wa miongo minne sasa inatimu mabasi ya daladala yalizaliwa, kwa maana ya kutoza nauli kwa bei ya shilingi tano.

Pia, ndio wakati ambao Paundi za Uingereza zilikuwa na thamani ya Sh. 20. Hata waliodai kama vile Benki ya Dunia na IMF, kwamba shilingi ilipandishwa zaidi thamani kuliko uhalisia. Dai la thamani ya shilingi ya Tanzania ilizidishwa kwa wastani wa asilimia 57.

**MATATIZO UCHUMI**

Kuanzia katikati ya miaka ya 1970 mpaka mwanzoni mwa 1980, kulikuwapo matatizo ya kiuchumi kitaifa, baadhi ya walioko nje ya nchi kunyooshea mkono sera ambazo hazikuwa sahihi.

Hata hivyo, taarifa zilizopo zinasisitiza kuwa matatizo haya hayakutokana na sera za uchumi za serikali ya Mwalimu Nyerere, bali yalitokea wakati akiwa Rais wa nchi. Ni matatizo yanayoorodheshwa katika maeneo kadhaa;

Mosi, kuna suala la kupanda bei ya mafuta kwa asilimia 400 na hatimaye serikali ilijikuta ikitumia asilimia 60 ya fedha za kigeni kuagiza mafuta peke yake.

Pili, ni kuvunjika iliyokuwa Jumuiya ya Afrika (EAC) mwaka 1977, kuliilazimisha Tanzania kuwekeza katika mashirika ya Reli(TRC), Ndege (ATC), Posta na Mawasiliano (TPTC) na Bandari (TPH), ili kuzinusuru huduma hizo.

Tatu, ilikuwa suala la kutokea ukame uliaothiri sehemu kubwa ya nchi, huku soko la mazao la mkonge duniani lilianguka. Awali zao hilo lilikuwa na soko kubwa kuingiza zaidi fedha za kigeni, kufungua biashara na ajira mjini na shambani.

Jambo la nne linatajwa kuwa, mwaka 1978, Tanzania ililazimika kuingia katika vita na Uganda.

Inaelezwa, katika kupambana na matatizo haya makuu manne, ndipo Rais Nyerere alianzisha mchakato wa kuwa na mfumo wa kuzalisha umeme, mradi wa Stiglers Gauge.

Katika hilo, mtikisiko wa bei ya mafuta uliifanya nchi kutumia zaidi ya asilimia 90 ya umeme unaowashwa kwa kutumia mafuta na serikali ikitumia asilimia 60 ya akiba yake fedha za kigeni, kuagiza mafuta.

Ukame huo ulilazimisha uagizaji chakula kutoka nje ya nchi na ni matatizo hayo yanayoweza kudondosha uchumi wowote uwe wa kijamaa kibepari au kikabaila. Ni mitikisiko wa kiuchumi, ambao kitaalamu hakukuwa na uhusiano wowote na sera zilizobuniwa na kusimamiwa.

**NINI CHA KUJIFUNZA?**

- Umuhimu wa kujitegemea ili kuwa na uhuru kiuchumi
- Viwanda ni muhimu kwa maendeleo ya sekta ya kilimo na hatimaye nchi kwa ujumla
- Mkakati wa kuchataka angalau asilimia 85 ya pamba kujitosheleza wenyewe
- Ni vyema serikali ikaendelea kusimamia uchumi ikiwamo viwango vya riba, kulinda thamani ya shilingi na usimamizi wa uzalishaji kuanzia ugani, pembejeo, bei na upatikanaji wa masoko.
- Nchi masikini iendelee kuwa na sauti ya pamoja katika kupigania usawa katika uchumi wa dunia.
- Afrika ina fursa ya kukuza biashara miongoni mwao na kubadilishana uzoefu wa kiuchumi.
- Mashirika ya umma yakisimamiwa vizuri, yana faida zaidi kwani serikali inapata kodi pamoja na gawio tofauti, biashara binafsi ambazo zinatoa kodi peke yake.
- Sera ya ujamaa na kujitegemea bado haijapitwa na wakati na ni tofauti za kimtazamo kwani ujamaa wa kidemokrasia una fursa ya kuamua aina ya mfumo wa uchumi na si kweli mfumo wa kiuchumi ndio inaamua mfumo wa itikadi.

Inaelezwa, bado fedha nyingi zinatengwa kwa ajili ya sekta kuu kama afya na elimu na kuna bodi ya mikopo, bodi ya nafaka, bima ya afya, hifadhi ya jamii, huduma za ugani kwa wakulima, vyote vinategemea ruzuku kubwa ya serikali.

***Kitaaluma, mwandishi wa makala hii bingwa wa uchumi.***

UCHUMI

# Wasomi Tanga wanavyochangamkia ufugaji ng'ombe, wakiipa kisogo ajira

• Mtaaluma wa ugavi autumia kuzalisha, kusambaza maziwa



Wafanyakazi katika mradi wa ufugaji ngombe, wakikamua maziwa mjini Tanga. **PICHA: MOSHI LUSONZO.**

**Na Moshi Lusonzo,** Tanga

UKOSEFU wa ajira ni kati ya mambo yanayowatesa wasomi wengi wa elimu ya juu au mafunzo mbalimbali ya elimu ya kati, ikiwamo ufundi.

Vijana wengi wanaomaliza elimu hiyo, wamekuwa wakihangaika mitaani kusubiri ajira serikalini na katika sekta za umma, ajira ambazo kadri mifumo ya kimaisha inavyobadilika, nazo zinazidi kuwa haba.

Kwa bahati mbaya, wengi hawataki kujiajiri katika shughuli kama kilimo, ufugaji, uvuvi na nyingine za kawaida zinazoaminika kufanywa na wenye elimu ndogo.

Hayo yanatokea, huku walioamua kujiajiri wakiwa na maisha bora kutokana na fedha wanazovuna kwenye shughuli hizo.

Hivi karibuni, wanahabari wanaounda Kituo cha Habari dhidi ya Umasikini (MeCAP), walikuwa mkoani Tanga kushuhudia na kujifunza namna sekta binafsi inavyosaidia katika mapambano dhidi ya umasikini.

Moja ya maeneo ushuhudia wao, ni jinsi vijana waliomaliza elimu ya juu walivyoamua kuachana na ndoto za kuajiriwa na kujikita katika ufugaji ng'ombe wa maziwa.

**USHUHUDA ULIVYO**

Baadhi yao wanasema wameamua kuingia katika ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, kwa sababu ni eneo lenye soko la uhakika na waliotangulia kufanya shughuli hiyo wana ushaidi wa kuondokana na umasikini kwa kiwango kikubwa.

> **"Ukiniuliza mimi juu ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ninaweza nikakupa jibu la uhakika kuwa, sekta ya ufugaji (maziwa) ina fursa nyingi za ajira na kila aliyejaribu kuingia hawezi kutoka.**

Peter Mshanga, ni mhitimu sa chuo kikuu, anayesema baada ya kusaka ajira bila ya mafanikio, aliamua kuingia katika ufugaji.

Mshanga mkazi wa Pongwe, nje kidogo ya Jiji la Tanga, anasema ameamua kufuga ng'ombe wa maziwa, baada ya kupata elimu ya ufugaji kutoka kwa rafiki yake ambaye ni mnufaika mkubwa wa sekta hiyo.

"Kuna rafiki yangu mmoja anaitwa Shayo. Huyu ndiye kaniondoa kwenye ndoto za kuajiriwa na kusema ukweli sasa sina wazo la kuomba kazi tena, kwa sababu ufugaji unamaliza matatizo yangu kwa kiwango kikubwa" anasimulia.

Kijana huyo anaeleza kwamba alianza na ng'ombe mmoja tu wa maziwa, lakini sasa anao watano wanaompatia wastani wa lita 60 za maziwa kwa siku.

Mshanga mwenye taaluma ya ugavi, anasema katika lita hizo 60, anapata wastani wa Sh. 120,000 kila siku, kiasi ambacho ni kikubwa na kinachotosha kuendesha maisha yake bila ya kufikiria kuajiriwa tena.

"Pengine ningeajiriwa mshahara wangu usingefika hata shilingi laki sita kwa mwezi. Lakini sasa nina uhakika wa kuvuna si chini ya shilingi milioni tatu kwa mwezi, ambazo hata nikitoa gharama za chakula cha mifugo, dawa na vitu vingine sikosi akiba ya Sh. milioni mbili" anasema.

Kuhusu soko, anasema yeye na wafugaji wengine wa ng'ombe wa maziwa mkoani Tanga, soko lao kubwa ni kiwanda cha kusindika maziwa cha Tanga Fresh, kilichoko eneo la Kange nje kidogo ya Tanga.

Kwa sasa, kijana huyu ni kati ya wanachama wanaounda ushirika wa Wafugaji Ng'ombe wa Maziwa katika mji wa Tanga, wanaokusanya maziwa na kukiuzia kiwanda hicho kwa utaratibu wa kulipwa mara mbili kwa mwezi.

Mshanga anauzungumzia ufugaji ng'ombe wa maziwa kama mkombozi sahihi wa maisha yake, hivyo hana sababu tena ya kufikiria ajira serikalini au nje ya chombo hicho.

"Ukiniuliza mimi juu ya ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ninaweza nikakupa jibu la uhakika kuwa, sekta ya ufugaji (maziwa) ina fursa nyingi za ajira na kila aliyejaribu kuingia hawezi kutoka," anaeleza Mshanga.

**CHANGAMOTO JE?**

Mshanga anakiri katika ufugaji huo anakutana na changamoto nyingi, ikiwamo kupata maziwa kidogo wakati wa ukame na wakati mwingine dawa wanazouziwa na wamiliki wa maduka ya dawa za mifugo kutokidhi viwango vinavyotakiwa.

"Mimi na wenzangu, kilio chetu kikubwa ni kuiomba serikali kuhakikisha kwamba dawa zinazouzwa kwenye maduka ya dawa za mifugo ni halisi, kwani baadhi ya wenye maduka hayo wanauza dawa ambazo ni hatarishi kwa mifugo yetu" anasema.

**KATIBU JE?**

Katibu wa chama hicho wilayani Muheza, Kudra Tindwa, anasema sekta ya maziwa ni mkombozi kwa wanachama wake waliojiajiri kupitia ufugaji.

Anasema, ushirika wao wenye wanachama 252, umewawezesha kumiliki kituo cha ukusanyaji maziwa na kuyauza katika kiwanda cha kusindika bidhaa za maziwa na wanachama wamekuwa wakijipatia kiasi kikubwa cha mapato.

Kwa mujibu wa katibu huyo, kila siku kuna jumla ya lita 2,600 hadi 3,000 za maziwa hukusanywa na ushirika wao na kila mwanachama ana uhakika wa soko la maziwa anayoyazalisha.

"Kupitia ushirika huu, kila mfugaji ana uhakika wa soko la maziwa anayoyakamua kila siku kupitia, " anasema Tindwa.

Anafafanya kuwa, pamoja na kuwapo uhakika wa soko, pia ushirika una dhamana kubwa kwa wanachama wafugaji pindi wanapokopa katika taasisi za kifedha, akisifu kipato kinachotokana na uuzaji maziwa, kinawapa uwezo wa kurejesha mikopo kutoka tasassi za fedha.

**MKAZI MUHEZA**

Dk. John Tesha, mkazi wa Muheza mkoani Tanga, ni mwanachama wa ushirika huo, anaeyeungana kukiri ufugaji umekuwa mkombozi sahihi kwa wanaotaka kujiajiri.

Anaeleza: "Awali tulikuwa hatuna uhakika wa soko na wapi unakwenda kuuza maziwa, lakini ushirika umetuwezesha kupata soko ambako ni Tanga Fresh, ninajikuta ninafuga kwa malengo na kipato ninachokipata kinaniwesha kujikimu kimaisha."

Lingine analolitaja kama faida, ni uhakika wa soko la maziwa yao, pia elimu ambayo ushirika kwa kushirikiana na kiwanda cha maziwa, wanaandaa semina ya kuwaongezea uelewa wa ufugaji bora na wenye manufaa, kuwaengua kutoka ufugaji wa mazoea.

**MENEJA MKUU**

Meneja Mkuu wa Kiwanda cha Tanga Fresh, Michael Karata, naye anajiunga katika orodha ya wanaokiri kwamba sekta ya maziwa inapunguza tatizo la ajira nchini, pia wafugaji wanaweza kuajiri vijana wanaomaliza shule kama za msingi na sekondari, hata vyuo.

"Kama tukiamua kufuga kwa utaratibu wa kisasa na malengo, sekta hii ina nafasi kubwa ya kuwaajiri vijana wengi walioshindwa kujiendeleza kimasomo, kwa sababu ufugaji wa kisasa unahitaji watu wengi wa kutoa huduma kwa wanyama hawa," anasema.

"Kuna vijana wanaoweza wakatumika kama wahudumiaji wa ng'ombe, kuanzia wachungaji, wakata majani, wakamuaji na hata wanaokwenda kuuza maziwa kupitia vyama vya ushirika vya wafugaji" anasema Karata.

Ombi lake kwa serikali ni kuitazama uzalishaji maziwa na kuirasimisha kwa kujengea uwezo wa masoko ya uhakika, sambamba na idadi kubwa ya wataalamu wa mifugo, ili wafugaji wawe na mifugo bora.



Mafundi wakiendelea na ujenzi wa moja ya madaraja katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, mkoani Mbeya jana, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya serikali kuimarisha miundombinu ya barabara. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mtendaji ahama, atishiwa kuuawa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

OFISA Mtendaji wa Kata ya Izira katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Ildephonce Kamugisha, amekikimbia kituo cha kazi baada ya kutishiwa kuuawa.

Kiongozi huyo alitimkia Mbeya Mjini, baada ya wanakijiji cha Mapita alikokuwa akifanyakazi kutishia kumuua.

Ilidaiwa kuwa kiongozi huyo aliondoka tangu Agosti mwaka huu baada ya wananchi hao kumtishia yeye pamoja na mmoja wa wanamgambo wa kata kuwa watawaua, hata hivyo kuondoka kwake kumesababisha wananchi kukosa huduma. Kuondoka kwa Kamugisha kulibainika juzi wakati Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Mbeya ilipofanya ziara ya kusikiliza kero za wananchi wa Kata ya Izira.

Baada ya malalamiko ya wananchi hao Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika alimtaka ofisa huyo, kutoa maelezo juu ya tuhuma hizo naye alieleza kuwa Agosti 8, mwaka huu mwananchi mmoja alijiua katika Kijiji cha Mpita kwa kujinyonga hali iliyosababisha wananchi hao kumlazimisha yeye pamoja na mgambo wa kata wamzike kwa madai kuwa ndiyo waliosababisha mtu huyo kujiua.

Alisema wananchi hao walidai kuwa mwanakijiji huyo aliamua kujinyonga kutokana na kufuatiliwa na mgambo kwa makosa aliyokuwa nayo hivyo wakawa wanataka kumshambulia askari huyo.

Alisema wakati wananchi hao wakitaka kumshambulia mgambo yeye aliingilia kati kuwatuliza ili kumwokoa ndipo wananchi hao wakamuunganisha naye kwenye tukio hilo.

"Walisema kwa sababu mtu huo amejinyonga basi na sisi tutatutafuta ili watunyonge, baada ya kusikia hivyo mimi niliamua kuondoka na kwenda Mbeya Mjini, nikiwa huko nilipata taarifa kuwa baadhi ya watu wanawahamasisha wananchi kuwa nikionekana tu nifanyiwe kitu ambacho nisingeweza kukisahau maishani mwangu," alisema Kamugisha.

Alieleza kuwa awali baada ya kutokea vurugu za mazishi ya mwananchi aliyejinyonga walipiga simu kituo cha Polisi Mbalizi kwa ajili ya kuomba msaada na polisi walifika wakasaidia kutuliza hali hiyo.

Baada ya maelezo hayo, Mkuu wa Wilaya, Ntinika aliliagiza Jeshi la Polisi kuwakamata wananchi wawili ambao ni Tumaini Mwazembe na Felix Mwazembe waliokuwa vinara wa kumtishia maisha Kamugisha.

Aliagiza kuwa mpaka kufikia jana jioni watu hao wawe wamekamatwa na kuwekwa rumande wakati wakisubiri hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

Aidha, aliagiza Ofisa Mtendaji huyo kurejea katika kata hiyo na kuendelea na kazi huku akiwataka wananchi wampe ulinzi asije akadhurika wakati serikali ikiendelea na taratibu zingine.

# Aamuru wachimbaji kufukia mashimo

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WACHIMBA dhahabu wilayani Chunya, wameagizwa kufukia mashimo mara moja, baada ya kumaliza kazi, ili kuepusha maafa ambayo ni pamoja na vifo baada ya watu kutumbukia.

Agizo hilo lilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya Chunya, Maryprisca Mahundi, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Maafa Duniani ambayo yalifanyika katika Kata ya Matundasi ambayo ni miongoni mwa kata zenye migodi mingi.

Alisema kuwa kwa mujibu wa sheria za madini ni kosa kwa mchimbaji kuacha shimo likiwa wazi baada ya kulitumia, lakini wachimbaji wengi wanapuuza sheria hiyo na hivyo kuhatarisha maisha.

Mahundi alisema watu wengi wamepoteza maisha hasa kipindi cha mvua kwa kutumbukia kwenye mashimo hayo ambayo hujaa maji.

"Hatutafurahi hata kidogo kuja mara kwa mara na kamati ya maafa kuopoa miili ya watu kwenye mashimo haya, sasa naomba tusaidiane kusimamia hili kwa kuhimizana kufukia mashimo baada ya kuyatumia maana vinginevyo tutaendelea kushuhudia maafa hayo," aliagiza Mahundi.

Aliagiza Ofisi ya Ofisa Madini wa Wilaya kushirikiana na viongozi wa kata na vijiji kutoa elimu kwa wachimbaji ili kuhakikisha mashimo yote yaliyotumika yanafukiwa mapema kabla mvua hazijaanza.

Alisema ikiwezekana wachimbaji wote watakaobainika wakiwa wametelekeza mashimo, wachukuliwe hatua za kisheria ikiwamo kutozwa faini ambazo zitakuwa fundisho kwa wengine.

Ofisa Madini Mkazi wa Wilaya ya Chunya, Gudson Kamhanda, alisema wilaya hiyo imekuwa ikikumbwa na maafa ya mara kwa mara katika maeneo ya migodi kutokana na wachimbaji kufukiwa na vifusi ama kuporomokewa na mawe.

Alisema tangu mwezi Agosti mwaka 2018 mpaka wiki hii Oktoba 15, wachimbaji 21 wamepoteza maisha kutokana na ajali hizo ambazo nyingi huwa zinatokea kutokana na wachimbaji kutochukua tahadhari.

Alisema ili kuepuka watu kupoteza maisha wananchi wanatakiwa kupatiwa elimu ya usalama kwenye maeneo ya migodi pamoja na njia za kuokoa endapo inatokea ajali kama hiyo.

"Kuna ajali za aina nyingi ambazo huwa zinatokea maeneo ya migodi ambazo ni pamoja na ajali za moto, watu kufukiwa na wengine kuporomokewa na mawe lakini kwa huku kwetu ajali za moto ni mara chache sana kwahiyo tutaendelea kushirikiana na wananchi kukabiliana na matukio haya," alisema Kamhanda.

Aidha, alisema wataendelea kutoa elimu kwenye maeneo ya machimbo yote ili wachimbaji waendelee kufukia mashimo wanayokuwa wanayatumia.

Baadhi ya wachimbaji waliviomba vyombo vya usalama kuitikia haraka kwenda kufanya uokoaji wanapopewa taarifa za ajali ili kuepusha vifo vya watu ambavyo sio

# Rungwe yaonywa mimba za utotoni

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

WAZAZI na walezi katika Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe mkoani Mbeya, wametakiwa kushirikiana na serikali katika vita dhidi ya mimba za utotoni.

Wilaya ya Rungwe inaelezwa kuwa ndiyo inayoongoza kwa mimba hizo zinazosababisha mabinti wengi kutofikia malengo yao.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Shule za God's Bridge, Athony Mwantona, wakati wa mahafali ya kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mpuguso iliyoko wilayani Rungwe yaliyoambatana na harambee kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule hiyo.

Alisema viongozi wa wilaya hawawezi kutatua tatizo hilo bila wazazi na walezi kuungana pamoja kuwalinda watoto hao akisema kuwa mara nyingi wanafunzi wanashiriki vitendo hivyo wakiwa nyumbani na sio shuleni.

Mwantona alisema kuna baadhi ya wazazi wamekuwa wavivu kufuatilia mienendo ya watoto wao na kuwaacha huru hali inayochangia kwa kiasi kikubwa watoto hao kufanya mambo ya ovyo.

"Wilaya yetu imepanda kielimu kwa miaka mitatu, lakini katika suala la mimba za utotoni sisi wana Rungwe tunaongoza kwa mkoa wa Mbeya jambo ambalo ni la aibu na linatuchafua hivyo naomba tushirikiane wote kupambana nalo," alisema Mwantona.

Kaimu Ofisa Elimu Wilaya ya Rungwe, Aucklend Hyera, aliwataka wazazi na walezi kuepuka kuwa kikwazo cha maendeleo ya elimu katika wilaya hiyo, huku akisema kuwa kuna tabia ya baadhi ya wazazi kutotoa taarifa za watoto wao wanapopata mimba.

Alisema wilaya hiyo imejipanga kupandisha ufaulu wa wanafunzi kwa kupata alama A, B na C hivyo ili kufikia lengo hilo lazima kuwepo umoja kati ya wazazi, serikali na wadau mbalimbali wa elimu.



# Fidia yabaini makaburi feki

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MGOGORO wa kuhamisha makaburi katika eneo la Chinyoya mkoani Dodoma, umetatuliwa na kubainika kuwa kati ya makaburi 79 yaliyofukuliwa manne yalikuwa hewa.

Awali, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma ,Patrobas Katambi, alisitisha uhamishaji huo ili kupisha ujenzi wa reli ya kisasa(SGR), baada ya kubaini kuna ndugu feki wa marehemu.

Kufuatia usitishaji huo, Katambi alilazimika kufanya kikao na ndugu wenye makaburi hayo ili kuwabaini wahusika na kufanikisha uhamishaji huo.

Akizungumza na Nipashe jana baada ya mgogoro huo kutatuliwa, Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Chinyoya, Faustina Bendera, alisema kazi hiyo ilikamilika juzi na makaburi 75 pekee ndiyo yalikuwa na mabaki ya miili na manne yakiwa hewa.

Alisema katika kikao hicho walibaini chanzo cha migogoro iliyokwamisha kuyahamisha hapo awali kuwa ni familia za marehemu kutoelewana kuhusu nani apokee fidia.

"Katika uhakiki walisimama watoto wa miongoni mwa wanafamilia, lakini wengine walipoona makaburi yanahamishwa na kulipwa fidia ndio wakajitokeza baada ya kubaini wahusika ndipo kazi ikiaanza kufanyika,"alisema Katambi.

Aidha, aliongeza kuwa katika idadi ya makaburi 79 yanayopitiwa na SGR, kati ya manne yaliyokuwa hewa moja likuwa na jiwe kubwa ndani.

"Malipo ya fidia kwa mujibu wa Shirika la Reli ilikuwa yatalipwa baada ya makaburi kufukuliwa, sasa haya manne ndugu walipoona ufukuaji umeanza walitokomea kutokana na udanganyifu wao,"alisema Mkuu wa Wilaya. Alieleza kuwa gharama za kuhamisha makaburi pamoja na kujengea zimelipwa shirika hilo ambapo fidia kwa kila kaburi ni Shilingi 200,000.

Oktoba 11, mwaka huu, Katambi alisitisha la uhamishaji baada ya kupokea malalamiko ya baadhi ya ndugu wa marehemu waliozikwa katika eneo hilo na kuagiza kusimamisha uhamishaji huo hadi kikao cha pamoja alichoagiza kifanyike ili kujiridhisha kabla ya kuhamisha.

Alisema alipata malalamiko ya baadhi ya ndugu na familia za watu waliozikwa hapo kwa kudai kuwa hawakuwepo wakati wa kuhakiki.

Mmoja wa ndugu, Mary Ndahani, aliishukuru serikali kwa kuingilia kati ili kila familia inayohusika na watu waliozikwa hapo watendewe haki.

"Ni kweli tumetoka mbali kwa ajili ya kuja kuhamisha makaburi ya wapendwa wetu lakini kutokana na kuwepo kwa malalamiko haya na sisi tumeyasikia ,tunaomba tuwe wavumilivu ili kazi ikamilike bila malalamiko "alisema Ndahani.



Baadhi ya viongozi wa kisiasa na dini wa Mkoa wa Dodoma, wakishiriki mkutano na Uongozi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), jijini humo jana, uliojadili kuhusu uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa mkoa huo, linalotarajiwa kuanza mwisho wa mwezi huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Watoto 550,000 kuchanjwa Dodoma

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WATOTO 550,388 kutoka wilaya mbalimbali za mkoa wa Dodoma wanatarajia kuchanjwa polio, surua na rubella ili kuwalinda na magonjwa yanayosababisha vifo na ulemavu kwa watoto.

Akizungumza na waandishi wa habari jana Mkuu wa mkoa wa Dodoma Dk.Binilith Mahenge, alisema chanjo hizo zinatolewa kwa njia ya sindano na hazina madhara kwa mtoto bali zinamlinda dhidi ya magonjwa ambayo yanasababisha ulemavu na vifo.

Alifafanua kuwa watoto 182,039 watapewa chanjo ya polio wakati 368,352 watapewa chanjo ya surua na rubella.

Alisema uzinduzi wa kampeni ya chanjo utafanyika wilaya ya Bahi mkoani humo na ni kwa ajili ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

"Chanjo itatolewa kwa siku tano. Hizi ni jitihada za serikali za kutokomeza vifo vya watoto hivyo wanakingwa wasipate magonjwa ,"alisema.

Alifafanua kuwa mapambano dhidi ya ugonjwa wa surua na rubella yanaendelea kwa kuwa magonjwa hayo yanaendelea kusababisha ulemavu, upofu na vifo kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

"Naomba nitoe wito kwa wana Dodoma kutumia nafasi hii kuwapeleka watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwenye vituo vya huduma za afya ili wakapatiwe chanjo hiyo," alisema Dk.Mahenge.

# NEC: Wengi mno wamepoteza kadi

**Ibrahim Joseph na Renatha Msungu,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa idadi kubwa ya wapiga kura kupoteza kadi ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazoikabili Tume ya Taifa ya uchaguzi (NEC) wakati wa kuboresha daftari la kudumu la wapiga kura unaoendelea nchini.

Kufuatia hali hiyo, NEC imewataka wananchi kutunza kadi na wale waliopoteza kadi wahakikishe wanakumbuka taarifa zao kwa usahihi ili kuepuka usumbufu utakaojitokeza.

Hayo yalibainishwa juzi na Mwenyekiti wa NEC, Jaji Semistocles Kaijage, wakati alipozungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano wa tume na wadau wa uchaguzi mkoani Dodoma.

Jaji Kaijage alisema licha ya kuwepo mafanikio kwenye kuboresha daftari hilo, kuna changamoto mbalimbali ambazo zilijitokeza ikiwemo wapiga kura kutokuwa na uhakika wa kukumbuka majina yao wanapokwenda kurekebisha taarifa zao na upotevu wa kadi hizo.

"Kutokuwa na uhakika wa majina yao kunasababisha kuchukua muda mrefu kituoni kutafuta majina yao kwa usahihi, pia changamoto nyingine ni kuwa na idadi kubwa ya wapiga kura waliopoteza kadi ,"alisema.

Kadhalika, aliwataka viongozi wa vyama vya siasa kuzingatia kanuni na sheria kwa katika uboreshaji wa daftari hilo la kupiga kura kwa kufuata utaratibu wa kutoa malalamiko yao na kuacha kulalamika kwenye vyombo vya habari.

"Ninaomba vyama vya siasa kuzingatia kanuni za uboreshaji wa daftari la kudumu la wapiga kura na maelekezo kwa vyama vya siasa kuhusu uboreshaji, nitoe rai kwa wadau wa uchaguzi pia kutoa taarifa zilizo sahihi, kwa wakati na kwa utaratibu mliojiwekea ili katika awamu hii ya kwanza ya uboreshaji kila mwananchi mwenye sifa ya kuandikishwa asajiliwe."

Vile vile, wanaohitaji kuboresha taarifa zao na wafanye hivyo, aliongeza. Mwenyekiti huyo alisema uboreshaji kwasasa unatarajiwa kufanyika mkoa wa Dodoma na utadumu kwa siku saba kuanzia Oktoba 26, mwaka huu.

Alieleza kuwa uzinduzi rasmi ulifanyika Julai 18 mwaka huu huko mkoani Kilimanjaro na baada hapo zoezi hilo limeendelea katika mikoa mbalimbali nchini kwa mujibu wa ratiba ya tume.

Alitaja mikoa mingine kuwa ni Arusha, Manyara,Simiyu,Mara,Mwanza,Geita,Shinyanga,Kagera, na Kigoma na kuongeza kuwa kazi itaendelea katika mikoa ya Tabora,Katavi na Rukwa .

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Tume hiyo Dk.John Charles, alisema uboreshaji wa daftari hilo utawahusu wapiga kura wapya ambao wametimiza miaka 18 na ambao watatimiza umri huo ifikapo uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 . Dokta Charles alisema pia itawahusisha wale waliohama kutoka maeneo yao ya wali ya kupigia kura , ambao kadi zao za kupigia kura ziliharibika na kupotea pamoja na wale waliofutwa kwa kupoteza sifa na waliofariki.

Aidha, Dk.Charles alisema uhakiki huo pia ulilenga kuangalia vituo vya kupigia kura ambapo katika Mkoa wa Dodoma vituo vimeongezeka kutoka vituo 2,606 mwaka 2015 hadi kufikia vituo 2,686 mwaka 2018.

Kwa upande wa Tanzania Bara vituo vya kupigia kura vimeongezeka kutoka vituo 36,549 mwaka 2015 hadi kufikia 37,407 mwaka 2018 na Zanzibar mwaka 2015 ilikuwa na vituo 380 mwaka 2018 vimefika vituo 407.





# Wanawake wafundwa kuhusu umiliki ardhi

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WANAWAKE wanaomiliki ardhi katika mkoa wa Kaskazini Unguja, wametakiwa kufanya utaratibu wa kutafuta hatimiliki ili kuepusha kupoteza mali zao pale inapotokezea migogoro ya ndoa baina yao na waume zao.

Mwanamtandao wa kupinga vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia Wilaya ya Kaskazini 'B', Akama Ali Mzee, alisema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari huko Donge, Kaskazini Unguja.

Alisema kumejitokeza udhalilishaji wanaofanyiwa wanawake kwa kunyang'anywa ardhi na waume zao na kujimilikisha, hivyo kusababisha migogoro pindi ndoa zinapovunjika.

Akama alisema umejitokeza mtindo wa baadhi ya wanaume kujimilikisha ardhi kwa madai ya kuwa ni haki za wake zao na hatimaye kusababisha migongano pale ndoa zinapovunjika. Hivyo kufanya wanawake walioachika kukosa haki zao.

Vitendo hivyo, alisema vinaendeleza unyanyasaji kwa wanawake na kusababisha kukosa haki zao za msingi.

Mwanamtandao huyo aliwataka wanawake kuhakikisha wanafuata sheria za umiliki wa ardhi ikiwamo kupata hatimiliki zao ili kuepusha kuporwa maeneo yao.

Naye Fatma Ali Makame, aliyemiliki ardhi na kupata changamoto ya kuchukuliwa eneo lake baada ya ndoa kuvunjika, alisema walipeana ardhi na aliyekuwa mumewe kwa makubaliano ya umiliki kwa kuwa walikuwa kwenye ndoa lakini baada ya kuvunjika, mtalaka wake alichukua eneo hilo na kukosa haki yake.

Aliwasihi wanawake wenzake kuhakikisha wanapomiliki ardhi, wahakikishe wanapata stakbadhi za umiliki ili ndoa inapovunjika, wapate haki zao.

# Wanaume vinara makosa barabarani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

OFISI ya Takwimu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Zanzibar imeripoti makosa 1,853 ya usalama barabarani kwa kipindi cha Septemba, mwaka huu, mengi yakionekana kufanywa na wanaume.

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu kwa kushirikiana na kitengo cha takwimu za makosa ya jinai, madai na jinsia, kati ya ajali 27 zilizoripotiwa, waathirika walikuwa 58, kati yao wanaume wakiwa 45 na wanawake 13.

Aidha, ripoti hiyo iliyowasilishwa juzi ilisema waliofariki dunia walikuwa 17 na 41 walijeruhiwa.

Mtakwimu kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu, Asha Mussa Mahfoudh, alisema kwa mujibu wa ripoti hiyo, Wilaya ya Mjini ndiyo iliyoripotiwa kuwa na ajali nyingi ikilinganishwa na wilaya zingine za Zanzibar.

Alisema katika Wilaya ya Mjini pekee, makosa manane yaliripotiwa na kufuatiwa na Wilaya za Magharibi A, Wete na Chakechake zikiwa na ajali nne kwa kila moja.

Wilaya ya Wete, alisema iliripotiwa kuwa na idadi kubwa ya walioathirika wa ajali 17 sawa na asilimia 29.3 zaidi ya robo ya waathirika wote.

Naye Mkuu wa Kitengo cha Takwimu za Kihalifu Makao Makuu ya Polisi Zanzibar, Inspekta Msaidizi Khamisi Mwinyi Bakar, alisema wanajitahidi kupambana na ajali za barabarani ili kuhakikisha zinapungua kwa kiasi kikubwa hususani katika maeneo yanayoripotiwa kukithiri kwa matukio hayo.

Alisema baadhi ya wananchi wa Zanzibar, bado wanaonekana hawajawa tayari kwa hiari kutii sheria za barabarani ndiyo maana ajali nyingi zinaongezeka na hata kusababisha ulemavu wa kudumu na vifo.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Isdor Mpango (katikati), akiwa na ujumbe wa Tanzania wakifuatilia majadiliano kwenye Mkutano ya mwaka ya Benki ya Dunia na Shirika la Fedha la Kimataifa, jijini Washington, nchini Marekani juzi. **PICHA: WFM**

# RC awapa mbinu kidato cha nne

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

MKUU wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, amewataka wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mitihani ya kidato cha nne mwaka huu kutumia muda uliosalia kujisomea ili kupata matokeo mazuri.

Ayoub alitoa wito huo juzi alipokutana na wanafunzi hao, walimu, wawakilishi wa wazazi na watendaji wa ngazi mbalimbali wa mkoa huo kwenye ukumbi wa Dk. Ali Mohamed Shein wa Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (Suza), kilichoko Tunguu mkoani humo.

Kwa mujibu wa Ayoub, iwapo watatumia kikamilifu muda huo na kuachana na vitendo vinavyokwenda kinyume cha masuala ya elimu, wanaweza kupata matokeo mazuri na kuendelea na elimu ya juu.

Alisema ili kufaulu mitihani hiyo, juhudi za pamoja zinapaswa kufanywa na wadau wote wakiwamo wazazi ili kuwa na maendeleo endelevu katika jamii.

Kwa miaka minne mfululizo, alisema mkoa huo umekuwa na idadi ndogo ya wanafunzi wanaofaulu kwa daraja la kwanza, jambo linalopaswa kubadilishwa kutokana na uwezo unaoonyeshwa na wanafunzi wanapokuwa katika mikoa mingine.

"Katika kipindi hiki ni lazima sote tuungane kuwasaidia vijana wetu ili kukabiliana na changamoto za mitihani hii na kubadili hali ya matokeo ya mitihani. Hivi walimu wakuu ambao kwa muda wote huo hamjawahi kutoa hata mtoto mmoja aliyefaulu kwa daraja la kwanza mmewahi kujiuliza au kujitathmini?" Alihoji mkuu huyo wa mkoa.

Ili kuhamasisha ufaulu wa mitihani hiyo, mkuu huyo wa mkoa aliwaahidi kuwapatia zawadi ya 'tablet' na seti ya vifaa na sare za shule wanafunzi wote watakaofaulu kwa daraja la kwanza sambamba na kutoa Sh. milioni 5 kwa walimu watakaofaulisha kwa daraja hilo.

Nao wanafunzi wanaotarajiwa kufanya mitihani ya kidato cha nne, waliushukuru uongozi wa mkoa huo kwa hamasa kubwa ulioionyesha kwa kuahidi zawadi mbalimbali pamoja na kudhamini kambi za wanafunzi kwa ajili ya maandalizi ya mitihani.

Katika hatua nyingine, Ayoub aliwataka wazazi ambao wamepokea mahari ya watoto wao kuirudisha na kutowaozesha watoto wao hadi yatakapotoka matokeo ya mitihani inayotarajiwa kufanyika mwezi ujao.

"Tuna taarifa kuwa baadhi ya wazazi wameshapokea mahari ya watoto wao ambao ni miongoni mwa watahiniwa. Niwaombe warudishe mahari au wasitishe mipango ya ndoa hadi matokeo yatakapotoka," alisema Ayoub.

Katika mkutano huo ulihudhuriwa na watahiniwa wa skuli zote 32 za sekondari za serikali na binafsi mkoani humo, Katibu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Kusini Unguja, Suleiman Mzee Suleiman 'Charas', alipongeza juhudi zinazochukuliwa na serikali ya mkoa kuimarisha sekta ya elimu.

Nao wakuu wa wilaya za Kati na Kusini, Hamida Mussa Khamis na Idrissa Kitwana Mustafa, waliahidi kushirikiana na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya mkoa kuimarisha elimu mkoani humo.

# Sekta binafsi: Matamko ya serikali kikwazo uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU wa sekta binafsi nchini wamesema Mpango wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili ASDP II bado kunachangamoto nyingi za ufanyaji biashara ikiwamo matamko yanayozui usafirishaji wa mazao nje ya nchi.

Wakizungumza wakati wa warsha ya kujadili ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa ASDP II iliyoandaliwa na Baraza la Kilimo Tanzania na kufanyika mkoani Morogoro, walisema ni muhimu mpango huo ukawa jumuishi si tu kwenye makaratasi, bali iwe jumuishi kwenye utendaji, maamuzi ya kila siku ya kisera ili sekta binafsi iweze kushiriki vema zaidi katika mpango huo.

"Tumekuwa tukiathiriwa sana na matamko mengi hasa ya ufungaji wa mipaka, mfano SUMRI alikuwa na tani 5,000 za mahindi ghafla likatoka tamko la kuzui kuuza nje, unaweza kuona namna tamko la mtu mmoja linavyoathiri sana, unakuta mtu mmoja anatoa tamko ambalo athari yake ni kubwa sana kiuchumi kwa mtu mmoja na jamii nzima," alisema Joseph Massimba kutoka kampuni ya SUGECO.

"Tamko la kutokutoa mazao wilaya moja hadi nyingine, sasa unaona ambavyo mazingira yanavyoiathiri sekta binafsi kwa hiyo ni muhimu changamoto hizi zikafanyiwa kazi vizuri na serikali ili tuweze kushiriki vizuri katika ASDP II," alisema.

"Kimsingi changamoto ni nyingi hasa haya mazuio ya usafirishaji wa mazao nje ya nchi yanaathiri sana, sisi tunategemea masoko ya nje sasa unapozuiwa unajikuta unabaki na mzigo mkubwa sana ambao soko la ndani haliwezi kuumudu mzigo ulipo, lakini pia ni muhimu tuwe tunashirikishwa kama sekta binafsi," alisema Sifa Gerana, msindikaji wa bidhaa za mchele na mahindi.

Mtafiti Mshauri aliyefanya utafiti kuhusu changamoto zinaikabili sekta binafsi kushindwa kushiriki kikamilifu katika ASDP II, Apromius Mbilinyi, alisema ni wakati mwafaka kwa sekta binafsi kuanza kuwekeza katika sekta ya kilimo kwani kuna fursa nyingi hasa katika uongezaji wa thamani.

"Asilimia 70 ya mbegu zinaagizwa nchi ya nje, hii ni fursa kwa sekta binafsi kuwekeza lakini lazima wajitokeze kuwekeza katika ujenzi wa maghala ya kuhifadhia chakula kwa sababu asilimia 30 ya mazao nchini yanaharibika baada ya kuvunwa kwa hivyo ni muhimu sekta binafsi ikazitazama fursa hizi," alisema.

Alisema kuwa sekta binafsi kwa sasa inachangia asilimia 65 ya ajira na kwamba kupitia ASDF II ajira nyingi zaidi zinaweza kupatikana hasa katika uongezaji wa thamani wa bidhaa za mazao.

Ofisa Sera Mwandamizi kutoka Baraza la Kilimo Tanzania, Laetitia Wiliam, alisema waliamua kufanya utafiti huo baada ya kuona wadau wengi wa sekta binafsi wakiwa na ukakasi katika kushiriki katika utekelezaji wa mpango huo, ambapo sekta binafsi inatarajiwa kutoa asilimia 59 huku serikali ikitoa asilimia 41 katika kukamilisha mpango huo.

Mchumi kilimo dawati la ASDP II kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Militon Manyara, licha ya kukiri uwapo wa changamoto kadhaa za kiutekelezaji wa ASDP II na kwamba serikali bado inaendelea kuzifanyia ili kukifanya kilimo kiwe na tija.

"Zaidi ya asilimia 78 ya tozo ambazo wadau wamekuwa wakizilalamikia tayari serikali imekwisha kuzifanyia kazi na kupitia Blue Print tunaamini changamoto nyingi zinazoelezwa hapa zitafanyiwa kazi kikamilifu," alisema Militon.

"Serikali inaendelea kuzifanyia kazi changamoto zote inapitia sera na taratibu na kanuni ili kukifanya kilimo kiwe chenye tija na iweze kumsaidia mkulima aweze kunufaika na sekta ya kilimo," alisema.



Mchuuzi wa matikiti maji akiyapanga wakati akisubiri wateja katika soko la Msasani, jijini Dar es Salaam jana. Tikiti moja liliuzwa kwa bei ya 2,000/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Sumukuvu yatishia chakula

**Na Mathias Canal**

SERIKALI imesema uwapo wa sumukuvu kunahatarisha usalama wa chakula hususan mazao ya mahindi na karanga, ambayo huchangia upatikanaji wa lishe bora.

Mbali na kuchangia lishe, mahindi na karanga ni chakula muhimu kwa Watanzania wengi.

Taarifa zinaonyesha kuwa tatizo la sumukuvu ni kubwa kwani inakadiriwa kuwa asilimia 25 ya mazao yote yanayozalishwa duniani yanaathiriwa na sumukuvu. sumukuvu ina athari kubwa za kiafya na huchangia karibu asilimia 30 ya saratani ya ini, kuharibu mfumo wa kinga na kupelekea udumavu kwa watoto.

Waziri wa Kilimo, Japhet Hasunga, ndiye aliyebainisha hayo juzi wakati akifunga Maadhimisho ya Siku ya Chakula Duniani mwaka 2019 ambayo kitaifa yalifanyika mkoani Singida.

Alisema athari hizo haziishii tu kwa binadamu, bali hata mifugo nayo huathiriwa na tatizo hili, hivyo kusababisha mtu kula sumu hizo kupitia mazao ya wanyama kama maziwa, mayai, samaki na nyama kutoka kwa wanyama waliolishwa vyakula vyenye sumukuvu kwa kiwango kikubwa.

Hasunga alisema mazao hayo pia yana umuhimu mkubwa katika kupata lishe bora, hivyo alitoa mwito kwa wafugaji nchini kuchukua tahadhari dhidi ya sumukuvu katika sekta ya mifugo.

# Utafiti wafichua sababu umaskini Bunda, Busega

**Na Ahmed Makongo,** BUNDA

UTAFITI uliofanywa na watafiti wakiwamo wa Chuo cha Mipango na Maendeleo Dodoma tawi la Mwanza, umebaini Wilaya ya Busega mkoani Simiyu na Wilaya ya Bunda mkoani Mara, wakazi wake wanakabiliwa na changamoto ya umaskini unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi na hali ya hewa.

Utafiti huo uliofadhiliwa na Shirika la Mpango wa Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) na kufanyika katika vijiji mbalimbali vya wilaya hizo, umebaini kuwapo kwa hali hiyo ya umaskini, ikiwamo na baadhi ya kaya kutokula milo mitatu.

Profesa Innocent Zilihona kutoka Chuo cha Mipango Dodoma tawi la Mwanza na Joshua Mirumbe, waliyasema hayo jana kwenye kikao cha mrejesho wa utafiti huo mjini Bunda.

"Tulifanya utafiti katika Wilaya ya Busega iliyoko katika Mkoa wa Simiyu na katika halmashauri mbili za Wilaya ya Bunda, mkoani Mara na kubaini kuna umaskini, ambapo moja wapo ni baadhi ya kaya kutokuwa na chakula na nyingine kutokula milo mitatu na hata kama wanapata, lakini siyo kwa kiwango kinachotakiwa," aliasema Prof. Zilihona. "Tulisaidiana na watu wa mipango tukaandika andiko hilo la mradi huo na kisha tukafanya utafiti huo na kubaini changamoto mbalimbali za umaskini kwa baadhi ya kaya katika wilaya hizo," alisema Mirumbe.

Kikao hicho kilishirikisha wadau wakiwamo viongozi wa serikali na wananchi wa wilaya hizo, na walichangia maoni yao ya nini kifanyike ili kuondokana na hali hiyo, huku baadhi wakilalamikia wanyamapori hasa tembo wanaotoka katika Hifadhi ya Serengeti kushambulia mazao yao, hivyo kuwasababishia umaskini.

"Wananchi wetu wamekuwa wakitegemea chakula kinachotokana na zao la muhogo, lakini sasa zao hilo limeingiliwa na ugonjwa... sasa hapa cha kufanya ni serikali kutafuta mbegu mbadala wa zao hilo ambayo haishambuliwi na ugonjwa," alisema Sabato Mafwimbo, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.

Mratibu wa mradi huo, Bonamax Mbasa, alisema mradi huo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na mazingira, utafiti wake ulifanyika kuanzia Juni hadi Agosti mwaka huu katika wilaya hizo.

Mratibu wa miradi ya UNDP nchni, Amon Manyama, alisema utafiti huo utaendelea, na kwamba watatekeleza mambo yote yatakayopendekezwa na wadau hao.

HABARI KIMATAIFA

# Kim Jong-un apanda mlima mtakatifu

**P'YONGYANG,** Korea Kaskazini

RAIS wa Korea Kaskazini, Kim Jong-un amepanda mlima mrefu kuliko yote nchini humo uitwao Paektu kwa kutumia farasi.

Hii si mara ya kwanza kwa kiongozi huyo kufanya hivyo kwani alishawahi kupanda kilele urefu wa mita 2,750 huku dhumuni likiwa ni kufanya matangazo muhimu.

Mlima huo ni mahali ambapo baba wa kiongozi huyo wa Korea Kaskazini alizaliwa huku pia ni kati ya vivutio vya nchi hiyo.

**Kitendo cha kiongozi huyo kupanda mlima wa Paektu ni kitendo kikubwa cha kihistoria.**

Kitendo cha kiongozi huyo kupanda mlima wa Paektu ni kitendo kikubwa cha kihistoria.

Kiongozi huyo ametafakari hatua iyo ya kupanda mlima Paektu kama kuongoza nchi hiyo huku akisema inahitaji kuwa imara kama mlima huo.

Mara ya mwisho Kim Jong-un kupanda mlima Paektu kumeleta matokeo makubwa na mipango mikubwa iliyofanywa na kiongozi huyo juu ya nchi hiyo. Inasemekana kuwa kiongozi huyo safari hii, anaweza kubadilisha mawazo yake juu ya majaribio ya makombora ya masafa marefu pamoja na silaha za nyuklia.

Inawezekana Kiongozi huyo wa Korea Kaskazini alipanda mlima huo kama mbinu ya kuelekea kukubaliana na mawazo ya uongozi wa Rais Trump.

Marekani imetakiwa kuja na suluhisho juu ya kusitisha mpango mzima wa nyuklia Korea Kaskazini, mpaka kufikia mwishoni mwa mwaka katika Mji mkuu wa korea kaskazini.

Kim amekuwa akikumbana na vikwazo mbele yake kabla hajatatua mgogoro huo wa nuklia, lakini amefeli kuwashawishi Marekani

Mwanzoni mwa mwezi huu, maofisa wa Korea Kaskazini walikutana na maofisa wa Marekani nchini Sweden huku ikiwa ni mara ya kwanza tangu Rais Trump na Kim walipokutana katika eneo la mpaka wa kati wa Korea juni, mwaka huu. Huku Marekani ikidai kuwa maamuzi mazuri na ya busara yalifanyika.

Kabla ya mazungumzo hayo Korea Kaskazini ilirusha aina mpya ya kombora huku ikiwa ni zoezi la 11 kwa mwaka huu. **BBC**

## Mbio za Uingereza kujitoa EU zafikia patamu

**LONDON,** Uingereza

MAKUBALIANO ya Uingereza kujitoa Umoja wa Ulaya (EU) yamefikiwa na timu za ufundi zilizofanya majadiliano kabla ya mkutano wa viongozi wa Ulaya kuanza mjini Brussels.

Waziri Mkuu wA Uingereza, Boris Johnson alituma ujumbe kwenye mtandao wa Twitter akisema: "Tumepata makubaliano makubwa mapya ambayo yataendelea kuwa na mashiko." Pande zote mbili zimekuwa zikifanyia kazi maandishi ya kisheria juu ya makubaliano hayo, lakini bado italazimu pande zote mbili za mabunge ya Uingereza na EU kuyapitisha.

Johnson na viongozi wenzake 27 wa EU wanakutana mjini Brussels katika kilele cha mazungumzo wanayotegemea yatamaliza hasira na maudhi juu ya mvutano unaoendelea kwa miaka mitatu ya Uingereza kujitoa katika umoja huo.

Hata kabla ya alfajiri, Johnson tayari alitakiwa akabiliane na vipingamizi vikubwa wakati washirika wa serikali ya Ireland ya Kaskazini waliposema hawataunga mkono pendekezo lake la kufikia muwafaka.

Johnson anahitaji msaada utakaoweza kupatikana ili kuweza kusukuma mbele makubaliano yoyote kuweza kupitishwa katika bunge lililogawanyika.

Kwa mujibu wa shirika la habari la AP mkutano huo uliongeza wasiwasi mkubwa, wakati nyaraka za masuala ambayo yalikuwa hayajapatiwa ufumbuzi juu ya kujitoa Uingereza yakibakia kutoeleweka.

Kamati ya ufundi inayojadili mara nyingine ilikutana juzi kurekebisha sheria za kodi ya forodha na mauzo ambazo zitaweza kudhibiti bidhaa katika biashara kati ya Ireland Kaskazini na Ireland ambapo walikuwa wamepangiwa kuendelea na mazungumzo mpaka wakati kilelele cha mkutano huo utakapofunguliwa.

Iwapo makubaliano yatafikiwa wakati wa mkutano huo wa siku mbili, Johnson anatarajia kuwasilisha katika Bunge la Uingereza makubaliano hayo katika kikao maalumu kinachotarajiwa kufanyika kesho kutwa. **VOA**



Mradi mpya wa reli ya kisasa uliozinduliwa na Rais Uhuru Kenyatta unaounganisha Nairobi na Susua. **PICHA: AFP**

## Erdogan aitupa barua ya Trump jalalani

**ANKARA,** Uturuki

RAIS wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan aliitupa barua ya Rais wa Marekani Donald Trump katika pipa la taka.

Katika barua hiyo ilioandikwa Octoba 9, mwaka huu na kutumwa baada ya vikosi vya Marekani kuondolewa Syria, Rais Trump alimweleza Erdogan: "Usijifanye kuwa na nguvu. Usiwe mpumbavu!"

Vyanzo vya ofisi ya Rais wa Uturuki vimeiambia Shirika la utangazaji la BBC kuwa barua hiyo ilimkasirisha sana Rais Erdogan.


Siku ambayo barua hiyo ilipokelewa, Uturuki ilianza operesheni yake dhidi ya vikosi vya Kikurdi katika eneo la mpakani.

"Wacha tufikie mpango mzuri! Bilashaka hutaki kuhusika na mauaji ya maelfu ya watu, na mimi pia sitaki kuhusika na uharibifu wa uchumi wa Uturuki - na nitafanya hivyo," alisema Rais Trump katika barua hiyo na kuongeza:

"Historia itakuhukumu kwa haki ukishughulikia suala hili kwa njia ya kibinadamu.



Erdogan



Trump

Itakuhukumu daima kama shetani kwa maovu," alisema Rais Trump.

Katika majibu yake, vyanzo katika ofisi ya Rais Erdogan vilisema: "Rais Erdogan alipokea barua, na kupinga vikali yaliomo na kuitupa kwenye pipa la taka."

Rais Trump amelaumiwa vikali kwa kuwaondoa wanajeshi wa Marekani nchini Syria huku wakosoaji wakisema kuwa hatua hiyo iliipatia Uturuki nafasi ya kuanzisha mashambulizi ya kijeshi nchini humo.

Katika hatua isiokuwa ya kawaida, wabunge 129 wa chama cha Republican katika bunge la uwakilishi waliungana na wenzao wa chama cha Democratic kupiga kura ya kupinga uamuzi huo.

Azimio hilo la pamoja ambalo pia lilimtaka Rais Erdogan kukomesha mara moja operesheni ya kijeshi dhidi ya vikosi vinavyoongozwa na wapiganaji wa Kikurdi, lilipitishwa kwa kura 354 - 60.

Spika wa Bunge la Marekani, Nancy Pelosi pia alikutana na Rais Trump, kujadili suala hilo katika mkutano uliokumbwa na majibizano makali yaliyochangia yeye na kiongozi wa wachache katika Bunge la Seneti, Charles Schumer, kuondoka katika chumba cha mkutano huo.

Mapema siku ya Jumatano Rais Trump, alisema Marekani haitaingilia kati operesheni ya kijeshi ya Uturuki nchini Syria, kwa sababu nchi hiyo sio mpaka wake, kuongeza kuwa Wakurdi ambao walikuwa washirika wao wa zamani sio malaika. **BBC**

# Dar kinara darasa la saba miaka mitatu mfululizo

**Na Beatrice Moses**

MKOA wa Dar es Salaam umeendelea kuwa kinara kwenye matokeo ya Taifa wa darasa la saba kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2017.

Kwa mujibu wa taarifa kuhusu ufaulu wa watahiniwa katika Mtihani wa kumaliza elimu ya Msingi (PSLE 2019) kwa kuzingatia umiliki wa shule iliyotolewa na Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), Mkoa wa Dar es Salaam ni kinara, huku Mkoa wa Mara ukiwa umeshika nafasi ya mwisho.

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Hamisi Lissu, alisema mafaniko hayo yametokana na moyo wa upendo, kujituma na kujitolea kwa walimu husika.

"Tumepata ufaulu wa asilimia 93.28 waliofaulu ni 69,907 kati ya waliosajiliwa kufanya mtihani huo 74,940 katika shule 648 zilizopo mkoani hapa," alisema Lissu.

Alisema katika idadi hiyo ya wanafunzi waliofaulu wavulana waliofanya mtihani huo ni 35,936 waliofaulu ni 33,561 na wasichana walikuwa 39,004, waliofaulu ni 36,346.

Lissu alibainisha jumla ya wanafunzi waliosajiliwa kufanya mtihani huo mkoani humo ni 75,539 kati yao wanafunzi 599 hawakufanya mtihani kwa sababu mbalimbali, kati yao wavulana walikuwa 370 na wasichana ni 229.

" Kutokana na matokeo haya mazuri, tumejipanga kuwapongeza walimu wetu wamefanya kazi kubwa , tumeongeza kiwango cha ufaulu tofauti na tulivyotarajia tuliamini tungepata ufaulu wa wastani wa asilimia 92 kama tulivyopata mwaka jana tulipata asilimia 92.6," alisema Lissu.

Katika matokeo ya mwaka huu Lissu alisema wamefanikiwa kwenye wilaya 10 zilizofanya bora, Dar es Salaam imeingiza wilaya mbili ambazo ni Kinondoni imeshika nafasi ya tatu ikitanguliwa na Arusha iliyoshika nafasi ya kwanza, Ilemela (ya pili) na Ilala imeshika nafasi ya tatu ikifuatia Mwanza jiji iliyoshinda nafasi ya nne.

"Japo hakuna shule yetu iliyoingia kwenye 10 bora, lakini bado tumefurahi miongoni wanafunzi 10 bora kitaifa wa tatu ni wetu alikuwa anasoma Shule ya msingi ya Mbezi ambayo ni ya Serikali," alisema.


Taarifa hiyo ya Nacte inaonesha Mkoa wa Mara umeshika nafasi ya 26 mwaka huu na mwaka jana ikionyeshwa kuwa na ufaulu wa asilimia 69.74, ikiwa na jumla ya watahiniwa 51,145 wavulana 25,693 na wasichana 25,452 waliofaulu ni 35,668 miongoni mwao wavulana ni 19,072 na wasichana 16,596.

Mkoa wa Mara shule umeingiza shule mbili kwenye shule10 bora zilizotoa wahitimu waliofanya vyema kwenye mtihani huo, shule hizo ni Graiyaki ilishika nafasi ya kwanza wakati ya pili ilishikwa na Twibhoki zote za mkoani humo, nafasi ya tatu imeshikwa shule ya Kemebos mkoa wa Kagera .

Kwa mujibu wa NECTA, matokeo hayo Mkoa wa Arusha ndiyo umeshika namba mbili mwaka huu kwa kuwa na ufaulu wa 91.67, hivyo kusogea kutoka kwenye nafasi ya 3 iliyoshika mwaka jana hatua ambayo imeutoa Mkoa wa Geita ulikuwa ukishikilia nafasi ya 2 mwaka jana hadi nafasi ya 14 mwaka huu kwa kuwa na ufaulu wa asilimia 79.12.

Nafasi ya tatu imeshikwa na Mkoa wa Iringa ambayo ina ufaulu wa asilimia 88.53 ambao mwaka jana ulikuwa nafasi ya 7,

Oktoba 15, 2019 NECTA ilitangaza matokeo ya kumaliza elimu ya msingi mwaka 2019 ikibainisha kuwa asilimia 81.50 ya watahiniwa 933,369 wamefaulu mtihani huo huku watahiniwa 909 wakifutiwa matokeo kwa sababu ya udanganyifu.



Ofisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Hamisi Lissu, akizungumza jijini humo jana, jinsi mkoa huo ulivyoongoza kwenye matokeo ya jumla ya Mtihani wa Darasa la Saba yaliyotangazwa na Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania (NECTA), kwa miaka mitatu mfululizo kuanzia mwaka 2017. **PICHA: BEATRICE MOSES**

# Shule za msingi kunolewa Kiingereza

**Na Mwandishi Wetu**

UTAFITI umebaini Watanzania wengi, hata waliohitimu vyuo vikuu, hawajiamini kuzungumza Kiingereza sanifu na fasaha mbele za watu, bila kukwamakwama kutokana na kutokujengwa katika misingi imara ya lunga ya hiyo tangu walipokuwa watoto.

Kwa kutambua changamoto hiyo, Taasisi ya Kiingereza ya British Council, imeanzisha kozi maalum kwa ajili ya watoto wa shule za msingi, ili kuwajengea msingi imara wa Kiingereza ili waweze kuzungumza Kiingereza kwa kujiamini.

Akizungumzia kuanzishwa kwa kozi hiyo kwa vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, Mratibu wa Mafunzo hayo wa British Council, Doris Likwelile, alisema mafunzo hayo yataanza kesho na yatakuwa yanafanyika kila siku za Jumamosi, ili kuwawezesha wanafunzi wengi wa shule za msingi kuhudhuria.

Wazazi wamehimizwa kujitokeza kwa wingi kuandikisha watoto wao, wafunzwe Kiingereza na wataalamu wabobezi wa lugha hiyo.

British Council ni shirika lisilo la kiserikali la mafunzo ya Kiingereza, liko katika nchi zaidi ya 60 duniani.

# Kigogo sekta binafsi matatani

INATOKA UK. 3

ripoti hiyo ilionyesha kuwa Kampuni hiyo ina upotevu wa zaidi ya Sh. bilioni 54.

Awali akiwasilisha ripoti ya ukaguzi huo, Mkaguzi wa Ndani Mwaandamizi Wizara ya fedha na Mipango, Idrisa Ally, alieleza kuwa ukaguzi huo ulianza Januari 22, hadi Februari 22 mwaka huu ambapo ulihusisha mwaka 2008 hadi 2018.

Ally alieleza kuwa kazi ya ukaguzi huo ulilenga kuangalia miamala ya Shirika la Hifadhi ya Jamii (NSSF), wakulima na fedha za Saccos ya wakulima hao sambamba na kuangalia mikataba iliyoingiwa na pande zote tatu.

Alieleza kuwa katika ukaguzi huo, zaidi ya Sh. bilioni 54 hazikufahamika zilipo ama matumizi yake yakiwamo madeni ya wakulima, makato ya wanachama wa NSSF, mkopo na kutolipwa kwa kodi ya serikali kwa mujibu wa taratibu.

Mkaguzi huyo alieleza yaliyojitokeza katika ukaguzi huo ni pamoja na madeni ya wakulima Sh. bilioni 29.8 ambazo hata hivyo alieleza hazikuonyeshwa kwenye taarifa za kampuni hiyo kiasi cha Sh. bilioni 1.7 za makato waliyokatwa wakulima huku Sacos ya wakulima ikiidai kampuni hiyo Sh. milioni 5.55.

Hata hivyo, ripoti ya mkaguzi huyo ilionyesha fedha zinazodaiwa na kampuni hiyo kwa wakulima ni zaidi ya Sh. bilioni 2.8.

Baada ya ripoti hiyo kuwasilishwa kwenye mkutano huo na Mkuu wa Mkoa kutoa nafasi kwa pande zote kujieleza ndipo mmiliki wa kampuni ya Katan Ltd, Salum Shamte kusimama na kukanusha ripoti iliyowasilishwa akidai haina usahihi zaidi na kwamba hawakushirikishwa katika kuiandaa.

Shamte alieleza kuwa wao kama walezi wa wakulima tangu mwaka 1999 walikuwa wakiendesha kilimo cha mkataba wa kibiashara baina yao bodi ya mkonge na wakulima.

"Hakuna mkulima anaeibiwa kwani sisi zote lengo letu ni kuinua zao la mkonge kwa kuwanufaisha wakulima hivyo mheshimiwa mwenyekiti (RC) ripoti hii haikuhusisha walengwa yaani Katan Ltd, hivyo naomba ipitiwe upya kwa kushirikishwa," alisisitiza Shamte.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### VIWANJA / MASHAMBA

**SHAMBA LINAUZW**A, Hekari 25@Tshs 800,000/= ziko Miono Kijiji cha Mkange Wilaya ya Chalinze (kuelekea Sadani Game Reserve) mwendo dakika 40 toka barabara kuu iendayo Tanga. Wasiliana na 0713 604049 / 0784 604049.


## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0767 223311**


### CHETI KIMEPOTEA



**NANCY ONESMO** wa Kona ya Bwiru, Mwanza anatangaza kupotelewa na Cheti cha kuhitimu Kidato cha Nne chenye Index Number S.0578/0055 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa mwaka 2012 katika Shule ya Sekondari TAQWA.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kwenye kituo cha Polisi kilicho karibu.

Taarifa ya Polisi:
**MW/KIR/RB/360540/2019.**

115465902

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO….. OF 2019
In the matter of the Estate of the late NOEL MICHAEL MASAKA
AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ISAKA MICHAEL MASAKA.

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the …….. Day of ………. 2019.

Dated at Dodoma this 2ND day of October, 2019.

……………………………………………….
PETITIONER
Presented of filling this ……9……… day of ……October……………2019.

115466102

---

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KEVIN RAPHAEL MZELELA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 255 APD TOYOTA LAND CRUISER. Chassis No. JTELB71J707044779.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DAR/OST/RB/389078/2019.**

115465102

---

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**JASIMINE ABDUL CHEGAMILA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NO **T910 BYG** SCANNIA. ENGINE NO **6004180.** CHASSES S **NO 4435911.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI.
**ARU/ARU/RB/383059/2019.**

115466702

---

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MICHAEL HERMENT MREMA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 462 BMR TOYOTA PRADO. Chassis namba RZJ95-0049398.


Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Control No. 9910810299494.

215466102

---

### KUPOTEA KWA CHETI



**EDICKO DAMAS BARAGULA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S3813-0013 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2014 katika Shule ya Sekondari Bwafuma.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.
**Polisi Taarifa: 2373/2019.**

115464302

---

**IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF MOROGORO**

**DISTRICT AT MOROGORO**

**PROBATE AND ADMINISTRATION**

**CAUSE NO…..6…..OF 2019**

**In the matter of the Estate of the late…**
**LETTER OF ADMINISTRATION**

**BY 1.EVA IBRAHIMU DAGLAS**
**2………………**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant of probate (or letter of administration) is made to the above- named petitioner.

Objection to the grant should be filed on or before the 28 day of ….10…2019

**Dated MOROGORO this.. 17…day of …10…2019**

115466602

---

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**PATRICK NYALANDO KASSERA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 672 CYK TOYOTA HIACE.** Chassis **No. TRH2140001634.** Engine No. **2TR0084478.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**DAR/KIJ/RB/389198/2019.**

115465702

---

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**NYANZA HAULLIER** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 671 BBR TRUCK IVECO.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**DAR/KIJ/RB/389198/2019.**

215465602

---

### KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GEORGE J KALESI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili MC 851 BPC aina ya KINGLION rangi nyekundu Chassis namba I7GPCKLYOGFO79826.


Yeyote atakayeionaatoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu.

Taarifa ya polisi
**MBE/MBE/RB/384979/2019.**

115466202

---

### KUPOTEA KWA CHETI



**JOHNSON JOEL KAMANDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0387-0073 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2013 katika Shule ya Sekondari Karagwo.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: **AR/RB/6100/2019**

115464902

---

THE UNITED REPUBLICK OF TANZANIA
SUMMONS FOR ORDERS
IN THE DISTRICT/RESIDENT MAGISTRATES COURT OF MONDULI
AT MONDULI

CIVIL CASE NO 02 OF 2019
MESHARCK POTARI LOOMU …………………PLAINTIFF
Versus
NAISHIYE SAMSON LEMUKA…………………DEFENDAT(s)

To: NAISHIYE SAMSON LEMKA
TERRAT- MURIET
ARUSHA

**SUMMONS FOR ORDERS**

WHERE AS the above names plaintiff(s) has/have instituted a suit against upon the claim, the particulars of which set out in the annexed copy of the plaint.

**YOU ARE HEREBY NOTIFIED** that you must file your **WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE** in duplicate within 21 days of services of this notice upon you. If there are more plaintiffs than one additional copies of your Written Statement of Defence must be field sufficient for service on each of the plaintiffs. If there are more defendants than one and the defence is not a joint defence must be filed sufficient for service on each of the other defendants.

**TAKE NOTIC**E that this case has been fixed mention on TUESDAY the 12 day of NOVEMBER 2019 at 09:00 am O'clock in the noon.

**AND TAKE FURTHER NOTICE** that if you default in filing of the Written Statement of Defence within the time specified the Court may pronounce judgment against you.

**GIVEN** under my hand and the Seal of the Court this 15th day of OCTOBER 2019

215464802

---

### KUPOTEA KWA KADI

**MOREEN KAALE**
Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili MC.357 BFF aina ya SUNLG.

Yeyote atakaiona atoe taarifa katika kituo cha polisi kilichopo jirani yake.

Taarifa ya Polisi:
**KAH/RB/TR/819/2019.**

215465002

---

### KADI YA GARI IMEPOTEA

**NYANZA HAULLIER** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 639 CCH STRALIS.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi:
**DAR/KIJ/RB/389198/2019.**

215465002

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO
Usimamizi wa mirathi No;208/2019
Ombi la JACKSON JULIUS MWANJA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu MARY ABEL MLEWA

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 19/11/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 17/10/2019

115465402


**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# UTD KUIPIKU REAL USAJILI WA MBAPPE



**PARIS,** Ufaransa

KLABU ya Manchester United imeripotiwa kuwa na mpango wa kuwapiku Real Madrid na Barcelona kwenye mbio za kumsajili nyota wa PSG, Kylian Mbappe, kwa mujibu wa Gazeti la Marca na nchini Hispania.

Rais wa Real Madrid, Florentino Perez amekuwwa akimuwania Mbappe kwa udi na uvumba na mpango wake ni kuhakikisha anainasa saini ya mshambuliaji huyo wa timu ya Taifa ya Ufaransa.

Gazeti la Marca limebainisha kwamba, Madrid mpango wao wa kwa Mbappe ni kumsajili kipindi cha majira ya joto cha mwaka 2021. Mpango wa Madrid kumsajili Mbappe kipindi hicho ni kwa sababu mkataba wake utakuwa umebakiza mwaka mmoja tu kufika mwisho.

Perez anataka kutumia ujanja kama ule aliotumia kuwanasa Thibaut Courtois na Eden Hazard aliposubiri hadi kwenye mwaka wa mwisho wa mikataba yao.

Lakini, sasa kwenye mbio hizo za Mbappe, Madrid watajiweka kwenye hatari ya kuzidiwa kete na timu nyingine wakiwamo Man United.

Man United wanahitaji kusajili wachezaji watakaoleta pesa kikosini na hilo watacheki hali ya kiwango chao kitakavyokuwa hadi kufika mwaka 2021.

# Vidic: Sitawasahau Drogba, Aguero

**LONDON,** England

NEMANJA Vidic ametaja washambuliaji wanne waliokuwa wakimnyima usingizi kabla ya kwenda kuwakabili, lakini hakumtaja mshambuliaji wa zamani wa Liverpool kwa wakati huo, Fernando Torres.

Torres alionekana kumsumbua Vidic kwenye mechi kadhaa za Liverpool na Man United, lakini beki huyo wa Serbia hakumtaja mshambuliaji huyo wa Hispania na kuonyesha kwamba hakuwa mtu aliyekuwa akimsumbua uwanjani.

Vidic amewataja washambuliaji Peter Crouch, Didier Drogba, Sergio Aguero na Luis Suarez hao ndio waliokuwa wakimtesa alipokutana nao uwanjani.

"Shughuli yangu ya kwanza ilikuwa Peter Crouch. Nilikuwa sijawahi kumkaba mshambuliaji mwenye kimo cha mita mbili," alisema Vidic.

Alikuwa Liverpool na tulicheza nao kwenye mechi moja ya kombe huko Anfield na nilijisemea mwenyewe 'Wow, nitafanyaje na huyu mtu leo? Kisha nikamwona Bellamy pembeni yake, si mchezaji bora sana akiwa na mpira, ila alikuwa na kasi sana. Anakimbilia kwenye nafasi na Crouch akiruka juu ni balaa. Sijawahi kuona mchezaji wa aina hii."

Kisha Vidic alimtaka Drogba, akisema straika huyo wa Ivory Coast alikuwa mjanja sana akiwasoma mabeki na kisha kutumia nafasi anayopata. Huku kwa Aguero, Vidic alisema: "Nilicheza na Aguero kwenye mechi ambayo tulipigwa 4-1 tukiwa na David Moyes.

"Aguero alivyo, haonekani kama anajali sana mpira anapokuwa uwanjani. Haonekani kama ni mtu anayeweza kukimbia mita 10, lakini jamaa yupo fasta sana. Ni mgumu sana kumkaba."





# *Emery kutosajili Arsenal Januari*

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Unai Emery amesema kwamba wala hatarajii kuongeza mchezaji yeyote kwenye kikosi chake wakati dirisha la usajili la Januari litakapofunguliwa.

Kocha huyo raia wa Hispania alishuhudia timu yake ikifanya usajili mkubwa kwenye dirisha lililopita la majira ya joto, hivyo haoni kama kuna ulazima wa kusajili tena Januari ambapo kwa sasa anajaribu kukiweka sawa kikosi chake kuwa cha kiushindani zaidi.

Emery kwenye dirisha lililopita aliwanasa Kieran Tierney, Nicolas Pepe, David Luiz, Dani Cebalos na kuingia moja kwa moja kwenye kikosi cha kwanza na kisha kuwandoa wengine.

Kikosi chake kimeanza vema kwenye Ligi Kuu England, kikishika nafasi ya tatu kwa sasa, huku kikiwa kimepoteza mechi moja tu walipocheza na Liverpool, ambao kwa sasa ndio vinara.

Mjadala ambao umekuwa ukiibuka kwenye kikosi hicho cha Arsenal ni kuhusu mabao, kwamba wamekuwa dhaifu licha ya timu kuwanasa Tierney na Luiz, huku William Saliba akijiandaa kutua rasmi kwenye kikosi hicho cha Emirates.

Kwenye dirisha la Januari, biashara pekee ambayo kocha Emery anaweza kuifanya ni kumfungulia mlango wa kutokea kiungo wake matata kabisa, Mjerumani Mesut Ozil, anayelipwa mshahara wa Pauni 350,000 kwa wiki na mpango ni kumtoa kikosini hata kwa mkopo.

## HABARI MICHEZO



# MESSI AKABIDHIWA KIATU CHA DHAHABU CHA SITA

**BARCELONA,** Hispania

LIONEL Messi amekabidhiwa Kiatu cha Dhahabu kwa mara ya sita, na kuendeleza rekodi yake nyingine kwenye Ligi Kuu ya Hispania, La Liga, juzi Jumatano.

Messi alitwaa tuzo hiyo, ambayo anapewa mchezaji ambaye amefunga mabao mengi zaidi kati ya ligi tano kubwa Ulaya, ambapo yeye alifikisha mabao 36 katika mechi 34 alizocheza kwenye La Liga msimu wa 2018-190.

Jitihada zake ziliisaidia Barca kutetea taji la La Liga na kutwaa Kiatu cha Dhahabu kwa msimu wa tatu mfululizo.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina alikuwa pamoja na watoto wake wakati akikabidhiwa kiatu hicho cha dhahabu jijini Barcelona, ambapo watoto wake wa kiume, Thiago na Mateo walipewa nafasi ya kumkabidhi.

"Ni kitu muhimu zaidi kwenye mashindano. Kama hauko poa kwenye mashindano, itakugharimu kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya," alisema Messi wakati akikabidhiwa tuzo hiyo.

"Asanteni wote. Familia yangu, makocha, wachezaji wenzangu, wote mlionisaidia mimi kuwa hapa leo."

Akiwa na tuzo ya sita ya Kiatu cha Dhahabu kwa jina lake, Messi amemzidi mara mbili Cristiano Ronaldo, ambaye ametwaa tuzo hiyo mara nne, kwa mara ya mwisho kuibeba ikiwa ni msimu wa 2014-15.

Messi amekuwa na wakati mgumu kwa msimu huu kutokana na majeraha na amefunga bao moja tu hadi sasa msimu huu.

# *AS Roma sasa yaanza rasmi kutumia Kiswahili*

**ROME,** Italia

AS Roma ya nchini Italia imekuwa klabu kubwa ya kwanza kutoka barani Ulaya kuanzisha ukurasa wake katika mtandao wa kijamii wa Twitter kwa kutumia lugha ya Kiswahili.

Ukurasa huo wa lugha ya Kiswahili ulizinduliwa rasmi juzi Jumatano na inaaminika lengo kuu la AS Roma ni kuwafikia mamilion ya mashabiki wake wanaotumia lugha ya Kiswahili.

Katika ukurasa wake huo wa Twitter, AS Roma iliandika: "Ni rasmi sasa; Ukurasa wa lugha ya Kiswahili umefunguliwa rasmi. Karibuni sana."

Akaunti hiyo iliwekwa video yenye maneno ya utani ya Kiswahili na imeonekana kupokelewa vizuri na wasomaji wa Kiswahili wa Tanzania na nchini Kenya ambao walitoa maoni yao mbalimbali.

Wengi wakiona kuwa ni ubunifu mzuri ambao unaonyesha kuwajali mashabiki wanaoongea lugha ya Kiswahili.

"Aisee nyie jamaa mmekuwa wabunifu kupata mashabiki Waswahili. Kongole kwa hilo," aliandika mmoja wa wasomaji Raymond Nyamwihula, @Nyamwihularay.

Rais wa Klabu ya AS Roma, Jim Pallotta ametumia ukurasa wake binafsi wa twitter kuthibitisha kuwa kurasa hiyo imefunguliwa. Ujumbe wa Twitter wa @jimpallotta13: Niliwaambia! Karibu Twitter @ASRomaSwahili Tufurahi pamoja sasa. #ForzaRoma Hakimiliki ya Picha @jimpallotta13@ JIMPALLOTTA13



"Tuna furaha kuzindua kurasa ya Kiswahili ya AS Roma", mkuu wa mipango Paul Rogers alieleza.

Uzinduzi huu umekuja baada ya maombi ya mashabiki kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Afrika ya Kati na mataifa mengine ya Mashariki na Kusini mwa Afrika.

# Aguero apata ajali ya gari

**MANCHESTER,** England

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Sergio Aguero, ameripotiwa kupata ajali akiwa njiani kuelekea mazoezini akiwa na gari yake binafsi aina ya Range Rover.

Gari hiyo ya Aguero imetajwa kuwa na thamani ya pauni 150,000 (sawa na zaidi ya Sh. milioni 430).

Aguero raia wa Argentina ambaye hakuwa sehemu ya kikosi cha timu ya taifa kilichokusanyika kucheza michezo ya kirafiki iliyopo katika Kalenda ya Fifa, alipata ajali hiyo akiwa njiani kuelekea mazoezini, lakini hakuumia.

Hii si mara ya kwanza kwa Aguero kupata ajali ya gari, kwani aliwahi kupata mwaka 2017 akiwa jijini Amsterdam nchini Uholanzi alipokuwa amekwenda kwa ajili ya kuangalia shoo ya msanii wa Argentina, Maluna.

Msanii huyo alikuwa anafanya tamasha la muziki nchini Uholanzi, na wakati Aguero anarudi kuelekea uwanja kwa taxi aliyokuwa amepanda, ikaacha njia na kugonga nguzo na alipata majeraha madogo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA, DE GEA RASMI SASA KUIKOSA LIVER

## Paul hatacheza mchezo huu, ila natumai Aaron na Anthony watakuwa tayari kuchaguliwa...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anatarajia kuwakosa wote kwa pamoja David De Gea, Jesse Lingard na Paul Pogba katika mechi ya Ligi Kuu England Jumapili dhidi ya Liverpool kutokana na kuwa majeruhi.

**De Gea alilazimika kutoka nje ya uwanja wakati akichezea Hispania kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 dhidi ya Sweden Jumanne wiki hii kwa kile kilichoonekana kama ni tatizo la nyonga.**

"David anahitaji kufanyiwa vipimo vya kina," Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer aliiambia Sky Sports. "Nadhani atakuwa nje. Kwa kweli ilionekana kama kawaida kuhukumu kuhusu usiku wa juzi kwa hivyo ni moja tu ya vitu hivyo."

Kukosekana kwa De Gea ina maana Sergio Romero ataanza mechi ya ligi kwa mara ya kwanza msimu huu kutokana na Muargentina huyo kucheza mechi za Europa League na Kombe la Ligi ['Carabao Cup'] pekee hadi sasa msimu huu.

Mhispania huyo anaungana na Pogba na Lingard chumba cha majeruhi na Solskjaer amesema wawili hao "hakuna nafasi" ya kuwa fiti kucheza.

Pogba amekuwa nje ya uwanja katika mechi tano kati ya saba zilizopita za United kutokana na matatizo ya kifundo cha mguu, na baada ya kutumia sehemu ya mapumziko ya mechi za kimataifa kufanyia kazi matibabu yake huko Dubai, Solsjkaer alifunguka kuwa kiungo huyu wa Ufaransa amepata shida.

Kocha huyo wa United aliongeza: "Paul alikuwa na majeraha, alirudi, alijitahidi sana. Alirudi na kucheza mechi mbili, pengine alicheza akiwa na maumivu makubwa.

"Alifanyiwa vipimo baada ya mechi dhidi ya Arsenal na pengine anahitaji wiki chache za kupumzika kujiimarisha, hivyo natumai haitachukua muda mrefu sana, lakini hatacheza mchezo huu, hapana."

United imeshinda mechi mbili tu katika nane za ligi za mwanzoni mwa msimu na inashika nafasi ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa ni ponti mbili juu ya ukanda wa kushuka wa daraja, na taarifa ya De Gea kujiunga na Pogba katika orodha ya majeruhi kunaendelea kuufanya msimu kuwa wa utata kwao.

Hata hivyo, Anthony Martial, Luke Shaw na Aaron Wan-Bissaka wanatarajiwa kulazimishwa kurejea wakitokea chumba cha majeruhi, na Solskjaer amethibitisha: "Siwezi kukuambia kwa asilimia 100 [nani] atakuwa fiti kama kitu fulani kinaweza kutokea.

"Lakini natumai Aaron na Anthony watahitimisha mazoezi wiki hii na kuwa tayari kwa kupata nafasi ya kuchaguliwa kucheza. Kama ni kwa nusu saa ya mchezo ama dakika 30 sijui bali ngoja tuone ni wapi."

## ZISIKUPITE

### ISCO KUMRITHI ERIKSEN SPURS

TOTTENHAM inaweza kuziba pengo la kiungo Mdenmark Christian Eriksen, 27, kwa kumsajili kiungo wa Real Madrid, Mhispania Isco, 27, katika dirisha la usajili la Januari. ***(El Desmarque, via Express)***

### YASHIKILIA REKODI KADI

CHELSEA imetangazwa rasmi kama klabu yenye rekodi mbaya zaidi ya nidhamu kwenye Ligi Kuu England, kutokana na kutokuwapo kwa klabu yenye kadi nyingi zaidi kwenye ligi hiyo tangu mwaka 1992. ***(Star)***

### OZIL AIGOMEA ARSENAL

KIUNGO wa Arsenal, Mesut Ozil, 31, amesisitiza hataondoka klabuni hapo, wakati huu mkataba wa nyota huyo wa zamani wa kimataifa wa Ujerumani ukitarajiwa kumalizika mwaka 2021. ***(Athletic)***

### ALLEGRI KUTUA NA CAN UTD

KOCHA wa zamani wa Juventus, Massimiliano Allegri anaweza kutua na straika Mcroatia Mario Mandzukic, 33, na kiungo Mjerumani Emre Can, 25, hapo Manchester United kama atateuliwa kurithi mikoba ya Ole Gunnar Solskjaer Old Trafford. (***Tuttosport, via Express)***

### KROOS, POGBA KUPISHANA

MANCHESTER United inataka kumsajili kiungo Mjerumani Toni Kroos, 29, kutoka Real Madrid, ambaye anaweza kutoa nafasi ya kufanyika mazungumzo ya kiungo Mfaransa Paul Pogba, 26, kutua upande wa pili kama sehemu ya kubadilishana. ***(Bild, via Sun)***

### VAZQUEZ AWAHIWA ARSENAL

ARSENAL imeripotiwa kutoa ofa kwa winga wa Real Madrid, Mhispania Lucas Vazquez, 28, kabla ya uwezekano wa kumfuata dirisha la usajili la Januari. ***(El Desmarque, via Football.London)***

### KUMRITHI SANCHEZ INTER

INTER Milan inazingatia mpango wa kumfuata mshambuliaji wa Chelsea na Ufaransa, Olivier Giroud, 33, kwa sasa kutokana na straika wa kimataifa wa Chile, Alexis Sanchez, 30, anayeichezea klabu hiyo ya Italia kwa mkopo akitokea Manchester United, kukabiliwa na kuwa nje ya uwanja kwa muda mrefu akiuguza majeraha ya kifundo cha mguu. (***Calciomercato, via Express)***

### KOMPANY AIPONZA ANDERLECHT

ANDERLECHT imepigwa faini ya pauni 4,300 na Chama cha Soka cha Ubelgiji kwa kitendo cha kumteua beki wa zamani wa Manchester City, Vincent Kompany, 33, kuwa kocha wao mkuu wakati hana taaluma hiyo ya ukocha. ***(Sun)***

### AGUERO AANGUSHA RANGE

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Muargentina Sergio Aguero, 31, aliiangusha Range Rover yake yenye thamani ya pauni 150,000 wakati akiwa njiani kuelekea mazoezini, lakini aliendelea na safari yake bila matatizo. ***(Mail)***

### DEMBELE, NIGUEZ KIPORO UTD

MANCHESTER United itasainisha wachezaji sita katika madirisha mawili ya usajili yajayo, akiwamo Moussa Dembele kutoka Lyon, kiungo wa Atletico Madrid, Saul Niguez na nyota wa Leicester City, James Maddison. ***(Mail)***

## Pete Daraja la pili kurindima Moro

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya mpira wa pete (Netball) Ligi Daraja la Pili, yanatarajiwa kuanza kurindima Septemba 25, mwaka huu mkoani Morogoro, imeelezwa.

Akizungumza na Nipashe juzi, Mwenyekiti wa Chaneta, Devota Marwa, alisema mashindano hayo yatashirikisha timu kutoka mikoa yote nchini.

"Maandalizi kwa ajili ya mashindano hayo yanaendelea vizuri, tunaomba wadau mbalimbali wajitokeze kuyaunga mkono," alisema Devota.

Aidha, mwenyekiti huyo alisema mashindano hayo yatasaidia vijana kupata uzoefu zaidi ili kuwasaidia kuinua vipaji vyao.

"Haya mashindano yatazidi kuinua vipaji vya vijana pamoja na kuutangaza mchezo huu ili urudishe hadhi yake ya miaka ya nyuma," alisema mwenyekiti huyo.

## Babu Seya, Papii Kocha jukwaani

**Na Steven William,** MUHEZA

MWANAMUZIKI Papii Kocha "Mtoto wa Mfalme" kwa kushirikiana na mkongwe wa muziki nchini, Nguza Viking maarufu, Babu Seya wanatarajiwa kushusha burudani ya kukata na shoka wilayani Muheza na Korogwe mkoani Tanga baadaye mwezi huu.

Shoo hizo mbili zilizoandaliwa na mfanyabiashara maarufu wilayani Muheza, Teddy Elieti kwa lengo la kuwaburudisha wakazi wa wilaya hizo mbili, zitaanzia Muheza Oktoba 25, mwaka huu kabla ya kesho yake wanamuziki hao kwenda kufunga kazi Korogwe.

Elieti alimwambia mwandishi wetu kuwa Nguva Viking maarufu Babu Seya kwa kushirikiana na mwanawe, Papii Kocha wameahidi kushusha burudani ya nguvu na kuwataka wakazi wa Muheza, Korogwe na Tanga kwa ujumla kujitokeza kwa wingi na wasingoje kuhadithiwa.

Alisema mbali na tungo zao zilizozoeleka, pia wanamuziki hao watashusha nyimbo za manguli wa kali zikiwamo muondoko wa rhumba na nyinginezo kali.



# KMKM, KVZ DIMBANI Z'BAR KUSAKA POINTI 3

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Kuu Zanzibar mzunguko wa sita inatarajiwa kuendelea kutimua vumbi leo kwa kupigwa michezo miwili ambapo Mabaharia wa KMKM na Maafande wa KVZ watashuka katika viwanja viwili tofauti, Uwanja wa Amaan mjini Unguja na ule wa Gombani Kisiwani Pemba kusaka pointi tatu muhimu.

Kwa mujibu wa ratiba ya Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF), mchezo namba 41 utapigwa katika Uwanja wa Amaan ukiikutanisha timu ya Chuoni ikiwa nafasi ya nne na pointi zake saba dhidi ya Mabaharia wa KMKM wenye alama 10 na wakiwa nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo.

Nahodha wa timu ya Chuoni, Saleh Hamid, aliliambia gazeti hili mapema wiki hii kuwa wanachoangalia hivi sasa ni timu yao kuweze kutoka na ushindi pamoja na mabao mengi ili kujiweka nafasi nzuri zaidi katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar.

**Alisema wamejipanga kucheza mchezo mzuri ambao watahakikisha wanaondoka na alama tatu zitakazowafanya kusonga mbele katika ligi hiyo yenye ushindani wa hali ya juu.**

Kwa upande wa mchezo namba 42 utakaopigwa Kisiwani Pemba utazikutanisha timu ya Mwenge yenye alama nne, huku ikishikilia nafasi ya 11 dhidi ya timu ya Maafande wa KVZ ambao waliopo nafasi ya tisa kutokana na pointi zao tano.

Ligi Kuu ya Zanzibar inashirikisha timu 16 ambazo ni Zimamoto, KMKM, JKU, Jang'ombe Boys, Chuoni, Mlandege, Machoma, Machomane, Mafunzo, KVZ, Kipanga, Mwenge, Polisi, Selem View, Malindi, Jamhuri na Chipukizi.

Hata hivyo, msimu huu jumla ya timu sita zitashuka daraja kwa mujibu wa kanuni ya mashindano na zitapanda timu mbili na kuwa na jumla ya timu 12 zitakazoshiriki Ligi Kuu msimu unaokuja.



Mchezaji wa timu ya mpira wa wavu ya Kivule Klabu, Said Othuman, akipiga mpira kufunga bao wakati wakifanya mazoezi katika viwanja vya Shule ya Msingi Kivule jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## *Tanzania yaburuzwa Pooltable A. Mashariki*

**Na Focus Nicus**

UGANDA na Kenya zimeigaragaza Tanzania kwenye mashindano ya Pooltable, kwa nchi za Afrika Mashariki yaliyojulikana kama "East Africa Chinise 8 Ball Competitions 2019" yaliyo malizika mwishoni mwa wiki Nanyuki nchini Kenya.

Katika mashindano hayo ambayo Mganda Amos Ndyagumanawe alizawadiwa Sh. 50,000 za Kenya sawa na Sh. milioni moja za Tanzania kutokana na kuibuka bingwa, nafasi ya mshindi wa pili ilikwenda kwa Mkenya John Kyalo aliyeibuka na Sh. 30,000 za Kenya sawa na Sh. 600,000 za Tanzania kutokana na ushindi huo.

Nafasi ya tatu ilitua kwa Dennis Kimani kutoka Kenya ambaye alizawadiwa shilingi 20,000 za Kenya sawa na Sh. 400,000 za Tanzania, huku Collins Tuwei kutoka Kenya akijinyakulia shilingi 10,000 za Kenya sawa na Sh. 200,000 za Tanzania kutokana na kushika nafasi ya nne.

Katika mashindano hayo yaliyoshirikisha wachezaji kutoka nchi tatu tu za Afrika Mashariki, Tanzania, Kenya na Uganda, Mtanzania Abdallah Hissein (Sniper) alijitutumua na kuwabeba Watanzania kwa kutinga robo fainali ya mchezaji mmoja mmoja (Singles).

Mashindano hayo yaliyoanza Oktoba 12 hadi 13, mwaka huu, yalikutanisha jumla ya wachezaji 64 kwa udhamini wa Moran Lounge and Grill, washindi wengine walioingia nane mbali na Mtanzania Hussein, ni Henry Mwangi, David Njane na Martin Mwangi (wote kutoka Kenya) ambao kila mmoja alizawadiwa shilingi 5,000 za Kenya sawa na Sh. 100,000 za Tanzania.

Akizungumza na wanahabari, wachezaji pamoja na wadau waliojitokeza kushuhudia mashindano hayo, Mkurugenzi wa Cresports Masters Limited, James Nderitu, kwanza aliwapongeza wachezaji kutokana na ushiriki wao na kusisitiza sasa ni wakati wa kuwekeza katika mashindano hayo.

Michezo
Ijumaa Oktoba 18, 2019
Nipashe



Pogba, De Gea rasmi kuikosa Liver UKURASA 30

TOBO!...



Kiungo wa Simba, Deo Kanda, anayeicheza timu hiyo kwa mkopo akitokea TP Mazembe ya kwao, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), akijaribu kupasua katikati ya wachezaji wa Aigle Noir ya Burundi kwa kumvisha tobo mmojawapo katika mchezo wa kirafiki uliomalizika kwa sare tasa juzi kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mjini Kigoma. **PICHA: SIMBA**

# Wabrazil wa Simba watisha mchangani

●●● Ni beki Tairone na kiungo Fraga, Aussems abaki akishindwa kuamini kombinesheni ikizidi kuitika huku...

**Na Focus Nicus**

WAKATI Kocha Mkuu wa Simba, Mbelgiji Patrick Aussems akionyesha kukoshwa kutokana na kombinesheni nzuri katikati safu ya ulinzi kati ya Muivory Coast, Pascal Wawa na Mbrazil Tairone Santos kwa kutoruhusu bao katika mechi walizocheza pamoja hivi karibuni, beki huyo raia wa Brazil na mwenzake kiungo Gerson Fraga, wameacha rekodi ya kushangaza Kigoma.

**Kusajiliwa kwa Wabrazil hao katika kikosi cha Simba kuliwafanya mashabiki, wachambuzi na wadau wengi wa soka kuamini watawika tu katika Uwanja wa Taifa na wa Uhuru jijini Dar es Salaam ama wa takapocheza CCM Kirumba jiji ni Mwanza na Kaitaba mkoani Kagera kwenye viwanja vizuri, lakini juzi wakiwa Kigoma walionyesha kwamba hata mchangani wanaweza kuwika.**

Pamoja na Uwanja wa Lake Tanganyika kutotofautiana sana na viwanja vingi vya mchangani jijini Dar es Salaam kutokana na ubovu wake katika eneo la kuchezea kutokuwa na nyasi, Wabrazil hao walionyesha kiwango cha juu na kuhimili mikikimikiki ya wapinzani wao bila kuhofia kuumia.

Fraga akiwa katika dimba la kati, kama kawaida yake alikuwa akikata 'umeme' [kuharibu mipango ya wapinzani] huku uchezaji wake ukionekana kutotofautiana na baadhi ya wachezaji wa Kitanzania ambao wamezoea viwanja vibovu.

"Huyu Fraga utafikiri Mbongo, sikutarajia kuona akimudu kucheza vizuri katika uwanja mbovu kama huu hasa ukizingatia ametoka Brazil ambapo tunaamini ni moja ya nchi yenye viwanja bora vya soka duniani," alisema Hamad Miraji, shabiki aliyeshuhudia mechi kati ya Simba na Aigle Noir ya Burundi.

Shabiki mwingine aliyejitambulisha kwa jina la Karim Ramadhan, alihoji: "Hivi huyu Tairone na mwenzake ['Fraga'] kweli wametoka Brazil? Siamini macho yangu, kumbe hata mchangani wanaweza kuibeba timu! Kweli kama unajua, unajua tu."

Katika mechi ya kirafiki dhidi ya Bandari FC ya Kenya, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Ben Mwalala, alimmwagia sifa Fraga kutokana na uwezo wake wa kutibua mipango ya mashambulizi, kukaba na kutoa pasi za haraka bila kupoteza muda hali iliyowapa wachezaji wake wakati mgumu wa kujipanga.

Tairone alionyesha uwezo wakicheza na Wawa kwenye mechi mbili za Ligi Kuu Bara dhidi ya Kagera Sugar ambazo Simba walishinda mabao 3-0 kisha dhidi ya Biashara United mabao 2-0 na wakacheza kwenye mechi ya kimataifa ya kirafiki dhidi ya Bandari ambayo walishinda kwa bao 1-0 kabla ya kuonyesha uwezo tena wakati wakitoka sare tasa dhidi ya Aigle Noir ya Burundi mkoani Kigoma.

Aussems alisema mabeki hao wamekuwa wakifanya vizuri na wanaelewana kwa sasa tofauti na zamani ndiyo maana wameweza kucheza kwa muda huo bila ya kuruhusu bao lolote la kufungwa.

"Hadi sasa hatujafungwa bao kwenye mechi ambazo Wawa amecheza na Tairone, jambo zuri ni kwamba wanaendelea kucheza kwa kuelewana kwa kadiri siku zinavyokwenda, lakini hilo haliwezi kuwa sababu yao kucheza kila mechi, hapa tuna wachezaji wengi wenye uwezo wa kucheza nafasi hiyo," alisema.

## Stars ni kufa kupona Sudan

**Na Somoe Ng'itu,** KHARTOUM

KUFA au kupona! Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kuwakabili wenyeji Sudan katika mchezo wa kuwania Kombe la Mataifa kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa El Merreikh Omdurman ulioko jijini hapa.

Mechi hiyo ya marudiano, itaanza kuchezwa saa 12:00 jioni ya Sudan, sawa na saa 1:00 usiku kwa saa za Afrika Mashariki.

Taifa Stars ambayo ilishiriki fainali za kwanza za CHAN zilizochezwa jijini Abdijan, Ivory Coast mwaka 2009, itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0, katika mchezo wa kwanza uliochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jijini hapa, Kaimu Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Etienne Ndayiragije, alisema wamejiandaa kufanya vizuri katika mchezo huo wa marudiano na wanaamini leo watakuwa bora zaidi kwa sababu wanahitaji ushindi tu.

Ndayiragije alisema wamefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo, na kwamba mechi ya kirafiki dhidi ya Rwanda (Amavubi) waliyocheza Jumatatu iliyopita, ilimsaidia kukiimarisha kikosi chake na kuwapa uzoefu zaidi baadhi ya wachezaji wake wapya.

Kocha huyo raia wa Burundi alisema kuwa mchezo wa kwanza kikosi chake kilitengeneza nafasi nyingi, lakini hawakuzitumia kama wenzao walivyofanya, hivyo amewaandaa nyota wake kutorudia makosa hayo.

"Changamoto tuliyonayo ilikuwa ni kuondoa uchovu, maana tulisafiri usiku baada ya kumaliza mechi kule Rwanda, lakini sasa tunaiangalia mechi iliyoko mbele, kimbinu tuko vizuri, hata mchezo uliopita sisi ndio tulimiliki zaidi mpira, nimewaambia na kuwakumbusha kuongeza utulivu, naamini tutafanikiwa katika mechi ya kesho (leo)," alisema Ndayiragije.

Alimtaja Mohammed Hussein "Zimbwe Jr", ndiye mchezaji aliyekuwa majeruhi, lakini mazoezi ya jana usiku ndio yangeamua nafasi ya beki huyo wa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba kama atacheza au la, lakini juzi alifanya vizuri mazoezi na wachezaji wenzake.

Nahodha Msaidizi wa timu hiyo, Erasto Nyoni, alisema kuwa wako tayari kucheza "kufa au kupona" ili kuhakikisha wanaibuka na ushindi katika mechi ya leo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002